# MWONGOZO WA MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

**WAHARIRI**

- IGUNZA MWANATUNZI
- JULIDAH KEMUMA

HAKIMILIKI ©2022 NA IGUNZA MWANATUNZI

**Haki zote zimehifadhiwa**

Nakala hii hairuhusiwi itolewe kwa njia yoyote ile kama vile kuichapisha tena au kuhifadhi kwa njia ya kieletroniki wala kuitumia bila ruhusa kutoka kwa mhariri, mwandishi ama mchapishaji.

Toleo la kwanza: November 2022

Kimechapishwa na Elong'o Publishers

**ISBN: 9798571417938**

## TABARUKU

*Tabaruku iwaendee wanachama wetu wa CHAKIKA (Chama cha Kiswahili cha Kayole) kwa kutusaidia kupalilia hamu ya kuenzi na kukuza Kiswahili, bila kusahau shule ya upili ya Kayole South chini ya uongozi wa mwalimu mkuu bwana Daniel Ngari, kwa mchango wao na yeyote yule aliyechangia kwa njia moja au nyingine, pokea mkono wa tahania.*

# YALIYOMO


**TABARUKU ..... iii**

**MIHIMILI YA KUJIBU MASWALI YA FASIHI ..... 1**

**1. FADHILA ZA PUNDA -*Rachael Wangari* ..... 4**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA. ..... 12**

**2. MSIBA WA KUJITAKIA-*D. W Lutomia* ..... 14**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA. ..... 23**

**3. MAPAMBAZUKO YA MACHWEO-*Clara Momanyi* ..... 25**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 31**

**4. HARUBU YA MAISHA-*Paul Nganga Mutua* ..... 32**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 39**

**5. SABINA-Winnie Nyaruri Ogenche ..... 43**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 48**

**6. MZIMU WA KIPWERERE-*Yusuf Shoka Hamad* ..... 51**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 59**

**7. KILA MCHEZEA WEMBE-*Pauline Kea* ..... 63**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 67**

**8. KIFO CHA SULUHU-Dominic Maina Oigo ..... 68**

**MBINU NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 78**

**9. AHADI NI DENI-*Rayya Timammy* ..... 80**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 85**

**10. TOBA LA KALIA-*Douglas Ogutu* ..... 85**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 94**

**11. NIPE NAFASI-Mzamane Nhalapo ..... 95**

**MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 101**

**12. NILITAMANI-Phibian Muthama ..... 101**

**13. PUPA-F.M Kagwa ..... 111**

# MIHIMILI YA KUJIBU MASWALI YA FASIHI

## Masuala ibuka katika utahini wa karatasi ya tatu

### 1. Mbinu za kimtindo

Mbinu za kimtindo ni mbinu za kisanaa na mbinu za lugha alizotumia mwandishi katika kufanya kazi yake kuvutia zaidi kwa msomaji.

### 2. Toni katika vitabu vya fasihi andishi.

Riwaya, tamthilia na hadithi fupi pia huwa katika toni. Toni hapa huwa ni hisia za msemaji wa maneno katika dondoo.

**Toni yaweza kuwa ya;**

- Huzuni,
- Huruma,
- Uchungu,
- Masikitiko,
- Tumaini n.k.

### 3. Taswira na aina za Taswira

Taswira ni mbinu ya mwandishi kutumia maelezo yanayoleta picha halisi ya matukio yanayotukia akilini mwa msomaji.

**Aina za taswira ni kama vile;**

- **Taswira oni**(Msomaji anapata picha ya kitu kwa macho
- **Taswira Mnuso**(picha ya kitu kwa kunusa)
- **Taswira sikivu**(picha ya kitu kwa kusikia)
- **Taswira mwendo**(Picha ya kitu kwa namna ya kutembea)
- **Taswira hisi**(Picha kihisia)
- **Taswira muonjo**(Picha ya kitu kwa namna kinavyoonja)

### 4. Mbinu za kimuundo

Hizi ni kama vile mbinu rejeshi, sadfa, kisengere mbele n.k.
**Umuhimu wa mbinu hizi ni kama vile**;

- kuwajenga wahusika,
- Kuendeleza ploti na pia
- Kuendeleza baadhi ya maudhui.

5. **Aina ya urudiaji.**

- Urudiaji wa neno.
- Urudiaji wa kimaana/kiusawe.
- Urudiaji wa sauti.
- Urudiaji wa silabi.
- Urudiaji wa vipande.
- Urudiaji wa kirai/kishazi.

6. **Namna ya kujibu swali la dondoo**

- Taja msemaji
- Taja Msemewa/mzungumziwa
- Taja mandhari
- Eleza wanachozungumzia kwa ufupi

7. **Umuhimu wa mandhari**

- Kuendeleza maudhui mbalimbali.
- Kuwajenga wahusika.
- Kuwatambulisha wahusika katika hadithi.
- Kuendeleza ploti ya hadithi.
- Kuonyesha wakati.

8. **Umuhimu wa mhusika**
    - Ametumiwa na mwandishi katika kuendeleza baadhi ya maudhui katika hadithi, riwaya ama tamthilia.
    - Ametumiwa na mwandishi katika kuwajenga wahusika wengine.
    - Kupitia kwake tunafahamu madhara ya…/umuhimu wa …
    - Ametumika katika kuendeleza ploti (angalia matokeo ambayo ameyafanya ili riwaya/tamthilia/hadithi fupi kurefuka).
    - Kielelezo cha watu wenye sifa kama vile…katika jamii.
    - Ametumiwa kuwakilisha jumuiya mbalimbali (wasomi, wakombozi…katika hadithi)
    - Kielelezo cha jinsia kama vile ya kike/kiume/wanawake/wanaume katika jamii.

9. **Nafasi za mhusika**
    Hii ni namna ambavyo mwandishi amemchora au kumsawiri kiumbe fulani katika kazi yake.
    **Maagizo ya ndani**

1. Andika nambari ya swali unalojibu kulingana na karatasi ya maswali na ikiwa ina sehemu mbalimbali ziweze kuandikwa ipasavyo. Kwa mfano 1 (a), (b) au 2 (a), (b), (c) nk
2. Elewa msamiati unaotumiwa na mtunzi wa swali. Ni vyema kufuata maagizo hasa kwa kuelewa mahitaji ya swali kutegemea istilahi zilizotumiwa kuulizia maswali. Istilahi hizo ni kama vile;
   - **Eleza**: Ni kufafanua kwa kina ili kilichoulizwa kieleweke kwa uwazi iwezekanavyo.
   - **Jadili**: katika mtihani wa fasihi, jadili ni kukubaliana na hoja/kauli/msimamo fulani kwa kufafanua kwa undani hoja zinazojibia swali husika.
   - **Onyesha**: ni kueleza waziwazi kwa ithibati (ushahidi ufaao) kutokana na kazi inayorejelewa.
   - **Fafanua**: ni kuonyesha waziwazi kwa njia ya kuondoa dukuduku yoyote sawa na kueleza. Hoja zitolewe na kuelezwa waziwazi.
   - Usitumie maneno ya kukana kama vile si mrefu, si mwenye bidi.
   - Tofautisha au linganua ni kutoa pande zote mbili zinazooana.
   - **Linganisha** ni sawa na kufananisha na hapa utaweka sifa sawa/ kuonyesha usawa.

## MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

### 1. FADHILA ZA PUNDA -*Rachael Wangari*

### MTIRIRIKO

Hadithi hii inaanza huku Lilia akigutushwa saa nane usiku na mshtuko wa kumbukumbu za mumewe Luka ambaye alikuwa anampitishia hali ngumu ya maisha. Ni usiku na Luka hajarudi nyumbani na alijua kuwa angepata adhabu ya kukosa kupokea simu aliyompigia simu mchana alipokuwa akioga.

Lilia anakumbuka kujuana kwake na Luka. Luka aliingia kanisani mwao Jumapili moja na kuketi mkabala naye. Mwishoni mwa ibada, mgeni, Luka, alipewa nafasi ya kuzungumza na hapo Lilia akavutiwa naye sana, haswa sauti yake. Lilia alimwomba na kumshawishi babake kumsaidia Luka, naye akafanya hivyo. Babake Lilia alimpa kazi ya kunadhifisha mazingira ya kanisa. Luka alijiunga na shule ya msingi iliyokuwa karibu. Alikuwa mwerevu na mwepesi wa kushika mambo shuleni. Urafiki wa Lilia na Luka uliendelea kukita mizizi.

Waliingia chuoni kusoma baba mtu ambaye alikuwa akiugua alisononeshwa na uhusiano ule, akajaribu kumrai bintiye aachane nao bintiye lakini wapi? Luka alifanya kazi kanisani na matunda ya kazi yake yalidhihirika na wakaona na Lilia.

Lilia alifanya kazi ya meneja wa benki moja mjini. Ndoa ilikuwa inaenda sawa kifo kilipomwiba babake Lilia. Luka akachukua hatamu za uongozi wa kanisa na kumshinikiza mkewe kuacha kazi.

Siku moja Luka akamwambia mkewe ashachoshwa na kuhubiri. Anataka kuwa mwanasiasa. Lilia alitanabahi kanisa limeisha. Luka alikuwa tayari keshaliuza. Hakujua ilikuwa biashara ile-kazi aliyoianzisha babake. Hakuteta, alinyamaza ili kudumisha amani katika ndoa yake. Ufa wa kwanza ulidhihirika wakati wa kampeni alipomtaka Lilia kuandama naye ilhali alikuwa mjamzito wa miezi minne. Lilia alikataa. Luka alimtusi na akatoka kwa hasira. Usiku ule hakurudi. Siku ya pili majirani waliitwa kumpeleka hospitali. Madaktari walishdwa kudhibiti mimba yake.

Kama Luka alihuzunika ilikuwa kwa muda tu. Hakutaka kuwa mzazi katika kipindi cha uchaguzi. Hatimaye Luka alipata ugavana aliopania. Ulaghai sasa ndio ibada yake kubwa, ongezea uzinzi juu yake. Alipohamia katika kasri ya gavana alisahau mwenziwe. Lilia aliambiwa kuwa alihitaji kuishi kijijini karibu na raia. Siku moja akaamua kwenda ofisini kumwona mumewe. Baada ya saa moja mumewe alirudi akiwa ameandamana na mwanamke. Lilia alipokewa na kuambiwa arudi nyumbani.

Jioni ile alipofungua mlango badala ya salamu alipokea kofi ambalo lilimfanya kuona vimulimuli kisha akaambiwa asionekane tena ofisini. Siku moja akaamua kuripoti na liwe liwalo. Alipoingia kituo cha polisi alilakiwa vizuri na kuelezwa kuwa mumewe alikuwa karibu kuja. Akaondoka maji yamejaa tumboni akijua mumewe atapashwa habari. Mumewe alikuja siku tano baada ya Lilia kwenda kwenye kituo cha polisi. Alipoingia tu mara alishikwa nywele karibu zing'oke. Alipigwa na kuumizwa mkono. Alimpigia mama mkwe simu naye akafadhaika sana kwa ukosefu wa fadhila za Luka. Mara moja akampigia mwanawe simu. Akamsomea na kumwambia atume ambulensi. Lilia alipozinduka alijipata kwenye kitanda cha hospitali. Siku ya nne aliamka na kupata hakuwa peke yake. Kuna mtu kando yake lakini asingeweza kumtambua maana kafungwa bendeji usoni.

Siku ya nne ndipo alipogundua kuwa mtu huyo aliyekuwa kando yake ni mumewe. Alikuwa amehusika na ajali mbaya sana ya barabarani. Kiruka njia wake alipogundua kuwa hatawahi tembea tena alipotelea mbali.

**ANWANI**

- Hata baada ya Lilia kumwonea Luka alipoingia siku ya kwanza alipohudhuria ibada na kumsihi babake kumsaidia na Luka kuhaidi kuwa nia yake kwa Lilia ilikuwa safi. Tunamwonya Luka akilipa fadhila zote za Lilia kwa kumtawisha na kumpiga kiasi cha kukaribia kumuua na hata mimba kutunguliwa.
- Fadhila za babake Lilia (senior pastor Lee) zinalipwa na mashuzi pale ambapo mamake Luka anapewa nafasi ya kazi ya kunadhifisha mazingira na hata kulipiwa karo lakini mhubiri anapokufa Luka anauza kanisa ( UK 5).

- Kuruka njia wa Luka anatanabai kuwa Luka hatawahi kutembea tena aligeuka na kuondoka. Hakuwahi kuonekana pale. Fadhila za Luka kwake anazilipa kwa mashuzi. ( UK 9).

**DHAMIRA**

- Lengo kuu la mwandishi ni kutahadharisha watu ambao wanapokuwa katika hali ya uhitaji na kusaidiwa baadaye kusahau na kulipa watu wema wao kwa mabaya /maovu. Luka baada ya kusaidiwa na babake Lilia alimlipa kwa uovu kwa kuuza kanisa lake na kumtesa mwanawe.

**MAUDHUI**

***Ukatili***

- Luka alimpiga mkewe kwa kosa ndogo kama vile kukosa kuchukua simu. Tunaambiwa kuwa mara ya mwisho ilikuwa teke lililompata tumboni sawasawa asiweze kujinyoosha kwa siku mbili kwa maumivumakali. ( UK 1)
- Kwenye veranda kulikuwa na kioo kilichopasuka kumbukumbu ya pigo jingine, kisingizio kuwa chakula hakikukolea chumvi.
- Jioni ile baada ya Lilia kutoka katika ofisi ya mumewe, alipofungua mlango, badala ya salamu alipewa kofi ambalo lilimfanya kuona vimulimuli. Kisha kofi likaandamana na teke lililomlaza kochini kama zigo. (Uk 6)
- Kila mara alimwona mumewe kwenye vyombo vya habari ameandamana na yule mwanamke, akidhubutu kuuliza alijibiwa kwa kipigo kilichomlaza kitandani siku mbili.
- Baada ya Lilia kwenda kwenye kituo cha polisi mumewe alirudi baada ya siku tano. Lilia alimfungulia mlango mara akavurutwa nywele karibu zing'oke. Akaburutwa hadi kwenye chumba cha malazi akapigwa na kuumizwa mkono. ( UK 7)

***Siasa***

- Siku moja Luka alimwambia mkewe kuwa ashachoshwa na kuhubiri anataka kuwa mwanasiasa. Luka aliendeleza mikutano ya siasa kila siku.
- Luka kujihusisha kwenye siasa kunaonekana kumbadilisha kihulka na kiutu. Anaonekana kufanya maovu huku akijua kuwa hakuna hatua yoyote angechukuliwa maana alikuwa gavana.

***Mapenzi***

- Babake Lilia alimpenda sana mamake Lilia ndio maana hata aliposhinikizwa aoe kutoka kwa wazee wa kanisa, wahubiri weza, mhubiri aliwaza kuwa hangepata mwandani kama mke wake marehemu. Kuwa hatoshi yeyote kujaza pengo aliloliacha mke wake. ( UK 3)
- Babake Lilia alimpenda bintiye sana na kumridhirisha kwa kila hali . Ndio maana anapomwomba amualike Luka, anafanya hivyo.

***Dini***

- Baba Lilia (senior pastor Lee Imani) alikuwa mhubiri.siku hiyo jumapili anafunza kuhusu kumpenda jirani yako. Ndipo akaingia Luka kanisani siku hiyo
- Luka alifanya kazi kanisani na matunda ya kazi yake yalidhihirika. Watu walitoka hata nchi mbali kuja kuombewa naye, wapate muujiza.

***Ndoa***

- Ndoa kati ya babake Lilia na mamake ilijengwa kwa misingi ya mapenzi ya dhati maana hata mamake anapokufa babake anawaza kuwa hangepata mwandani kama mke wake.
- Ndoa kati ya Luka na Lilia ni ndoa ambayo imejaa manyanyaso na ukatili. Luka anampiga mke wake hata kwa kosa ndogo sana kama kutoshika simu, chakula kutokolea chumvi.

***Mauti / kifo***

- Mamake Lilia anakufa kwa ajali ya barabara na kuacha pengo kubwa kwa familia yake.

***Umaskini***

- Taswira ya namna Luka alivyovaa mara ya kwanza kanisani ilikuwa ya kimaskini. Tunaelezewa kuwa alikuwa amevaa shati mararu, suruali fupi ambayo uzi umetoka kiunoni ishara ya umaskini. (UK 2)
- Mwandishi anatuelezea kuwa dhiki ziliwaandama akina Luka vibaya. Vipeni alivyovipata mamake havikutosha kulipia kibanda walichokondisha au chakula, usisahau mahitaji mengine. (UK 3)

***Utu***

- Mhubiri (babake Lilia) anampa Luka nafasi ya kazi, kunadhifisha mazingira ya kanisa (UK 3).
- Masomo ya msingi yalipokwisha Luka akajiunga na shule ya upili ya kutwa hapo karibu, mhisani wake akiwa mchungaji ( UK 3).

***Elimu***

- Luka na Lilia wanasoma. Mwishowe, waliingia chuo kimoja kusoma.

***Mapuuza***

- Lilia anapokataa kuandamana na Luka shughuli za kisiasa. Luka anatoka kwa hasira na usiku ule hakurudi nyumbani hadi siku ya pili.
- Jioni majirani wakaitwa kumpeleka hospitalini kwa sababu alikuwa amekesha usiku kucha na hakulala kwa sababu ya mawazo madaktari walishindwa kudhibiti mimba ( UK 5). Kwa hivyo Luka hakuwajibika kama mume kuhusu hisia za mkewe.
- Luka alipohamia katika kasri alisahau kitu kimoja-mwenziwe mwandani wake. Lilia aliambiwa kuwa alihitaji kuishi kijijini ili kuwa karibu na raia. Kwa hivyo hakuwajibika majukumu yake.

*Taasubi ya kiume*

- Luka anamkanya mkewe kwenda ofisini ati anamwaibisha. Anasema " Nisikuone tena ofisini mwangu mwanamke wewe,kuja kuniaibisha wapinzani wangu waseme nimeshindwa kumdhibiti mke wangu. ( UK 6)
- Luka alimtawisha mkewe. Alikuwa hataki azungumze na rafiki zake maanake wakija mumewe alimchapa.( UK 6)

**WAHUSIKA**

1. **Luka**

Ni mumewe Lilia.

**Sifa zake**

***Katili***

- Anamchapa mkewe hata kwa kosa ndogo kama kukosa kuchukua simu, chakula kutokolea chumvi. Anampiga mkewe kiasi cha kumpa makovu shavuni.

***Mwenye bidii***

- Alifanya kazi kanisani na matunda ya kazi yake yalidhihirika watu walitoka hata nchi za mbali kuja kuombewa naye.

***Mwerevu***

- Tunaambiwa Luka alikuwa wembe masomoni akili zake kama smaku hunasa yote wafunzayo walimu. ( UK 3)

***Msomi***

- Alitia bidii masomoni na alisoma hadi chuo kikuu. ( UK 4)

***Mlaghai***

- Wananchi wamegundua kuwa ahadi zote alizowahi kutoa zilikuwa uongo.

***Ana msimamo thabiti***

- Mkewe anasema kuwa Luka akishatunga nia, habadili(uk 5)

***Mwenye taasubi***

- Anamdhibiti mkewe nyumbani ili asitangamane na wenzake.

***Mwenye tamaa***

- Hata baada ya mkewe kuipoteza mimba hakujali. Hakutaka kuwa mzazi katika kipindi cha uchaguzi. Alitamani sana ukubwa.

***Mpyaro***

- Anamwambia mkewe kuwa umbo lake ni kama nguruwe.

***Mzinifu***

- Ana wanawake tele akiwemo aliyekuja hospitalini.

**Umuhimu wa Luka**

- Anaendeleza maudhui ya ukatili. Anamchapa mke wake kwa kosa dogo kama vile chumvi kutokolea kwa chakula.
- Anaziumba sifa za wahusika wengine kama vile Lilia kuwa ni mvumilivu. Mbali na madhila yote aliyopitia, bado aliendelea kumpenda.
- Anawakilisha watu ambao wana tamaa ya uongozi. Aliuza kanisa ili kujiunga na siasa.

2. **Lilia**

Ni mkewe Luka, mtoto wa mhubiri ( senior pastor Lee imani).

**Sifa zake**

***Mwenye mapenzi ya dhati***

- Alimpenda Luka kwa dhati ndio maana alimwomba babake kumwalika Luka ofisini.
- Licha ya Luka kumtesa na kumpiga, Lilia hakuacha ndoa yake wala kulipiza kisasi.

*Ni mpenda amani*

- Mumewe aliposema amechoshwa na kuhubiri, akajaribu kumbembeleza mumewe lakini wapi. Hakuteta alinyamaza ili kudumisha amani katika ndoa yake.

*Ni mwoga*

- Alimwogopa sana mumewe kwa sababu ya kichapo. Ndio maana amelala pale juu ya kochi ili akiingia tu, hata kabla ya kubisha mlango awe tayari kuufungua.

*Ni Msomi*

- Amesoma hadi chuo kikuu na ni meneja wa benki moja mjini.

*Ni Mvumilivu*

- Anavumilia kichapo cha kila wakati kwa mumewe kwa makosa yasiyo na msingi.

**Umuhimu wa Lilia**

- Kupitia kwake tunapata sifa za Luka kuwa ni katili. Anampiga Lilia kwa makosa madogomadogo.
- Anaendeleza maudhi ya uvumilivu. Anavumilia kuishi na Luka hata kwa mateso.
- Anawakilisha wanawake ambao wameolewa na wanasiasa na kupitia mateso mengi

**3. Baba Lilia ( senior pastor Lee Imani)**

**Sifa zake**

*Mwenye mapenzi*

- Alimpenda sana mkewe. Ndio maana hata mkewe anapokufa anawaza mahali ambapo atampata mwandani kama mke wake. Anasema, "Hatoshi yeyote yule kujaza pengo aliloliacha mke wangu mpenzi."

*Mlezi mwema*.

- Anamlea bintiye kwa mapenzi. Ndio maana anamrai bintiye kuhusu uhusiano wake na Luka

*Mwenye utu*

- Anampa Luka kazi ya kunadhifisha kanisa.
- Pia anamsaidia Luka kufikia kuwa mhubiri katika kanisa lake.

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA.

*Kinaya*

- Ni kinaya kwa Luka kumdhulumu Lilia kwa kumchapa hata baada ya babake kumtendea wema.
- Ni kinaya kuwa Luka anachoshwa na kazi ya kuhubiri na kuamua kuingilia siasa.

*Kisengere nyuma.*

- Lilia anakumbuka mara ya mwisho kupokea simu alipigwa teke tumboni sawasawa asiweze kujinyoosha kwa siku mbili kwa maumivu makali.
- Kovu alilo nalo shavuni  Lilia, linamkumbusha pigo jingine kisingizio kuwa chakula hakikukolea chumvi.

*Tashbihi*

- Ghamidha itakuwa imezidi, imefuta kama hamri ( UK 1).
- Kucheka kulikuwa nadra kama kupatwa na mwezi.
- Bintiye katika kama maji mtungini (UK 2).
- Kibinti kilimlanda mamake kama shilingi kwa ya pili.
- Anayempenda kama mboni ya jicho lake ( UK 3).
- Badala yake lilichochea kama moto kuuvuvia (UK 4).
- Nia yangu nyeupe kama pamba ( UK 4).
- Kofi lililomlaza kochini kama Zigo lililosukumwa ( UK 6).
- Akitetea kama unyasi upepo uvumapo ( UK 7).

***Misemo***

- ★ Mvumilivu hula mbivu ( UK 1).
- ★ Kumtoa nyoka pangoni (UK 2).
- ★ Rafiki wa kufa kuzikana (UK 3).
- ★ Utajua kilichomtoa kanga manyoya shingoni (UK 6).

***Taswira***

- ★ Nywele za Luka zilikuwa matimutimu, uso umechorwa mistari myeupe, shati refu limemfika magotini.
- ★ Lilia alikuwa na ngozi nyororo kila mara ikijishobwekea na vidu kudhihiri kila alipocheka.

***Tabaini**.*

- ★ Si wahubiri si wazee wa kanisa si washirika ( UK 3).
- ★ Si makofi, si ngumi, si mateke ( UK 7).

***Methali***

- ★ Usione wembamba wa reli gari moshi upita pale. ( UK 2)
- ★ Yaliyopita si ndwele. (UK 5)
- ★ Umdhaniaye ndiye kumbe siye. ( UK 5)
- ★ Lisemwalo lipo na kama halipo li njiani laja. ( UK 6)
- ★ Mwanzo wa ngoma ni Lele.
- ★ Fadhila za punda ni mashuzi. (UK 8)
- ★ Uliacha mbachao kwa msala upitao.
- ★ Lilia alipigwa na butwaa.

***Tashihisi.***

- ★ Yeye na maji walikuwa mahasimu.( UK 2)

***Jazanda***

- ★ Kondoo – waumini.

## 2. MSIBA WA KUJITAKIA-*D. W Lutomia*

## MTIRIRIKO

Hadithi hii inaanza huku wakazi wa jimbo la Matopeni likionekana kujutia chaguo la kiongozi wao. Hali ya maisha inaonekana kuwa ngumu sana.

Machoka, mkaazi wa matopeni anadhihirisha hali hii jioni moja kwa kuchoka sana baada ya harakati za mchana mzima za kutafuta kibarua ila hakupata kibarua chenyewe. Hana chochote kwake, anapata pangu pakavu (uk 10) hata chakula pekee hana.

Machoka anakumbuka wanasiasa na siasa zao walipokuwa wananadi sera kuomba kura huku wakitoa ahadi nyingi, zingine kwenye mihadhara ya kisiasa, kwenye redio, runinga na hata kwenye mitandao ya kijamii. Zuhura ni mmoja wa wakaazi wa Matopeni ambaye anajutia uongozi mbaya uliomwelekeza kwenye udhikifu alio ndani sasa. Licha ya yeye kuwa mtetezi mkubwa wa mwanasiasa Sugu Junior kwa kauli ya kuwa ni mtu 'wake'. Hivii sasa hawajatimiza ahadi yoyote ile. Anajutia pia kuchagua viongozi kwa kushawishiwa na pesa.(uk 12).

Msimulizi anasimulia usuli wa uhasama kati ya viongozi wawili wakuu hasimu: Sugu Junior ambaye ndiye kiongozi wa sasa wa Matopeni na Fumo Matata ambaye ndiye mpinzani wake. Babake Fumo Matata, bwana Zuzu Matata aliyependekezwa kuwa kiongozi wa Matopeni, ila Zuzu Matata akakataa kuchukua uongozi hadi pale Sugu senior, babake Sugu junior angetolewa gerezani. Sugu senior akaishia kuwa maarufu sana na kuchukua uongozi wa Matopeni ambao ulirithiwa mwanake Sugu junior na hivyo uhasama kati ya familia hizi mbili ukaendelea kupaliliwa hadi wa leo. Kunao wanaoshangazwa na hali ya kuwepo familia mbili pekee zinazozozeania uongozi wa Matopeni (uk 13)

Sugu junior anashinda tena kura ya uongozi wa Matopeni. Kunao wengi ambao hawakufurahishwa na ushindi huu ila hawakuwa na la kufanya. Kuna tetesi za wizi wa kura ambapo Fumo Matata ananyang'anywa ushindi wake. Kahindi Mlalamo ni miongoni mwa watu wanaothibitisha hili anapomwandikia Fumo Matata ujumbe mfupi wa simu na kumpongeza kwa ushindi wake japo unanyakuliwa. Anampa matumaini ya kesho nzuri kisiasa kwa wana Matopeni. Siku ya kusheherekea ushindi wa Sugu Junior

inaandaliwa sherehe kubwa inayopangwa kuhudhuriwa na watu wengi sana ila inakuwa fedheha kubwa kwa Sugu Junior kufika uwanjani na kupata wafuasi wachache sana, Zuhura akiwa miongoni. Siku hiyo vyombo vyote vya habari vikiwemo vya kimataifa viliarifu kuwa viongozi wa majimbo jirani wasusia sherehe za kuapishwa kwa Sugu Junior.

**DHAMIRA.**

- Mwandishi anadhamiria kumulika siasa mbaya za kikabila zinavyoishia kuwaathiri wananchi kiuchumi haswa, na hili linadhihirika Matopeni.
- Mwandishi anakashifu vitendo viovu vya wizi wa kura vinavyoweza kuathiri na kuaibisha viongozi namna alivyoaibishwa Sugu Junior.
- Mwandishi alitazamia kuelimisha wananchi namna siasa za utangulizi wa nchi huathiri siasa za baadaye.

**UFAAFU WA ANWANI.**

- Anwani; msiba wa kujitakia inajitokeza waziwazi kwa mhusika Zuhura anayeishia kuathirika na uongozi wa Sugu Junior baada ya yeye kumpigia kura kwa visababu visivyofaa kama yeye ni mtu wa kwao (uk 11)
- Sugu Junior anapata msiba wa kuaibishwa kwa kukosa wafuasi na wanasiasa wa majimbo jirani kukosa kuhudhuria mkutano wa sherehe za ushindi na kuapishwa kwake kwa kuiba kura.
- Zuzu Matata anapata msiba wa kukosa uongozi wa Matopeni anapokataa kutawazwa kiongozi wa Matopeni na wakoloni ati Sugu Senior aachiliwe huru. Anaishia kukosa uongozi wa Matopeni kabisa.
- Wanamatopeni wapitia hali mbaya ya maisha na kiuchumi kwa kuchagua viongozi wasiofaa kwa misingi ya kikabila.
- Shairi la malenga mteule kaulimbiu yake ni msiba wa kujitakia, hana kilio linalowakashifu wanasiasa ambao ni walafi huku wengine wakizidi kufilisika.

**MAUDHUI**

**UMASKINI.**

Ni hali ya uchochole na uwezo mdogo wa kifedha na mali.

- Wanamatopeni wanalemewa na mzigo wa maisha kwa ukata na umaskini unaowaandama. Msimulizi anasema; 'Takriban kila mmoja akiwa ameghadhabishwa na hali ya maisha hapo walipopaita kwao-Matopeni' (uk10). Machokaa anaonekana kupitia hali ugumu ya maisha. Ametafuta kibarua na kukosa na kushindwa kuhimili makali ya njaa. Anashindwa la kufanya (uk10).
- Machokaa anasema kuwa maisha ya wanamatopeni ni maisha ya pangu pakavu. wasakatonge ambao wapiga kura ni tofauti sana na wapigiwa kura ambao ni tajiri.
- Malenga mteule kwenye shairi lake la msiba wa kujitakia hauna kilio anazungumzia umaskini ambao unawakumba wananchi huku walaji wakiendelea kufurahia.
- Zuhura mkazi wa Matopeni anajutia kuchagua viongozi kwa sababu ni 'mtu wao' na kupewa visenti ilhali viongozi wao hao sasa hawajatimiza ahadi zao na hivi sasa anapitia hali ngumu ya maisha na umaskini haswa (uk11)
- Kuna sehemu mbili katika uwanja wa Mamboleo, sehemu ya waheshimiwa na sehemu ya pili kwenye jua kali aliyokaa Zuhura. Ni sehemu ya maskini na wananchi watozwa ushuru(uk14)

**UTABAKA.**

- Machoka anazungumzia tofauti za mpiga kura na mpigiwa kura. Anasema kwanza makundi haya mawili yametengana kama ardhi na mbingu. Huu ni utabaka (uk10)
- Kunaonekana kuwa na familia mbili ambazo zinaonekana kugombania uongozi wa Matopeni. Wanaonekana kuwa ndio wa tabaka la juu Matopeni.
- Kiwanjani Mamboleo kumeandaliwa sehemu mbili kuu. Upande mmoja umeandaliwa waheshimiwa na upande mwingine ni wa wananchi. Msimulizi anasema kuwa "kuna tofauti kati za pande hizi mbili. Walipoketi waheshimiwa pametandikwa hema kubwa, meza zilizoandaliwa maridadi na chupa za maji na soda kuwekwa juu yake kukidhi mahitaji ya matumbo yao. Zuhura naye amechukua nafasi kwenye sehemu ya pili palipoandaliwa kwa ajili ya watu kama yeye,

sehemu ambayo jua kali lilipenyeza miale yake ya ghadhabu, sehemu ya wapiga kura, watozwa ushuru!" (uk14)

## SIASA

- Siasa za Matopeni ni za kuwahamasisha wananchi wawapigie kura ya kihadhara, ya kisiasa, kwenye redio, runinga na hata mitandao ya kijamii.(uk11). Ahadi nyingi zilitolewa kwa wananchi. Wote serikalini na upinzani walitoa ahadi chungu nzima. Ahadi hizi zilionekana kutotimizwa kama anavyosema Machoka na Zuhura.
- Siasa za Matopeni zilizua uhasama. Kuna uhasama kati ya Machoka na Zuhuru kama kutokana na upande tofauti za viongozi walioshabikia. Vilevile kulikuwa na uhasama wa muda mrefu kati ya Fumo Matata na Sugu Junior, uhasama ulioanza tangu ukoloni na wazazi wao na unaendelezwa na wanao Matata na Sugu.
- Upigaji kura na kiongozi anayeishia kuongoza Matopeni anaonekana kutokuwa kiongozi halali maana kuna tetesi za wizi wa kura. Msemaji anasema; "pale Matopeni kupiga kura na kutopiga kura ni mamoja." Uamuzi wa mpiga kura hauheshimiwi……" (uk13). Tetesi hizi zinaungwa mkono na kahindi mlalama anayempongeza Fumo Matata kwa ushindi japo unaibwa. Anampa matumaini ya kesho nzuri kisiasa. Hili linajitokeza zaidi sherehe za ushindi wa Sugu Junior na kuapishwa inaposusiwa na wanamatopeni na viongozi wa majimbo jirani (uk15).

## UONGOZI MBAYA.

- Ni kuongoza kwa namna wananchi wasiyopenda, wasiyofurahishwa au kuridhishwa na wengi.
- Wanamatopeni wanaonekana kupitia hali ngumu ya kimaisha. Msimulizi anasema "Takriban kila mmoja ameghadhabishwa na hali ya maisha ya hapo walipopaita kwao- Matopeni." (uk18) Wananchi wanaonekana kubebeshwa mzigo mzito wa maisha wanaopania kuutua. Huu ni uongozi mbaya.
- Kuna tofauti kubwa za kimaisha kati ya wapiga kura na wapigiwa kura kulingana na usemi wa Machokaa. Hii ni ishara tosha ya uongozi mbaya unaokithiri Matopeni.

- Shairi lake Malenga Mteule anasema; “Tunazidi filisika walaji kujijazija” wanakaliwa hawa ni viongozi wanaongoza vibaya bila shaka.
- Zuhura analalamikia udhikifu unaomkumba. Hili analaumu kuchagua viongozi kwa kuwa ni “mtu wao” na kupewa vijisenti. Viongozi hawa wanaishia kuwapitishia dhiki Zuhura na wanamatopeni wenzake.
- Msimulizi anasema; “Jimbo la Matopeni lilikuwa limegeuzwa ngome ya watu fulani binafsi. Watu wenye ushawishi mkubwa serikalini. Watu wasiojali maisha ya wapiga kura kama Machoka na Zuhura…… (hii ni ithibati ya uongozi mbaya uliokuwa matopeni.) (uk11). Wanamatopeni walipotathmini hali zao, walijifananisha na panya kwenye mtego wa uhitaji. Uhitaji ambao mishahara yao duni iliyokwama huko kwenye udhalimu haingekidhi. Vilevile mishahara ilimezwa na jisu kubwa la ushuru…..” (uk12)
- Uongozi wa Matopeni na wanaoshughulika kutangaza kiongozi wa ushindi wa uchaguzi wanafanya vibaya kwa kuwalazimishia wananchi kiongozi wasiyempenda na wasiyemchagua. Msimulizi anasema, “pale Matopeni kupiga kura na kutopiga ni mamoja. Uamuzi wa mpiga kura hauheshimiwi…..”
- Kahindi Mlalama kupitia kwa ujumbe wake mfupi anaoandikia Fumo Matata anazungumzia vizingiti vya viongozi vikiwemo; kulimbikiziwa viongozi, udikteta, ukoloni mamboleo. Huu ni uongozi usiopendwa.
- Wananchi na viongozi wa majimbo jirani hawapendezwi na uongozi wa Sugu Junior anayefaa kusheherekea ushindi wake na kuapishwa. Hii ndiyo sababu wanasusia sherehe hii inayotazamiwa kuwa kubwa na haikufana.

**MABADILIKO.**

- Kuna mabadiliko ambapo sherehe ya Sugu Junior kuapishwa iliyotarajiwa kuwa kubwa inasusiwa na wananchi na viongozi wa majimbo jirani.
- Machoka anaona mabadiliko yanayotokea viongozi wote wa serikali na upinzani wanavyokosa kutimiza ahadi zao baada ya kutwaa uongozi.
- Zuhura naye anajuta nafsini na kujisuta baada ya kupigia kura viongozi ambao ni “mtu wao”na kupewa visenti na kujuta viongozi

wanapokosa kutimiza ahadi zao. Viongozi hao hubadilika wanapofika uongozini na kukosa kutimiza ahadi zao.

- Mabadiliko ya uongozi na ushawishi yalitokea ambapo baada ya Zuzu Matata kukataa kutwaa uongozi wa Matopeni hadi Sugu Senior aachiliwe huru, umaarufu wake uliongezeka na akaishia kuwa kiongozi wa Matopeni. Zuzu Matata Hakupata tena fursa ya kuongoza Matopeni.
- Kahindi Mlalama kwenye ujumbe wake mfupi kwa Fumo Matata, anazungumzia changamoto za wizi wa kura, kulimbikiziwa viongozi, udikteta, na ukoloni mambo leo. Hata hivyo anampa Fumo Matata matumaini ya mabadiliko. Anamwambia "…..ila kesho…..kesho…. kesho yote haya yatakuwa marehemu." (uk13).

## MIGOGORO.

Ni tofauti zinazojitokeza au uhasama kati ya watu, kundi la watu au hata nchi na nyingine.

- Kuna migogoro kwenye nafsi ya Zuhura. Msimulizi anasema ; "Zuhura alijisuta nafsi yake….." (uk11). Hii ni baada ya yeye kuchagua viongozi kwa kuwa ni "mtu wao"na kupewa visenti ili kuchagua viongozi ila sasa anapitia hali ngumu ya maisha na hata mfumko wa bei. Majuto haya yanamsababishia migogoro nafsini mwake.
- Kulikuwa na migogoro kati ya Zuhura na Machokaa kutokana na tofauti zao za kisiasa. Msimulizi anasema "Kwa muda mrefu, Machoka na Zuhura walikuwa kama fahali wawili- hawakai katika zizi moja." Kisa na maana ni wafuasi wa watu wawili tofauti. (uk11)
- Kulikuwa na mgogoro wa kisiasa kati ya Fumo Matata na Sugu Junior. Sugu junior alikuwa ndiye serikali ilhali Fumo Matata ndiye alikuwa upinzani. Mgogoro huu ulianza zamani sana kuanzia familia zao mbili, baba zao Zugu senior na Zuzu Matata. (uk12)

## WAHUSIKA

## MACHOKA

Ni Mwanamatopeni na hasimu wa kisiasa wa Zuhura.

**SIFA ZAKE**

***Ni mwenye bidii***

- Alitafuta kibarua mchana kutwa japo ziligonga mwamba. (uk10)

***Ni mzalendo***

- Ana shughulishwa na uongozi wa Matopeni
- Alihudhuria na kufuatilia sherehe na kampeni za wanasiasa wa matopeni. Ndio maana anakumbuka ahadi zao ambazo haziishi kutimizwa.

***Ni mchochole***

- Alikabiliwa na umaskini. Jioni alikuwa amechoka baada ya kutafuta kazi na akakosa, anahisi njaa.
- vilevile taswira ya chumba chake ingeweza kumliza kipofu ni kutokana na hali ya uchochole uliokuwa ndani.(uk10)

***Ni msomi***

- Alikuwa amesoma ndio maana anakumbuka shairi alilowahi kusoma la Malenga Mteule.

**Umuhimu wa Machoka**

- Anaendeleza maudhui ya uzalendo. Alihudhuria na kufuatilia sherehe na kampeni za Matopeni
- Kupitia kwake tunapata sifa za Sugu Senior kuwa ni katili. Anawaongoza wanamatopeni kidhalimu
- Anawakilisha wananchi wanaofanya uamuzi wa busara wakati wa uchaguzi

**ZUHURA.**

**SIFA ZAKE**

***Ni mzalendo***

- Anajishughulisha na siasa za nchi. Ndio maana alihudhuria mkutano wa kuapishwa kwa Sugu Junior. Vilevile alishiriki uchaguzi japo anaishia kujutia chaguo lake.

***Ni mwenye majuto***

- Anajutia na kuisuta nafsi yake kwa kupigia viongozi ambao ni "watu wake" na waliompa visenti ila mwishowe hawakutimiza ahadi zao na sasa yeye pamoja na Machoka wako katika hali ya udhikifu. (uk11).

***Ni maskini***

- Zuhura anajuta kupigia kura"watu wao" ilhali bado wanaogelea kwenye umaskini na udhikifu, yeye na mwenzake Machoka. (uk11)
- Anachukua nafasi yake kwenye sehemu palipoandaliwa kwa ajili ya watu kama yeye- maskini (uk14)

***Ni mjinga***

- Anapigia kura viongozi maana ni "watu wao" na akaishia kujuta mwishowe kwa ahadi zilizotumiwa na kubakia maskini.
- Licha ya kupigia kura viongozi wasio na mabadiliko na wasiotimiza ahadi zao, bado Zuhura anahudhuria mkutano wa kusheherekea Sugu Senior ambaye hakuleta mabadiliko. Anaketishwa sehemu ya pili ya maskini wanapochomwa na jua ila hapati funzo kutokana na hali hii bado.(uk14-15)

**Umuhimu wa Zuhura**

- Anawakilisha watu ambao hawafanyi maamuzi mazuri ya uongozi kisha wanakuja kujutia baadaye.
- Ni kilelezo cha watu ambao hawajifunzi kutokana na makosa yao
- Anaendeleza maudhui ya ujinga, hata baada ya kumpigia Sugu junior na kukosa kutimiza ahadi za kampeni, bado alimpigia kura kwa mara ya pili na kuhudhuria sherehe yake iliyosusiwa.

**SUGU SENIOR.**

Ni babake Sugu Junior na kiongozi wa kwanza wa Matopeni.

***Ni mzalendo***

- Aliongoza nchi yake- huu ni uzalendo
- Alipigania nchi yake kutoka kwa walowezi hii ndio maana alifungwa jela.

***Ni mlezi mwema***

- Alimlea mwanawe akaishia kumrithi kama kiongozi wa Matopeni.

**Umuhimu wa Sugu Senior**

- Ni kielelezo cha viongozi dhalimu wasiotimiza ahadi zao wakati wa kampeni

**SUGU JUNIOR**

Ni mwanawe Sugu Senior na kiongozi wa Matopeni.

***Ni mwongo***

- Hakutimiza ahadi alizowapa wanamatopeni na bado alitaka uongozi kwa mara nyingine.

***Ni dhalimu***

Msimulizi anasema "jimbo la Matopeni lilikuwa limegeuzwa ngome ya watu fulani binafsi. Watu wasiojali maisha ya wapiga kura kama Machoka na Zuhura (uk11)

***Ni fisadi***

Aliiba kura za Matopeni ilhali hakupendwa na watu wa Matopeni na hakuchaguliwa nao.

**ZUZU MATATA.**

- Ni babake Fumo Matata na kiongozi wa kwanza wa upinzani Matopeni.

***Ni mjinga***

- Alikataa nafasi ya kuongoza Matopeni alipopendekezwa na wakoloni ili Sugu senior aachiliwe huru kwanza. Mwishowe Sugu Senior alipata umaarufu zaidi na Zuzu Matata hakupata kuongoza Matopeni tena (uk12)

***Ni mzalendo***

- Alipigania kuongoza Matopeni japo hakupata nafasi ya kuongoza.

***Ni mwenye kujali***

- Anakataa ubinafsi wa kufanywa kiongozi wa Matopeni ili Sugu Senior aachiliwe huru kwanza. (uk 12)

**FUMO MATATA**

Ni mwanawe Zuzu Matata na anapigania nafasi ya kuongoza Matopeni.
***Ni mzalendo***

- Anapigania mabadiliko ya uongozi Matopeni na kutaka kuwa kiongozi wao.

***NI mwenye bidii***

- Kampeni yake ilikuwa ya kupigiwa mfano na Fumo Matata alikuwa na wafuasi wengi.

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA.

## MAJAZI

1. ***MATOPENI-*** Ndiyo nchi ya kina Machoka na Zuhura. Kuna umaskini mwingi ambao ni sawia na Matope.
2. ***MACHOKA-*** Ni mwanamatopeni
   - Anafika jioni kutoka kutafuta kazi bila kupata huku amechoka zaidi ya kuchoka.
3. ***ZUZU MATATA-*** Ni babake Fumo Matata.
   - Anaonyesha uzuzu anapokataa kuchukua hatamu za uongozi wa Matopeni ili Sugu senior aachiliwe huru. Sugu mwenyewe anaishia kuwa maarufu na kuwa kiongozi wa Matopeni. Zuzu Matata anajaribu kivyovyote vile kupata uongozi wa Matopeni lakini hapati.
4. ***MATATA-*** ni hali ya kutofautiana kimawazo na mtu mwingine. Zuzu Matata aliishia kutofaitiana na Sugu Senior hadi akaishia kuwa kiongozi wake mkuu wa upinzani.
5. ***SUGU SENIOR-*** Baada ya Zuzu Matata kukataa kuchukua uongozi wa Matopeni alipopendekezwa na wakoloni, anakuja kuwa maarufu na Sugu kwa Zuzu Matata. Zuzu Matata anajaribu kutwaa uongozi kutoka kwake lakini hakuweza.
6. ***KAHINDI MLALAMA-*** Ni rafiki ya Fumo Matata na anamwandikia barua.
   - Ni katika barua hii anapolalamikia kuibiwa kura kwa Fumo Matata,kulimbikizwa viongozi,udikteta na ukoloni mamboleo.

*7. MAMBOLEO-* Ni kiwanja alichopania kufanyia sherehe Sugu Junior sherehe za ushindi wake na kuapishwa.

- Mamboleo kulifanyika mambo siku hiyo ya kustaabisha. Wananchi na viongozi wa majimbo jirani kususia sherehe za kuapishwa Sugu Junior.

**TASHBIHI**

★ Yametengana kama mbingu na ardhi…(uk10)
★ Maisha ya Matopeni yalikuwa kama mchezo wa karata …(uk11)
★ Wanajitenga na umma kama wagonjwa wa ukoma…(uk15)

**TAKRIRI**

★ ….Maisha (uk 10)
★ ….hiki na kile, kile na hiki…(uk11)
★ ….ndoto (uk 12-13)

**UHUISHAJI/TASHHISI**

★ Maonevu yalihukumu nafsi yake (uk10)
★ Ukumbi wote ulimkondolea macho (uk15)
★ Ndoto isiyojua wakati wa kuamka (uk12)
★ Ushindi huo huenda usione jua (uk13)

**MSEMO**

★ Wajinga ndio waliwao (uk11)

**MASWALI BALAGHA**

★ …...Wananchi wataendelea kulimbikizwa viongozi wasiowataka? (uk13)

**METHALI**

★ Walikuwa kama fahali wawili hawakai katika zizi moja…(uk11)
★ Msiba wa kujidunga huambiwi pole.(uk11)

- ★ Maji yakimwagika hayazoleki..(uk11)
- ★ Mwana akinyelea paja halikatwi (uk11)
- ★ Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi (uk11)
- ★ Lisilobudi hubidi (uk12)
- ★ Ukistaajabu ya Musa hujayaona ya firauni (uk 13)
- ★ Subira huvuta heri (uk15)

## 3. MAPAMBAZUKO YA MACHWEO-*Clara Momanyi*

### MTIRIRIKO

Mzee Makutwa alizoea kumpitia mzee Makucha kila siku jioni baada ya shughuli ya siku. Walikuwa marafiki tangu zamani. Urafiki wao ulidumu hata baada ya kustaafu. Walijulikana vizuri mambo ambayo mzee Makutwa akijishughulisha nayo. Mara alionekana na gari lake aina ya probox akiwa amewabeba vijana. Alimsuta kwa kukosa kujishughulisha na biashara kubwakubwa na kuridhia kuchuuza vitafunaji majiani.

Mkewe mzee Makucha alimweleza awache urafiki wake na makutwa lakini mumewe akasema kuwa hawakuwa na usuhuba na salamu za Mungu hazinyimwi mtu. Mzee Makucha alipigwa kalamu kazini miaka mingi iliyopita. Shirika la reli alipohudhuria tangu macheo ya maisha yake lilimtimua kazini ili kupunguza idadi ya waajiriwa. Shoka likamwagukia miongoni mwa wengine. Bintiye wa pekee aliwatoroka akiwa na umri mdogo kwenda kuolewa ughaibuni. Hakuweza kustahimili hayo maisha.

Mzee Makucha alipokuwa akiwazia kuhusu kazi anayoifanya mzee Makutwa, alishtuka kumwona mzee Makutwa amefunga breki za gari karibu na pahali alipoketi. Ndani ya gari mlikuwa na vijana wachache waliokuwa wakifanana Marangi. Alimkejeli mzee Makucha kwa biashara anayoifanya akimwambia kuwa anadhalilisha umri wake na kuwa awachie vijana wadogo wafanye kazi hiyo naye apumzike nyumbani.

Mzee makucha pia aliwaza juu ya kazi aliyoifanya mzee Makutwa. Alitaka kujua ukweli huo hasa kutokana na kauli alizotoa. Alipokuwa akiwazia hili, vijana wawili walikuja na kununua kashata. Walionekana

kuchoshwa na maisha kutokana na yale mazungumzo yao. Mzee Makucha hakushangazwa na hilo kwani vijana wengi walizurura ovyo bila kazi.

Vijana hao walikubaliana kuwa wakiona gari aina ya probox waliabiri. Mzee Makucha naye akaamua kufuata gari hilo kwa kutumia teksi. Walifika mahali ambapo palikuwa tambarare kubwa lililopambwa kwa viduta vidogovidogo vya mchanga. Kulikuwa na watoto wadogo ambao hata hawajafikisha Miaka kumi ambao walikuwa wanafanya kazi. Walipofika mjini kazakamba , mzee Makucha alifululiza hadi kwenye kituo cha polisi. Huko alieleza yale aliyoona. Polisi walielekea kumtia mbaroni mzee Makutwa.

Alipokuwa akiwaza kwa nini hajatiwa mbaroni, mlango ulibishwa. Tajiri mmoja mle kijijini alikuja kumpongeza mzee Makucha kwa kazi nzuri. Alimpa bahasha ambayo ilikuwa na hundi la pesa . Mzee Makucha alifurahi na kusema kuwa ingawa amefikia magharibi ya maisha, hundi hiyo imempa tumaini la mapambazuko mapya maishani.

**DHAMIRA**

- Mwandishi alikuwa na Lengo la kueleza namna ukosefu wa kazi unaweza kumfanya mtu kufanya kazi yoyote . Mfano mazungumzo ya Sai na Dai. ( UK 19)
- Alidhamiria kuelimisha athari ya kuajiri watoto wadogo ambao wanapaswa kuwa shuleni.

**ANWANI**

- Mzee Makucha anamwambia Makutwa kuwa “ Heri wewe unayestaladhi katika machweo ambayo sasa ni mapambazuko kwako” kuwa heri yeye hata baada ya kustaafu ana pesa. Kuliko yeye anayeuza vifafunaji tu. (UK 18)
- Mzee anasema kuwa mwomba Mungu hachoki kuna siku jua la macheo litanibishia mlango hata kama naelekea machweo. (UK 19)
- Siku ilikutwa ikashuhudia mzee Makutwa akiwekwa korokoroni kwa kosa la jinai. Mkono wa sheria nao ukamsukumia kuyakabili machweo ya maisha yake kifungo. (UK 23)

- Mzee Makucha alimshukuru sana tajiri yule aliyemtunuku zawadi huku akisema ingawa alikuwa amefikia magharibi ya maisha yake, sudi hii imempa tumaini la mapambazuko.

**MAUDHUI**

***Kazi***

- Mzee Makucha na mzee Makutwa walikuwa wakifanya kazi katika nyadhifa mbalimbali. Mzee Makutwa alistaafu katika nyadhifa ya uwaziri. Makucha naye alipigwa kalamu katika shirika la reli.
- Baada ya mzee Makucha kupigwa kalamu, kila siku asubuhi alichukua kigoda chake Pamwe na bidhaa ndogondogo alizochuuza kando ya barabara. ( Luzi, tende , kashata) ( UK 17).
- Mkewe mzee Makucha aliupitisha muda wake akichuuza kaimati na vitumbua kwenye veranda ya nyumba.
- Mzee makutwa anamiliki migodi ambapo amewaajiri watoto wadogo ( UK 21)

***Umaskini***

- Mzee Makucha hata baada ya kupigwa kalamu na kukosa kulipwa marupurupu kwa sababu shirika la reli lilisambaratika kutokana na hali ngumu ya kiuchumi maisha yake yakaporomoka kama mabasi hata bintiye akatoroka hakuweza kustahimili hayo maisha. ( UK 18)
- Mzee makutwa alikuwa akiwachukua vijana na watoto waliokuwa wakihangaishwa na maisha ya uromo mjini na kuwaleta katika migodi kumfanyia kazi. ( UK 22)

***Ukatili***

- Katika mgodi wa bwana Makutwa kulikuwa na watoto wadogo wengine hata bado kufikia umri wa miaka kumi ambao walikuwa wamesimamiwa na wanyapara waliokuwa wakiwaamrisha kwa sauti za kutisha.
- Mazingira katika mgodi hayakuwa mazuri. Vijana waliokuwa wakichimba Madongo ya mchanga walikuwa wameloa jasho kutokana na uhaba wa hewa mle ndani.

- Mzee Makutwa alikuwa akiwachukua vijana na watoto waliokuwa wakihangaishwa na maisha ya umaskini kuwaleta katika mgodi. Ajabu ni kwamba wakiingia humo mgodini hawatoki ng'o! Ua wa stima uliozungushwa makazi haya pamoja na mabawabu katili wenye majibwa makubwa.

***Ajira ya watoto***

- Mzee makutwa aliwaajiri watoto wadogo waliostahili kuwa shuleni. Polisi anamuuliza " Mnadhani nchi itakuwa na viongozi gani kesho ikiwa mnawafungia watoto hapa wasiende shule? Hujui ni hatia kuajiri watoto enh? ( UK 23)

***Utetezi wa haki***

- Mzee makucha alifululiza hadi kwenye kituo cha polisi huko alieleza yale aliyoona kwa mgodi wa Makutwa. ( UK 22)

***Utabaka***

- Dai anasema "Tumeishia kuwa masazo ya miji kwa maana ajira zimekatwa kututembelea . Tumeziona zikipita tu kuelekea kwa akina ' heri wao'"

**WAHUSIKA**

1. **Mzee Makutwa**

**Sifa zake**

***Mwenye bidii***

- Alifanya kazi kwa bidii na kustaafu katika wadhifa wa uwaziri serikalini.

***Mwenye majitapo***

- Aliona kazi ambayo ilifanywa na mzee Makucha kama kazi ya vijana na ya kudhalilisha. Anasema " Unadhalilisha umri wako

mwenzangu. Mwacheni kijana mdogo afanye kazi hii ukajipumzishe kwako nyumbani.”

***Amekengeuka***

- Mzee Makucha hakuelewa kwa nini mzee wa umri tawili kama mzee Makutwa kustarehe na vijana wa rika la wajukuu wake.

***Ni Katili***

- Amewaajiri watoto wadogo wanaopaswa kuwa shuleni. Watoto hawa walifanya kazi nzito na walisimamiwa na wanyapara waliokuwa wakiwaamrisha kwa sauti za kutisha.

**Umuhimu wa makutwa**

- Anaendeleza maudhui ya ukatili. Anawaajiri na kuwafanyisha kazi watoto waliopaswa kuwa shuleni.
- Kupitia kwake tunapata sifa za mzee Makucha kuwa ni mtetezi wa haki.
- Anawakilisha waajiri ambao huwanyanyasa waajiriwa.
- Anawakilisha pia watu waliokengeuka katika jamii. Anatembelewa na vijana wadogo licha ya umri wake.

**2. Mzee Makucha**

**Sifa zake**

***Mwenye bidii***

- Alifanya kazi katika shirika la reli. Kazi ambayo alipigwa kalamu.

- Kila siku asubuhi alichukua kigoda chake Pamwe na bidhaa ndogondogo alizochuuza kando ya barabara.

***Mvumilivu***

- Alivumilia machungu aliyopitia baada ya kufutwa kazi na kukosa kulipwa marupurupu.

***Mpelelezi/ mdadisi***

- ➢ Anaamua kufuata gari la mzee Makutwa ili kujua anaendeleza biashara gani.

***Mtetezi wa haki***

- ➢ Anafululiza hadi kwenye kituo cha polisi kueleza aliyoyaona kwenye mgodi wa mzee Makutwa.

***Mwenye shukrani***

- ➢ Alipopewa zawadi ya bahasha alimshukuru sana tajiri yule huku akisema . "Kwa kweli asiye na tumaini hufikiria Kuwa jua hutua asubuhi."

**Umuhimu wa mzee Makucha**

- Anayajenga maudhui ya utetezi wa haki. Anahakikisha Kuwa vijana wale wamepata haki.
- Kupitia kwake tunapata sifa za mzee Makutwa Kuwa n katili.
- Anawakilisha watu ambao huwaonea huruma watu wanaonyanyaswa katika jamii.

3. **Bi machweo ( mkewa mzee  makucha)**
   **Sifa zake**

***Mshauri mwema***

- ➢ Anamtahadharisha mumewe kutokuwa na urafiki na mzee Makutwa. Anasema gari lake husheheni vijana wa mitaani, walevi na wavuta bangi.

***Mwenye bidii***

- ➢ Alichuuza kaimati na vitumbua kwenye veranda ya nyumba yao.

**Umuhimu wa Bi. Machweo**

- Ni kielelezo cha wanawake ambao huwatadharisha waume zao dhidi ya marafiki wabaya.
- Anaendeleza maudhui ya uwajibikaji kwenye ndoa
- Anajenga wahusika wengine kama vile mzee Makucha

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

***Msemo***

- Jambo usilolijua  ni usiku wa giza ( UK 16)
- Akimpaka vumbi mbele ya mkewe ( UK 16)
- Unayepakwa mafuta kwa mgongo wa chupa ( UK 17)
- Ndio mwanzo ukoko unaalika maua. (UK 18)

***Nahau***

- Ujana ulikwisha kumpa kisogo ( UK 18)

***Tashbihi***

- Alisimama mahali alipokuwa kama sanamu. ( UK 22)

## 4. HARUBU YA MAISHA-*Paul Nganga Mutua*

### MTIRIRIKO

Hii hadithi ya Kikwai, mhusika mkuu anaeleza changamoto chungu nzima anazozipitia kwenye familia na anakofanya kazi.
Mwanzo anapokea simu huku akiwa kazini ni simu ya mkewe, mama Mercy. Kwenye simu analalamikia kuchelewa kwake na kuwa mtoto wao angelala alikuwa akimsubiri. Hili lilimgusa Kikwai na akaamua kuharakisha safari ya kwenda nyumbani.
Njiani alipigiwa simu na mama yake ila hakuipokea. Hakukuwa na msongamano wa magari na hivyo alifika nyumbani haraka. Nyumbani kulikuwa na tatizo la kukosekana chakula, naye Mercy alikuwa analalamika kuhisi njaa. Mkewe naye alikuwa analalamikia kuachwa bila pesa. Hapo hapo, alikumbuka kumpigia mamake simu naye mambo yalikuwa yale yale, pesa! Mamake alikuwa anadai kuwa fundi wa nyumba alikuwa anadai malipo yake, na alikuwa anatishia kutwaa mifugo kwa malipo. Kikwai alimtuliza na kumwomba wawe watulivu na angetafuta suluhu.
Jioni hii Kikwai alienda kwa Vaite. Alimkopesha kwa heshima ya mkewe. Anaandaa chajio na kumlisha Mercy, kisha yeye akabaki kula. Chakula chenyewe kilikuwa na mwonjo wa mafuta taa. Mkewe alikataa kula na wanakuwa na mazungumzo kwa kina kuhusu hali ilivyo na mwishowe mama Mercy anamwambia Kikwai kuwa alifaa kwenda kazini na Mercy kwa sababu ya mtoto kukosa chakula mchana na kumsumbua mamake.
Alfajiri siku iliyofuata, kikwai anabumburushwa kutoka uzingizini na kilio cha Mercy. Alikuwa anahisi njaa. Hapa hapa kikwai alilazimika kujiandaa kwenda kazini.
Kikwai anapofika kazini, alimkuta Bosi wake ameshafika. Alimwulizia alikokuwa Nalikosi mfanyikazi mwenzake. Kikwai anamweleza kuwa Nilakosi anafanya tathmini ya mswada fulani wa riwaya. Bosi anamweleza kuhusu kumsitisha kazi contract yake ikiisha. Kikwai naye anamweleza Bosi kuhusu hali ngumu ya Nilakasi ya kifedha na hivyo alihitaji apewe advansi ili alipe kodi ya nyumba.
Bosi alipokea simu na baada ya hapo akamtuma Kikwai kumpeleka mtoto hospitalini. Hapo kikwai alimwambia hakuwa amekuja na gari kwa kukosa pesa za kununulia mafuta. Hapo bosi anamgombanisha.
Siku iliyofuata Kikwai na Nilakosi walienda kazini na kutoka wakiwa katika hali ile ile ya kukosa pesa. Jioni walirudi wakitembea kurudi nyumbani.

Kikwai alipotoka nyumbani palikuwa na pango jipya la mama tajiri aliyetaka kuasilisha mtoto wa kike kwa tudui kubwa. Kikwai anawaza sana na kutamani kupeana Mercy kwa sababu ya ule ulitima aliokuwa ndani.
Anatoka na kwenda kwa Bishop. Alimwomba chakula na hapo akapata riziki ya hiyo siku.
Keshoye Kikwai alipofika ofisini, Nilakosi hakuwa amefika kazi. Anapoendelea kuwazia hili anapokea ujumbe kutoka kwa Nilakosi kuwa hangeweza kufika kazini siku hiyo maana hali ilikuwa mbaya sana.
Muda mchache baadaye Bosi aliingia na kumpigia Kikwai simu aende ofisini kwake. Hapo hapo alimfuta na kumlipa pesa zake na kumwambia arejeshe mali yote ya kampuni.
Kikwai alienda nyumbani alasiri ile, akanunua vitu kadhaa vya matumizi ya nyumbani kwa duka la *Tuskys*, akaandaa chakula nyumbani na baada ya kupumzika kidogo, alichukua kipakatalishi chake na kuanza kupiga msasa tawasifu kazi yake. Aliona kuwa huu ulikuwa wakati wa kuchukua hatua nyingine ya kuendeleza maisha na katika hili bidii ilihitajika.

## DHAMIRA

- Mwandishi alidhamiria kueleza kinagaubaga changamoto za maisha ya ndoa kama vile alivyopitia Kikwai, mkewe na mtoto.
- Vilevile mwandishi alidhamiria kueleza chamgamoto wanazopitia wafanyikazi wengi kwenye maeneo yao ya kazi.
- Mwandishi pia alitaka kueleza umuhimu wa bidii na uvumilivu kwenye maisha ya sasa.

## UFAAFU WA ANWANI

Harubu ni hali ya kutokuwa na raha, taabu au hata adha.

- Harubu ya maisha ni changamoto zinazoishia kusababisha kukosa raha, kuwa na taabu.
- Kikwai anapitia hali ngumu inayomkosesha raha anapokosa kulipwa kazini kwa miezi miwili.
- Mercy anapitia harubu ya maisha anapokosa chakula. Hili linafanya kulia mchana na hata usiku.
- Mamake Mercy anagusia na kusababisha harubu ya maisha anapokosa mahitaji ya kimsingi ya nyumbani,na hata kukosa muda wa kutosha

wa kuwa na mumewe. Hili linamfanya kukasirika na hata kukataa kula.

- o Nilakosi harubu za maisha zinamsababishia kukosa kwenda kazini. Anasema kuwa hali ilikuwa mbaya sana. Kikwai pia anamwombea advansi kwa bosi kuwa alikuwa anaelekea kufungiwa nyumba kwa kukosa kodi.
- o Harubu za maisha zinamfanya Kikwai kuwazia kuasilisha mwanawe Mercy kwa yule mama tajiri kama vile ilivyokuwa kwenye bango la kuingia kwao. Vilevile analazimika kukopa chakula kwenye duka la Vaite na hata kwenda kuomba chakula kwa bishop.
- o Harubu za maisha zinajidhihirisha mamake Kikwai anapompigia na kumwambia kuwa mambo yalikuwa magumu nyumbani na yule fundi na nyumba alikuwa anadai malipo yake, hatulii.

**MAUDHUI.**

**NDOA NA CHANGAMOTO ZAKE.**

- Kikwai anapitia changamoto katika familia yake. Mwanzo anakosa fedha za kuikimu familia yake kiasi cha kulazimika kukopa chakula kwa duka la Vaite. Vilevile anaenda kwa bishop ili kumwomba chakula.
- Mercy, mwanawe Kikwai analia njaa mchana na hata usiku .
- Tunaelezwa hali aliyopitia Kikwai kwenye ndoa yake kuwa mwanzoni haikuwa mbaya vile kisha Mercy alipozaliwa akaja na changamoto zake zikiwemo: meno, mafua, kutia punje za mahindi puani na sikioni na kulazimisha miadi na daktari.
- Mamake Mercy anaonekana kukasirishwa na mumewe Kikwai kwa kutoweza kukimu familia na kutowapa muda wa kuwa naye nyumbani.
- Nilakosi anapitia changamoto za ndoa kukimu familia yake. Anatumia Kikwai ujumbe mfupi kuwa hali ilikuwa mbaya sana ndio maana anakosa kwenda kazini.
- Bosi anapitia changamoto za kifamilia mwanawe anapougua na kumtaka Kikwai kumpeleka hospitalini.
- Mama tajiri anapitia changamoto za kifamilia kwa kukosa mtoto. Hivyo aliandika bango kwenye lango la kuingia kwa Kikwai la kutaka kuasili mtoto wa kike.

## KAZI NA CHANGAMOTO ZAKE.

- Kikwai anafanya kazi kwa muda mrefu sana. Hii ndio maana mkewe anakasirika na kugombana kuhusu hili.
- Familia ya Kikwai inapitia changamoto nyingi kwa kukosa fedha za kuwakimu kwa sababu ya kutolipwa kazini kwa muda wa miezi miwili.
- Kikwai analazimika kukopa chakula kwa duka la Vaite na hata kuomba chakula kwa bishop. Ukosefu huu wa hela unasababisha Kikwai kuwazia kuasili mwanawe Mercy.
- Nilakosi anapitia hali ngumu ya kukosa kulipwa kazini. Anamtumia Kikwai ujumbe mfupi kuwa hangefika kazini kwa kuwa hali ilikuwa mbaya sana. Vile vile Kikwai alimwambia bosi kuwa Nilakosi alikuwa anaomba advansi ili alipe kodi asije kufungiwa nyumba.
- Kikwai anatakikana kwenda kazini na gari la kampuni ilhali hajalipwa kwa miezi miwili na hakuwa na pesa za kununulia gari mafuta. Hili linasababisha kufutwa kazi kwake.
- Nilakosi na Kikwai wanalazimika "kuuponda wa fisi" Hii ni baada ya kukosa kulipwa mshahara wao na hata wanakosa pesa kidogo za nauli.
- Bosi anadai kuwa yeye binafsi hajalipwa kwa kipindi karibia miezi minne.
- Bosi alipanga kufuta Nilakosi ikiwa kazi ilikuwa kidogo kwake na kama contract yake ilikuwa imeisha.(uk 29)
- Mwishonii mwa hadithi, Kikwai anachukua kipakatalishi chake na kuanza kupiga msasa tawasifu kazi yake. Anaamua kukabiliana na changamoto za kazi na maisha, ambapo mwenyewe anajua kuwa bidii ilihitajika.

## WAHUSIKA

### 1. KIKWAI

Ni babake Mercy na mumewe mama Mercy.

**Sifa zake.**

***Ni mwenye bidii***

- Anajikaza na kwenda kazini hadi kufutwa licha ya changamoto ya kukosa kulipwa miezi miwili.
- Alitembea hadi kazini na hata kutoka kazini kwa miguu.
- Mwishoni mwa hadithi, hata baada ya kufutwa kazi anaanza kupiga msasa tawasifu kazi yake na kujiandaa kusonga mbele na maisha. Hili kutekeleka anasema kuwa bidii inahitajika.

***Ni mvumilivu.***

- Alivumilia kwa kuendelea kufanya kazi licha ya kutolipwa kwa kipindi cha miezi miwili. Alihisi machozi yanatunga kwenye ncha za macho lakini akajikaza kimwanaume.(uk26)
- Alitembea kwa miguu kwenda na kutoka kazini alipokosa pesa za nauli.
- Alivumilia kuzomewa na bosi wake licha ya kwamba bosi wake ndiye alikuwa na makosa.

***Ni mwenye kuwajibika.***

- Aling'ang'ana kuikimu familia yake licha ya kukosa kulipwa mshahara kwa miezi miwili.
- Alikopa chakula kwa duka la Vaite na hata kwenda kuomba chakula kwa bishop.
- Alipika chakula na kumlisha Mercy.

***Ni mwenye mapenzi***

- Alimpenda mkewe na mwanawe Mercy licha ya changamoto nyingi walizokuwa wakipitia**.**

***Ni mwenye kujali***

- Anamjali rafikiye na mfanyikazi mwenzake Nilakosi, ndio maana alimwombea advansi kwa bosi wake. Vilevile anashtushwa na kufika kazini na kupata kuwa hakuwa amefika kazini.

**Umuhimu wa Kikwai**

- Anawakilisha watu ambao ni wavumilivu kazini. Anavumilia na kuendelea kufanya kazi licha ya kutolipwa miezi miwili

- Anaendeleza maudhui ya uvumilivu. Alivumilia kazini huku akiwa halipwi
- Anaziumbua sifa za bosi kuwa ni katili

**2. NILAKOSI**

Ni mfanyikazi mwenza wa Kikwai

**Sifa zake**

***Ni mvumilivu***

- Alivumilia hali ngumu ya maisha kazini. Hata hivyo bado alienda kazini hata kwa miguu.

***Ni mwenye bidii***

- Kikwai anasema kuwa Nilakosi alikuwa anafanya tathmini ya mswada fulani wa riwaya. Ashamaliza usomaji wenyewe, sasa anaandika ripoti ya tathmini yake.

***Ni mkwasi***

- Kikwai anasema kuwa Nilakosi ana kipawa cha kutumia lugha kwa namna za kuchekesha. (uk30)

**Umuhimu wa Nilakosi**

- Anawakilisha wafanyikazi wanaopitia magumu kazini
- Anaendeleza maudhui ya bidii.

**3. MAMA MERCY**

Ni mkewe Nilakosi.

**Sifa zake**

***Ni mwenye mapenzi ya dhati***

- Anamjulia hali mumewe kazini. Ndio maana anampigia simu na kumwuliza mbona alichelewa.
- Vilevile analalamikia mumewe kutokuwa na muda nao kama familia ndio maana mtoto angemsahau.

***Ni mwenye malalamishi.***

- Analalamikia hali ilivyokuwa mbaya kwa mumewe kudai kuwa hawajalipwa n.k

***Ni mwenye hasira.***

- Anaghadhabishwa na kuliliwa na mtoto huku hana chakula cha kumpa hadi akamwambia Kikwai aende na mtoto kazini.

**4. MERCY.**

Ni mwanawe Kikwai na mama Mercy

**Sifa zake**

***Ni mtoro***

- Alitia punje la mahindi puani au sikioni na kulazimisha miadi na daktari
- Hakuelewa lugha ya "hakuna". Maisha yake ni kutaka akapata. Akikosa atalia mpaka usingizi umtwae.

***Ni mchangamfu***

- Siku ile baada ya kushiba na kwenda kucheza na rafiki zake nje, anajitoma ndani ya nyumba na kusema "Dadii *nashkia* nimeshiba"

**5. BOSI**

Ndiye mwajiri wa Kikwai na Nilakosi

**Sifa zake.**

***Ni katili***

- Alitarajia Kikwai kuenda kazi na gari licha ya kutomlipa mshahara kwa muda wa miezi miwili.
- Alimfuta kazi Kikwai kwa kizingizio cha kutoenda kazini na gari.
- Anapanga kumfuta kazi Nilakosi punde tu contract yake ikiisha.

***Ni mwajibikaji***

- Anamtuma Kikwai kumpeleka mwanawe hospitalini aliyeugua. Hii linaonyesha uwajibikaji kwa familia yake.

***Ni mwenye kujali***

- Anaonyesha mapenzi kwa wafanyikazi wake mfano kwa kumpa gari Kikwai la kampuni kwa usafiri wake.

**Umuhimu wa Bosi**

- Anaendeleza maudhui ya ukatili. Anamfuta kazi Kikwai kwa kisingizio cha kutoenda kazini na gari ilhali hajamlipa.
- Kupitia kwake tunapata sifa za Kikwai kuwa ni mvumilivu
- Anawakilisha waajiri ambao ni katili katika jamii. Anakosa kuwalipa Kikwai na Nilakosi

**6. BISHOP**

***Ni mkarimu***

- Anampa Kikwai usaidizi wa chakula alipoomba.

***Ni mcha Mungu***

- Anaposalimiwa na Kikwai anajibu kwa kusema, “Bwana amekuwa mwaminifu” (uk31)

**7. VAITE**

***Ni mkarimu***

- Alimkopesha Kikwai chakula kwenye duka lake.

***Ni mwenye utu***

- Alimwelewa Kikwai na hali yake na kumkopesha chakula licha ya kuwa alikuwa analifunga duka wakati huo.

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Uhuishaji/Tashhisi**

- ★ Niliweza kunusa harufu ya hasira katika maneno yake (uk26)
- ★ Kama njaa niliyokuwa nayo ingeniruhusu kulala (uk 26)

**Dayolojia**

- ★ Kuna mazungumzo kati ya Kikwai na mwanake Mercy (uk25)

- ★ Kuna mazungumzo kati ya Kikwai na mamake Mercy. (uk 26)
- ★ Kuna dayolojia kati ya Kikwai na Bosi

**Nidaa**

- ★ Mama Mercy! (uk26)
- ★ "Dadii nashkia njaa sana!" (uk26)
- ★ Chakula kina harufu ya mwonjo wa mafuta taa! (uk26)
- ★ Usiniulize maswali! Unajua ninachomaanisha! (uk27)
- ★ Yametosha basi! (uk 27)
- ★ Mama! Naomba mnivumilie tu! (uk28)

**Kuchanganya ndimi**

- ★ ……bad coincidence…(uk26)
- ★ It is virtually unsustainable kuwa na wafanyikazi wengi (uk 29)
- ★ Contract yake inakatika lini? (uk 29)
- ★ "Okay" (uk29)
- ★ …kwa ajili ya emergencies (uk30)
- ★ He is now stable….naam (uk32)

**Maswali ya balagha**

- ★ Unanielewa…? (uk 26)
- ★ …tena hapo hapo katika chumba kimoja?…(uk 26)
- ★ "Unalala nini sasa?" (uk 27)
- ★ Na mshahara? (uk27)
- ★ "kila siku hujalipwa?….mpaka lini? (uk 27)
- ★ Mbona sikuelewi? (uk27)
- ★ Kama yapi? (uk27)
- ★ Atachukua simu katika majira haya? (uk 27)
- ★ Contract yake inakatika lini? (uk
- ★ Unasemaje wewe? (uk 30)
- ★ Unatoa mfano gani kwa wenzako kazini? (uk 32)

**Msemo**

- ★ Kuongeza msumari wa moto kwenye kidonda kibichi. (uk26)

**Methali**

- ★ Kila msiba huandamwa na mwenziwe (uk 26)

**Kubadili msimbo.**

- ★ Out of danger…..absolutely (uk 32)

**Mdokezo**

- ★ Kila siku hatujalipwa?……(uk 27)
- ★ Dadii nashkia njaa……(uk 26)
- ★ …kisha nianze safari…(uk 25)
- ★ "pole, mama. Nimefika…" (uk 25)
- ★ ….ulichoshindwa kukizumbua…(uk 25)
- ★ Tuweze kusukuma siku ….(uk 27)
- ★ Mama analia…. (uk 28)
- ★ Unasema yuko wapi….? (uk 30)
- ★ Kisha akaendelea….haya…(uk 30)
- ★ Nikaona heri kusubiri…..(uk 30)
- ★ Nitafanya tu bora jamaa yangu ipate chakula…..hata cha leo tu…" (uk 30)
- ★ Mwenyewe unionavyo sijalipwa kwa karibu miezi minne…" (uk 32)
- ★ Nikawa sina budi ila kuliacha gari…" (uk 32)

**Uzungumzi nafsi**

- ★ Atapokea simu majira kama haya? (uk27)
- ★ ….si aliwahi kunieleza kuwa hapo kwake hapawezi kukosa chakula? Hapo ndipo riziki yangu leo! (uk 31)

**Takriri**

- ★ Mara meno mara mafua (uk29)
- ★ Mambo yalikuwa yale yale (uk30)

**Utohozi**

- Advansi (uk29)
- Shillingi (uk29)
- Ofisi
- Bosi

**Nahau**

- Kuchapa kazi (uk30)
- Nafa njaa (uk 31)

**Tashbihi**

- Na usingizi wa mtu mwenye njaa ni adimu kama mikoko jangwani. (uk31)

**Sadfa**

- Ni sadfa kuwa kadri Kikwai anapowazia hali ya maisha ilivyokuwa ngumu, ndipo anapoingia kwenye lango kuu la kuingia kwao. Anapatana na bango kubwa la mama tajiri wa mali aliyetaka kuasilisha mtoto tena wa kike naye Kikwai mwanawe ni Mercy, wa kike. Hapo wazo la Mercy linamjia Kikwai. (uk 31)
- Punde tu Kikwai anapowazia aliko Nilakosi, kuwa hajafika, hapohapo hazikupita dakika mbili arafa ya Nilakosi iliingia, kuwa hakuwa anakuja kazini hali imekuwa mbaya sana (uk32)

**Kinaya**

- Ni kinaya kwa bosi kuona ampunguzie Kikwai taabu kwa kumfuta kazi, hili badala yake litakuwa la kumwongezea taabu.
- Ni kinaya kuwa Bosi hawezi kumlipa Kikwai pesa zake kawaida tu, ila anapomfuta anamlipa pesa zake zote hapo hapo.
- Ni kinaya Bosi kumgombanisha Kikwai kwa kutoenda kazini na gari ilhali Kikwai hakuwa na pesa za kuweka gari mafuta.

- ★ Ni kinaya kuwa kikwai anadai kuwa hana pesa kwa mkewe na mamake ilhali yuko kazini na hata hutoka kama amechelewa.
- ★ Ni Kinaya Bosi anasema kuwa pesa zake zimechelewa miezi minne sasa.

**Taharuki**

- ★ Msomaji anaachwa na taharuki na kujiuliza maswali chungu nzima iwapo Kikwai alipata kazi baadaye au la.
- ★ Hatujui kama Kikwai alirejesha mali ya kampuni aliyokuwa nayo.
- ★ Hatufahamu kama Nilakosi alifutwa kazi au la? Bosi alimpa pesa zake au la?
- ★ Msomaji anatamani kujua iwapo Nilakosi alipewa advansi na Bosi au la? Ama kama landlord alimfungia nyumba au la?
- ★ Msomaji ana taharuki ya kujua iwapo fundi wa nyumba alitulia ama alitwaa mbuzi na kuku ili kujilipa na kama Kikwai alimtumia mamake hizo pesa au la.
- ★ Msomaji hajui kama Kikwai alimlipa Vaite pesa zake au hakumlipa.

## 5. SABINA-Winnie Nyaruri Ogenche

## MTIRIRIKO

Jumapili ya mwisho kabla ya mtihani wa taifa wa darasa la nane iliibua hisia mseto ndani ya moyo wa Sabina. Alifikiria kuhusu mtihani uliodhamiriwa kuanza siku ya Jumanne. Mtihani ambao ugemwenzesha kupata ufadhili katika shule ya upili ya bweni ikiwa angepita vyema.

Kabla ya kwenda shule alitakiwa kutekeleza yaliyokuwa ada yake . Aliwakama ng’ombe akapeleka kisonzo shambani, kisha akaenda kuuza maziwa. Sabina alikuwa na miaka kumi na minne . Mamake Nyaboke alimzaa akiwa mwanafunzi wa kidato cha pili, naye alimlea mwanawe kwa shida sana . Kwa bahati mbaya aliaga kutokana na kipele kilichotokeza shingoni. Akiwa darasa la tano nyanya na babu yake waliaga kutokana na jiko la makaa walilotumia kuchoma mahindi usiku huo.

Ilibidi Sabina kuridhia kuishi na mjomba wake Ombati na mkewe Yunuke. Mwanzoni mambo yalikuwa magumu kutokana na majukumu mazito aliyopewa lakini baadaye alipata uzoefu. Wakati wa mtihani mwalimu alimnusuru kuuza maziwa asubuhi . Badala yake aliwaandikia wapishi barua ya kumruhusu Sabina kupeleka maziwa shuleni.

Mwezi mmoja baada ya mtihani kukamilika, Ombati alifika kijijini kwa ajili ya likizo ya mwezi wa Desemba pia alifika kwa maandalizi ya kumpeleka mkewe katika shule ya upili. Ripoti za Yunuke kwa mumewe kuhusu jinsi Sabina alivyofanya mumunye la kuharibikiwa ukubwani zilimfanya aanze mipango ya kumwona mara moja. Matangazo ya mtihani wa taifa yalimkuta Sabina shambani huku mjomba wake anafanya matayarisho ya kupokea mahari.

Punde wageni watarajiwa waliwasili tayari kumchukua mke wao. Wakati wanaendelea kula, umati wa watu waliokuwa wakiimba nyimbo za kusifu Sabina ulifika pale. Alipofika walimzoa kunukuu na kuanza kuimba. Ombati alijitambua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni. Sabina alijishika tama na kuvuta kumbukumbu ya maisha yake. Kila siku Yunuke alimkumbusha kuwa alikuwa kiokote. Maisha magumu kweli lakini natokwa mazuri.

**DHAMIRA**

- Lengo la mwandishi ni kueleza matatizo yanayomkumba mtoto wa kike.

**ANWANI**

- Sabina ni mhusika mkuu na anapitia changamoto mbalimbali baada ya mamake kufa na nyanya na babu yake kufa pia.
- Anaishi na mjomba wake Ombati ambapo mkewe anamfanyisha kazi ngumu kila asubuhi kabla kwenda shuleni. Aliwakama ng’ombe, kuzoa kisonzo, kuuza maziwa, kuwapeleka mifugo malishoni na kazi zote za nyumbani.

- Sabina alifaulu mtihani wake wa kitaifa licha ya kuwa na majukumu chungu nzima. Yunuke na Ombati hawakutaka kumwachilia hata sekunde.

## MAUDHUI

### *Ukatili / dhuluma*

- Sabina alitakiwa kukama ng'ombe, kuzoa kisonzo, kuuza maziwa, kuwapeleka mifugo malishoni na kutekeleza majukumu yote ya nyumbani kabla ya kwenda shuleni. ( UK 36)
- Shule zilipofungwa hakupata afueni yoyote kwani binamu zake walimzidishia kazi badala ya kumpunguzia. Walimgeuza Sabina kijakazi, walimwita awafanyie hili au lile. ( UK 36)
- Badala ya Yunuke kuhakikishiwa na wanafunzi waliosoma na Sabina kwamba matayarisho ya mtihani yalikuwa yamekamilika naye Sabina hajafika, alipofika kabla ya kutoa mkoba, Yunuke alimrukia kama simba anayelivamia windo lake. Alimcharaza kwa bakora mfululizo bila kusema lolote. ( UK 38)
- Ripoti za Yunuke kwa mumewe jinsi Sabina alivyokuwa mumunye la kuharibikia ukubwani zilimfanya aanze mipango ya kumwoza mara moja. ( UK 39)

### *Mauti / kifo*

- Mamake Sabina ( Nyaboke ) aliaga kutokana na kipele kilichotokeza shingoni. Kipele kilichotunga usaha na kuvimba.
- Nyanya na babu yake waliaga kutokana na jiko la makaa walilotumia kuchoma mahindi usiku. Milango na madirisha yalifungwa kiasi cha kutopata hewa wala kutoa nje moshi.

### *Ushirikina*

- Kipele kilichotokeza shingoni mwa mamake Sabina na kusababisha kifo chake, kilisemekana kuwa alilaaniwa na babake mzazi kwa kujifungua akiwa nyumbani kwao.

- Wengine walishikilia kuwa mamake alimlaani kwa kosa la kuwakataa wanaume wote waliofika nyumbani kwao kumchumbia.
- Wapo walioamini kuwa laana iliyomwandama Nyaboke ilitokana na ndugu yake , Ombati. Walisema kuwa Ombati alitazamiwa kujitajirisha kutokana na mahari ya dadake. ( UK 35).

***Bidii***

- Sabina alitia bidii masomoni. Alisoma usiku akitumia kibatari alipomaliza kazi. Hata wakati mwingine Mike alizoea kubeba vitabu vya kudurusu ambavyo walidurusu na Sabina wakiwa katika kazi ya uchungaji.
- Nyaboke alijifunga kibwebwe vibaruani ili kuhakikisha kuwa alimtimizia bintiye mahitaji ya kimsingi.

## WAHUSIKA

### 1. Sabina

**Sifa zake**

***Mwenye mawazo***

- Kichwa chake kidogo kilikuwa uwanja wa mawazo ainati yaliyomchezea.

***Ni Mwoga***

- Alimwogopa sana Yunuke ndio maana alipomwita alizinduka ghafla kutoka kwa mawazo na kwenda kutekeleza majukumu ambayo alikuwa hajafanya.

***Ni Mvumilivu***

- Alivumilia madhila yote aliyotendewa, ikiwemo kukamua ng’ombe, kuuza maziwa na hata kwenda shuleni akiwa amechelewa.

***Ni Msomi***

- Anasoma kwa bidii na kupita mtihani licha ya changamoto alizokumbana nazo.

***Ni Mtiifu***

- Alifanya kila kitu ambacho alitakiwa kufanya bila kulalamika.

**Umuhimu wa Sabina**

- Anaendeleza maudhui ya  elimu. Anasoma kwa bidii na kuupita mtihani wake.
- Anaziumba sifa za Yunuke kuwa ni katili . Anatesa Sabina kwa kumpea kazi nyingi asubuhi kabla ya kwenda shuleni.
- Ni kielelezo cha wasichana ambao hupitia matatizo wanapokuwa hasa mayatima  ambao huishi kwa wajomba.

2. **Yunuke**
   **Sifa zake**

***Ni Katili***

- Anampa Sabina kazi nyingi za kufanya kabla ya kwenda shuleni.

***Ni Mwongo***

- Anamdanganya mumewe kuhusu jinsi Sabina alivyokuwa mumunye la kuharibikiwa ukubwani.

***Ni Mnafiki***

- Sabina aliposhinda katika mtihani Yunuke na Ombati hawakutaka kumwachilia hata sekunde.

**Umuhimu wa Yunuke**

- Anawakilisha watu ambao huwafanya watoto mayatima kuwa vijakazi na kujifanya ati wanawasaidia.

**3. Ombati**

**Sifa zake**

***Ni Katili***

- Anaamini yale yote anayoambiwa na mkewe kumhusu Sabina na ndio maana anaanza mipango ya kumwoza mara moja.

***Ni Mnafiki***

- Anasema kuwa anafurahi bintiye kufaulu katika mtihani ilihali alitaka kumwoza na pia alitaka Mike kupita.

**Umuhimu wa Ombati**

- Kielelezo cha wajomba ambao hawawajibiki maelezi ya watoto wa ndugu zao wakati wanapoaga.
- Anaendeleza maudhui ya ukatili

**4. Nyaboke**

**Sifa zake**

***Mwenye bidii***

- Alijifunga kibwebwe vibaruani ili kuhakikisha kuwa alimtimizia bintiye mahitaji ya kimsingi.

**5. Mwalimu mkuu**

**Sifa zake**

***Ni Mwenye huruma***

- Alimhurumia Sabina na kumruhusu kupeleka maziwa shuleni.

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

***Mbinu rejeshi***

- Sabina anakumbuka maneno ya mwalimu mkuu kuwa "Mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu lazima mtie bidii".

- ★ Mjomba wake Sabina anaposema kuwa ana furaha kubwa bintiye amefaulu mtihani, Sabina alivuta kumbukumbu ya maisha yake. Yunuke alimkumbusha kuwa alikuwa kiokote.
- ★ Alikumbuka wakati wa mtihani wa kitaifa alivyokuwa na majukumu chungu nzima.
- ★ Alikumbuka hisani ya mwalimu mkuu ya kumnusuru kwenda kuuza maziwa asubuhi.

**Tashihisi**

- ★ Kichwa chake kidogo kilikuwa uwanja wa mawazo ainati yaliyomchezea.

***Msemo***

- ★ Kuyazika katika kaburi la sahau. ( UK 34)
- ★ Kulea mimba si kazi, kazi ni kulea mwana. ( UK 34)

***Kinaya***

- ★ Ni kinaya Ombati anaposema kubwa amefurahi binti yake kuupita mtihani ilhali alimtaka Mike kuupita mtihani.
- ★ Ni kinaya kwa Yunuke kusema kuwa Sabina hakuwa na akili za masomo ati akili zinachangamkia barua na mambo ya wanaume ilhali ni uongo. Na mwishowe akapita mtihani wake.

***Methali***

- ★ Mtaka cha mvunguni sharti ainame. ( UK 34)
- ★ Ganga Ganga za mganga humwacha mgonjwa na matumaini. ( UK 35)
- ★ Mtoto wa nyoka ni nyoka. ( UK 39)

***Mdokezo***

- ★ Yeyote atayechelewa kufika ........

***Nahau***

- ★ Alipigwa na butwaa. ( UK 34)
- ★ Kuchana mbuga. ( UK 38)

***Sadfa***

- ★ Inasadifu kuwa wageni watarajiwa waliwasili tayari kumchukua mke wao. Wakati wanaendelea kula, umati wa watu waliokuwa wakiimba nyimbo za kumsifu Sabina ulifika pale.

***Tashbihi***

- ★ Amefurisha shingo kama kiboko. ( UK 35)
- ★ Alikimbia kama mwehu hadi nyumbani. ( UK 35)
- ★ Miguu ya Sabina ilikufa ganzi akabaki amesimama kama kisiki. ( UK 37)

***Takriri***

- ★ Sabina ..... Njoo : Sabina nenda......Sabina leta...... Sabina kimbia...

## MTIRIRIKO

Mzimu wa kipwerere ni hadithi inayojikita kufichua unafiki, hadaa kama vile uzinzi na ulauguzi wa dawa za kulevya.

Hadithi inaanza huku msimulizi akielezea imani na mtazamo wa kutisha uliokuwepo kuhusu mzimu wa kipwerere. Anasema ulikuwa kichaka kidogo cha miti mseto yenye mshonano wenye giza. Kichaka hiki kilitisha na kupewa jina la mzimu.

Mzimu huu pia katikati yake ulikuwa na kichanjaa ( uwanja) kikubwa Chenye uwazi wa kiasi cha hekari moja. Mzimu huu uliitwa wa kipwerere kwa kuwa baada ya kipwerere kufariki , inasemekana alizikwa hapo. Baada ya kuzikwa tu, kichaka kikubwa cha moto kikaota za hapo kichaka hicho kikawa mzimu kwani kulitokana na kaburi la mwanamema huyo aliyeitwa kipwerere ( Kipwerere alikuwa yule jamaa yake bwana Musa aliyepata shetani aliyefichua damu siku zile za ujahiliya ( kipindi kijana anapobalegha na kiasi sheria au desturi za kwake). Kifupi ni kuwa ilikuwa dhahiri kuwa kumbe kichaka kilichounda mzimu kiliota kutokua na kuzikwa mtu aliyekuwa akitisha kwa nguvu za miujiza, nyakati hizo. Hii iliongeza sababu ya mzimu wa kipwerere kuwa kitisho cha aina yake.

Mzimu wa kipwerere ulizingirwa na eneo tambarare lililobaki bola kutumiwa kwa shughuli ya makaburi ya watu wenye utukufu katika jamii hiyo. Kulikuwa na miiko iliyohusishwa na mzimu wa kipwerere- yeyote hakuruhusiwa kuingia maeneo hayo usiku. Vilevile yaliruhusiwa tu kwa wazee wa mji au wahenga wenye utukufu. Yeyote angevunja miiko hii angetolewa kafara.

Wakati wa usiku mzimu huu ungeonekana mwanga wa taa, kungesikika sauti za wanawake na wanaume wakizungumza kwa sauti ya chini. Vilevile ungesikia harufu ya vinywaji na dawa za kulevya. Mzimu huu pia ulikuwa na uongozi- salihina alikuwa mdhamana mkuu wa mzimu. Haya yote yalimpa msimulizi hamu ya kuingia Mzimuni kujua hali halisia.

Siku moja baada ya kudadisi, hata kujua wimbo wa kuingia kule msimuni, msimulizi aliingia na kupata hali halisi ya yaliyokuwa yanatokea mle. Mwanzo mlikuwa na Makanda na makasha ya tumbaku, unga wa kulevya na bangi kwenye marobota. Kulikuwa na mapipa yaliyojaa chang'aa na tembo ya mnazi. Palikuwa pia na kitanda cha besera.

Kidogokidogo aliingia salihina na Bishoo, mke wa mvuvi. Baada ya nyimbo za kuruhusiwa kuingia. Baada ya kutambulishana kwa nyimbo waliingia na kufanya mazungumzo karibu na kile kitanda huku msimulizi amejificha mvunguni. Walifanya mazungumzo mengi kuhusu mipango yao ya ulanguzi na usafirishaji wa dawa za kulevya. Baada ya hapo, walianza shughuli za utumizi wa dawa za kulevya. Ulevi uliponogea waliimba na kuserevuka. Walisogea pale kitandani na walipokuwa karibu kuanza tendo lao, kabla ya kuwasha kibatari, msimulizi alijitokeza mvunguni na maguo yake meupe kama maziwa na kuangua Mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama. Mwanamke yule alianguka pale pale na kuzimia . Hakuamka tena hadi asubuhi. Salihina naye huku akijaribu kukimbia , kanzu lake lilinasa kwenye mti na kumzuia asikimbie, akaanza kulalama na kupiga mayowe ya Mwangwi.

Msimulizi aliondoka mle Mzimuni huku akiamini kuwa kisanga kile kingechuma hadi asubuhi na siri zote za mzimu wa kipwerere zingefichuka! Waliogopa kiasi cha kuuabudu ingefichuka kuwa ulikuwa ulaghai, unafiki na uovu uliokuwa ukitendeka mle wala sio walivyojua siku hizi zote.

## DHAMIRA

- Mwandishi alidhamiria kufichua maovu ya kijamii yanayofanywa kisiri na kinafiki kama vile uzinzi na ulanguzi wa dawa za kulevya.
- Alipania kufunza kuwa, licha ya maovu yanayofanywa kisiri na kinafiki kufanywa, huishia kufichuliwa na kuwa na adhabu yake baadaye.

## MAUDHUI

### *Usaliti*

- Bishoo anamwita Salihina muadhama- neno la kutanguliza kutaja jina la kiongozi wa madhehebu, ilhali amekuja kwa mipango na shughuli za kukagua dawa za kulevya na vilevile uzinzi. Huku ni kusaliti dini.
- Bishoo anamsaliti mumewe kindoa kwa kwenda kuzini na salihina. Ana mume mvuvi na siku hizi anamdanganya kuwa ameenda kumjulia hali mtoto wa jirani ambaye ni mgonjwa.
- Salihina anaiita kazi ya ulanguzi wa dawa za kulevya kuwa takatifu na uadilifu mkubwa. (UK 46)
- Bishoo kumwacha mumewe ambaye mchana mzima alikuwa anaumwa na jino na mchana kutwa alikuwa akigaragara kwa maumivu ili kwenda kuzini na salihina, ni usaliti. Alifaa kumshughulikia mumewe mgonjwa.

***Utumizi wa dawa za kulevya***

- Salihina na Bishop wanapanga mipango na mikakati ya kusambaza dawa za kulevya. Wanapanga kutumia wanawake kusafirisha dawa hizi huku wakijifanya kwenda kuchotea maji shetani wa Mzimuni huku wamezitia dawa zenyewe kwenye ndoo badala ya maji.
- Salihina baada ya mazungumzo ya kutayarisha dawa za kulevya na Bishoo, alianza kujishughulisha na kujisahau kwa kunywa vinibu vya mnazi. Alivuta pande la msuba lililohanikiza harufu mbaya.
- Msimulizi anasema kuwa, siku ile alipoingia ndani ya mzimu wa kipwerere, alichokiona huko hakuamini macho yake. Mle ndani ya mzimu mlikuwa na Makanda ya tumbaku, unga wa kilevi na bangi kwenye marobota. Vilevile kulikuwa na mapipa yaliyojaa chang’aa na tembo ya mnazi. (UK 45)
- Msimulizi katika udadisi wake na hamu ya kujua kilichokuwa kinaendelea kwenye mzimu wa kipwerere, siku waliokuwa wakipita karibu na ule mzimu, walisikia harufu kali ya sigara au tumbaku kali au aina fulani ya kileo kinachofanana na tumbaku. Walipouliza kama kawaida hawakosi jibu, waliwaambia mashetani wengine huvuta sigara, tumbaku na kila aina ya vileo kama wanadamu. ( UK 43)
- Msimulizi anasema kuwa katika kijiji hiki kuvuta aina yoyote ya kileo cha tumbaku kilikuwa marufuku na kungeweza kugharimu hata maisha ya mtu. Vilevile kubwia unga na hata kunywa pombe yalikuwa

makosa ya jinai ingawa pamoja na juhudi zote hizi za kuzuia dawa kama hizi, mji wa watu hawa uliongoza kwa uagizaji, usambazaji na hata utumiaji wa vileo na dawa za kulevya. Msimulizi alijiuliza wapi dawa hizi zinatoka, nani anazileta na nani anazisambaza. ( UK 43- 44)

***Utamaduni***

- Msimulizi anasema kuwa mzimu wa kipwerere ulikuwa na miiko yake, miongoni mwa miiko hiyo, ilimpasa mtu yeyote asipite kichakani pale, haikuruhusu yeyote kupita eneo lile majira ya usiku. Vilevile hapakuwa na ruhusu kwa mtu yeyote kuingia mle kichakani ikiwa si mmoja kati ya wazee wa mji au wahenga watukufu waliotukuka. Iwepo yeyote angevunja miiko hiyo, basi angetolewa kafara. ( UK 42)
- Salihina alikuwa mzee wa kijiji na mdhamana mkuu wa mzimu. Yeye ndiye alikuwa mtendaji mkuu wa shughuli za kimila kama vile matambiko na ugotozi wa jambo lolote litakalofanywa katika kijiji au kwa mwanakijiji.
- Katika jamii hii kulikuwa na maadili yaliyowekwa na yeyote aliyevunja maadili na mila za wahenga. Kulikuwa na adhabu mfano wa ile aliyopewa msimulizi ya kuchapwa viboko kumi kwa kosa la kusimama na msichana mmoja wa makamo pembeni yake.

***Ulaghai***

- Wananchi wanalaghaiwa na kutishwa kuhusu mzimu huu wa kipwerere. Ilisemekana ilikuwa mwiko kwa yeyote kupita kichakani pale majira ya usiku isipokuwa wazee wa mji na wahenga wa mji wenye utukufu uliotukuka, kumbe ilikuwa njama ya kufanya maovu sehemu hii. ( UK 42)
- Msimulizi alipouliza wazee ili kupata ufafanuzi kuhusu sauti za watu za mwanamke na mwanaume usiku wa mapema kwenye ule mzimu wa kipwerere, wazee waliwalaghai na kuwadanganya kuwa mle ndani shetani wa mzimu ana mke na mara nyingi ukiskia wakiongea basi ujue watoto wamelala. ( UK 43)
- Ungepita karibu na ule mzimu ukiskia harufu kali ya sigara au tumbaku kali au aina fulani ya kileo kinachofanana na tumbaku,

unapouliza wazee , kilaghai wangejibu kuwa mashetani wengine huvuta sigara, tumbaku na kila aina ya vileo kama wanadamu. ( UK 43)

- Wazee wa mji na wahenga waliotukuka wanawalaghai wananchi kuwa mzimu wa kipwerere lilikuwa eneo hatari na ilikuwa na mashetani, kumbe eneo hili lilikuwa linatumiwa kuendeleza uovu wa kupanga na kutumia dawa za kulevya na vilevile usherati kama anavyofanya salihina na Bishoo.
- Bishoo anamlaghai mumewe kuwa usiku huo alikuwa ameenda kwa jirani kumjulia hali mtoto wake mgonjwa, kumbe alikuwa amepanga mtindo ya uzinzi na ulanguzi wa dawa za kulevya na salihina. ( UK 47)
- Bishoo anatoa mikakati ya usambazaji na uuzaji wa dawa za kulevya. Anasema “ Tunachukua vyombo tunasema tunaenda kuchotea maji shetani wa mzimuni. Hapo hakuna anayetutilia shaka. Hata polisi hawatatushughulikia. Wakati huo , kila ndoo tunaijaza mizigo badala ya maji” Huu ni ulaghai na udaganyifu wa hali ya juu. ( UK 46)

**WAHUSIKA**

1. **Msimulizi**

   **Sifa zake**

***Ni mwenye shauku***

- Anatilia shaka majibu anayopewa na wazee kuwa waliokuwa wakiongea kwenye mzimu wa kipwerere alikuwa shetani na mkewe wakati watoto wao wamelala. ( UK 42- 43).
- Hakuamini usemi wa wazee kuwa harufu kali ya sigara au tumbaku kali au aina fulani ya kile kinachofanana na tumbaku iliyosikika kule kwenye mzimu wa kipwerere , eti mashetani wengine huvuta sigara , tumbaku na kila aina ya vileo kama wanadamu. Hii ndio maana alifanya udadisi na kuishia kujua ukweli wake.

***Ni mdadisi.***

- Anasema kubwa , " Fikira na mawazo yangu juu ya mzimu yalitawala Mtima na akilia zangu siku hadi siku. Kadri siku zilivyosonga, moyo na akili yangu, tofauti na wengine vilikuwa zaidi katika baadhi ya udadisi ".( U k 44)
- Udadisi wa msimulizi ndio ulimwelekeza kwenda kwenye mzimu wa kipwerere na mwishowe kujua ulaghai uliokuwemo alipowafumania salihina na Bishoo. ( UK 47- 48)
- Alidadisi na kujua namna ya kuingia kule kwenye mzimu hata kabla ya kwenda siku ile mwenyewe . Hapo ndipo aliposhika ule wimbo wa ufunguo wa kuingia kule kwenye mzimu. ( UK 45)

***Ni jasiri***

- Hakuogopa kwenda Mzimuni licha ya vitisho vilivyokuwa vimewekwa kuwa mle Mzimuni mlikuwa hatari.
- Aliwashtua salihina na Bishoo wasiendeleze ushetani waliotaka kuendeleza kwa kuangua Mwangwi mkali mfano wa parapanda ya usiku wa kiama. Wawili hao walitoroka kwa woga sana. ( UK 47)

**Umuhimu wa Msimulizi**

- Kupitia kwake tunapata sifa za Salihina na Bishoo kuwa ni wanafiki.
- Anawakilisha wanajamii ambao wanapinga maadili mabaya katika jamii.
- Ni kielelezo cha vijana jasiri wanaofanya udadisi na kujua chanzo cha matukio na imani zilizowekwa.

**2. Salihina**

**Sifa zake**

***Ni mlanguzi wa dawa za kulevya***

- Alipanga na Bishoo mikakati ya usafirishaji na uuzaji wa dawa za kulevya.
- Alikuwa anatumia kinibu huku akicheza wimbo wa kidumbaki. ( UK 47)

***Mzunifu***

- Alitaka kuzini na Bishoo kabla ya kushtuliwa na msimulizi. (UK 47)

***Ni mfaniki***

- Anaitwa kwa jina la kidini-muadhamu, ilhali anafanya maovu ya kulangua dawa za kulevya na kuzini na Bishoo.
- Alimtandika msimulizi viboko kumi kwa mwiko wa kuku ( UK 43) kwa kosa la kusimama na msichana wa makamo pembeni, ilhali mwenyewe alizini na Bishoo.( UK 48)

***Ni mwadilifu***

- Inasemekana salihina alipata nafasi ya kuwa kiongozi wa mzimu kwa uadilifu wake mkubwa wa kuaminiwa kwake na wanakijiji. ( UK 43)

***Ni mtamaduni***

- Salihina alikuwa ndiye muandaaji mkuu wa shughuli za kimila kama vile matambiko na ugotozi wa jambo lolote litakalofanywa katika kijiji au kwa mwanakijiji. ( UK 43)

***Ni msiri***

- Tunaelezewa kuwa Salihina alikuwa na dhamana ya kutunza mzimu na ni yeye tu aliyejua siri ya mzimu ule. (UK 43)

***Ni mwoga***

- Aliposhtuliwa na msimulizi siku ile akiwa na Bishoo, alikimbia, japo kidogo tu kanzu lake jeupe la mafuta lilinasa kwenye mti na kumzuia asikimbie.

***Ni mwenye kujirudi***

- Baada ya kileo kile chenye fadhaa, huku akikimbia aliomba msamaha. Anasema, “ Nisamehe mwanangu nisitiri mwanangu.....” ( UK 48)

**Umuhimu wa Salihina**

- Ni kielelezo cha viongozi wanafiki wanaotumia nafasi zao visivyo.
- Kupitia kwake tunapata sifa za Bishoo kuwa ni mzinifu na mlanguzi wa dawa za kulevya
- Anaendeleza maudhui ya unafiki. Anakataza kuingia kwenye mzimu wa Kipwerere kuwa ni sehemu marufuku, kumbe anaitumia kufanya maovu

3. **Bishoo**

**Sifa zake**

***Ni mzinifu***

- Alitaka kuzini na Salihina kabla ya kushtuliwa na msimulizi. ( UK 47)

***Ni mwongo/ laghai***

- Alimdanganya mumewe kuwa alikuwa ameenda kwa jirani kumjulia hali mtoto wake alikuwa mgonjwa , kumbe alikuwa amekuja kumwona salihina katika mipango yake na salihina ya kusafirisha na kuuza dawa za kulevya, anasema kuwa wangechukua vyombo na kusema kuwa walikuwa wanaenda kumchotea maji shetani wa Mzimuni. Wakati huohuo kila ndoo wangeijaza mzigo badala ya maji na hapo hawangetiliwa shaka hata na polisi.

***Ni katili***

- Anamwacha mumewe ambaye mchana mzima alikuwa anaumwa na jino na kugaragara na kuja kufanya hila na Salihina.

***Ni mwoga***

- Waliposhtuliwa na msimulizi alianguka na kuzimia. ( UK 47)

**Umuhimu wa Bishoo**

- Ni kielelezo cha wanawake wasiokuwa waaminifu katika ndoa zao. Anataka kuzini na Salihina.

- Kupitia kwake tunapata sifa za Salihina kuwa ni mnafiki wanapopanga pamoja kuendeleza biashara ya ulanguzi wa dawa za kulevya huku wakidai kuwa dawa za kulevya zilikuwa marufuku pale kijijini.
- Anaendeleza maudhui ya ulanguzi wa dawa za kulevya

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

***Nyimbo***

- ★ Kuna wimbo wa kuingia kwenye mzimu wa kipwerere aliosikia msimulizi siku ile akidadisi jinsi ya kuingia mle. Ulikuwa wimbo wa sauti ya mwanaume ulioimbwa; 'mzimu wa kipwerere ugonywe wee! Mzimu wa kipwerere ugonywe, ugonywe koma na ndondi!'uliimbiwa upande wa pili wa ule mzimu na mwanamke kwa kusema; ' Ayee! Naugonywe wee! Mzimu wa Tate! Naugonywe , ugonywe koma na ndondi! ( UK 45)
- ★ Msimulizi aliimba wimbo ule wa ufunguo kuingia Mzimuni aliosikia ukiimbwa jana yake kabla ya kuingia kwenye mzimu wa kipwerere.
- ★ Salihina na Bishoo waliimba wimbo wa ufunguo wa kuingia kwenye ule mzimu wa kipwerere usiku ule waliposhtuliwa na msimulizi. (UK 46)
- ★ Kuna wimbo wa kidumbaki ; rhumba bila kulewa, utaichezaje rhumba aliocheza salihina huku akisogelea Bishoo siku ile walioshtuliwa na msimulizi. ( UK 47)

***Tashbihi***

- ★ Mzimu wa kipwerere ukitisha kama simba. ( UK 41)
- ★ Mwenye nguvu na mkali mithili ya simba jike anayenyosha watoto wake. ( UK 43)
- ★ Nikitandikwa viboko kumi kama mwizi wa kuku. ( UK 43)
- ★ Nilivaa guo jeupe lilonifunika gubugubi kama maiti. ( UK 45)
- ★ Matendegu marefu kama miguu ya punda kirongwe. (UK 46)
- ★ Yakawa kama masikio ya sungura anayeiba mazao shambani. ( UK 46)

- ★ Nikaangua Mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama. ( UK 47)

***Tabaini***

- ★ Si mchana si usiku. ( UK 41)

***Tahakuzi***

- ★ Iwe mbalamwezi au mchana. ( UK 41)
- ★ Kufa au kupona. ( UK 44)

***Nidaa***

- ★ Lazima uogope tu! ( UK 41)
- ★ Naam! ( UK 41)
- ★ Nyakati hizo. ( UK 42)
- ★ Na ajiandae kutolewa kafara! ( UK 42)
- ★ Kwamba shetani wa mzimu ana mke! ( UK 43)
- ★ Maadili na mila za wahenga! ( UK 43)
- ★ Lazima azma yangu itimize. ( UK 44)
- ★ Harusi ya kuthamini! ( UK 45)
- ★ Bishoo! ( UK 46)
- ★ Wanafiki wakubwa nyie! (UK 47)
- ★ Uchaji uliotukuka! (UK 48)

***Uhuishaji***

- ★ Woga ulioweza kukutia maradhi hata senene. ( UK 41) na
- ★ Nikajua hapa nikibaki nitayashughulisha masikio yangu bure kwa kusikiliza porojo zisizo na kichwa wala miguu. ( UK 48)

***Maswali balagha***

- ★ Kwa nini kitishe kiasi hicho? ( UK 41)
- ★ Ataacha kuogopa? ( UK 42)
- ★ Hawawezi hata kujenga nyumba ya miti na udongo ya kukaa? ( UK 44)

***Istiari***

- ★ Yaani kile kitendo cha kichaka kuitwa mzimu tu kilikuwa na homa ya jiji na shetani tosha.( UK 41)

***Misemo***

- ★ Lisemwalo lipo. (UK 42)
- ★ Porojo zisizo na mbele wala nyuma. ( UK 48)

***Nahau***

- ★ Kutolewa kafara. (UK 42)
- ★ Kukata kiu. ( UK 43)

***Takriri***

- ★ Tofautitofauti. ( UK 43)
- ★ Siku hadi siku.( UK 44)
- ★ Hatua kwa hatua. ( UK 44)
- ★ Ufunguo. ( UK 44)
- ★ Naugonywe. (UK 44- 45)

***Kinaya***

- ★ Ni kinaya kuwa mji wa watawa uliongoza kwa uingizaji , usambazaji na hata utumiaji wa vileo na dawa za kulevya ilihali mambo hayo yalikuwa yamepigwa marufuku.( UK 44)
- ★ Salihina anaiita kazi ya ulanguzi wa dawa za kulevya kuwa takatifu. Anasema" Basi kama ni hivyo, sawa. Nimefurahi wewe walete tu. Naamini watapenda kuifanya kazi hii takatifu kwa uadilifu mkubwa." ( UK 46) Hiki ni kinaya.
- ★ Ni kinaya kuwa Bishoo anamwita Salihina muadhamu, jina liitwalo kiongozi wa madhehebu, ilhali wanafanya biashara ya ulanguzi wa dawa za kulevya pamoja na uzinzi. ( UK 47)
- ★ Ni kinaya kwa salihina kumchapa msimulizi viboko kumi kama mwizi wa kuku, na wanajamii wengine walipata adhabu za aina hiyo kwa kila aliyevunja maadili na mila za wahenga, ilhali yeye mwenyewe anazini na Bishoo na vilevile kulangua dawa za kulevya.

**Taharuki**

- ★ Msomaji anaachwa na taharuki kuu ya kutamani kujua ipi ilikuwa hatima ya Bishoo baada ya kuanguka na kuzimia? Je , aliamka, alipatwa au alikufa kabisa?
- ★ Msomaji pia anataka kujua hatua alizochukua mumewe Bishoo baada ya kisa kile cha kudanganywa na mkewe kuwa alikuwa ameenda kuona mtoto wa jirani ambaye alikuwa mgonjwa na kumbe alikuwa amekuja huku kupatana na salihina.
- ★ Hatima ya salihina ni taharuki. Hatajui kama alijinasua kutoka kwenye mti uliomzuia au alipatwa na wanajamii? Na ikiwa alipatwa, hatua gani zilizochukuliwa? Je ? Aliendelea kuwa mzee kijijini na mdhamana mkuu wa mzimu au alivuliwa wadhifa huo?
- ★ Ni taharuki huku msomaji akitaka kujua hatua walizochukua wanakijiji baada ya kujua kuwa kumbe mzimu wa kipwerere waliokuwa wakiogopa na kuamini kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka! Kumbe ulikuwa uongo na sehemu ya kufanyia maovu ya uzinzi walivyofanya Salihina na Bishoo na kulangua dawa za kulevya. Walifanyaje baada ya kugundua hili na msimulizi alifanyiwa nini kutokana na hili.

## 6. KILA MCHEZEA WEMBE-*Pauline Kea*

### MTIRIRIKO

Mhusika Tembo ambaye ni mgonjwa katika hospitali ya Uhai ni Neema anamwandikia mke wake Emmi. Barua akimweleza yale yaliyomsibu baada ya yeye kuwa mraibu wa pombe.

Anamwomba Emmi msamaha na anajuta kwa yale aliyofanya. Anasema amekosa mbele ya Mungu, mbele ya Emmi na mbele ya ulimwengu. Anasema kuwa amefanya marafiki humo humo hospitalini. Rafiki wa kwanza ni muuguzi Nasir na mwingine ni mwathiriwa. Anasema kuwa dada zake na kaka walimtapika zamani. Alipokuwa anakanywa juu ya tabia yake, alijuta mapuuza.

Anakumbuka siku yake ya maangamizi alipoenda kwa mamapima na kisha baadaye kwenda ngomani kusaka rumba binti fulani alimjia ili wacheze. Anaendelea kusema " nilipoamka ilikuwa asubuhi yaelekea saa nne. Niliamshwa na sauti nyembamba ya kushawishi Mandhari ya hapo yalikuwa kijumba cha udongo, kimeezekwa kwa mabati mabovu kilango kina mianya ya kutosha kupitia ngamia. Pazia la mlangoni limechanika halitekelezi tena dhima yake. Yule waliyekuwa naye kitandani alikuwa adinasi wa kutisha.

Bi. Kizee huyo alimwagiza kulipa kwani hakukuwa na huduma za ubwete. Alipotoka hapo alitembea kwa miguu kutoka hapo majengo hadi kikutaruni. Anaendelea kusema kuwa anashikilia kuwa unyende aliopiga uliyanusuru maisha yake. Anasema " Nafikiri ulipogundua hali yangu ulijua nilihitaji dhamira ya matibabu".

Tembo anaendelea kumwomba Emmi aende amtoe kwenye lindi la majaribu, anamwomba ampe nafasi ya mwisho moyoni. Pia anamwambia awasalimie ndugu, wazee na wanao.

### ANWANI

- Katika hadithi ya 'Kila mchezea wembe' kuna wahusika ambao walichezea mambo ambayo si mazuri.

- Tembo alikuwa mraibu wa pombe ambaye hakusikiliza makanyo na maonyo aliyopewa na kaka na dada zake. Hata anakumbuka alizua zogo siku ya kusindikizwa kwa mpwa wake.
- Mke wa Tembo-Emmi alijaribu kumweleza kuwa pombe si chai ya kujinywea tu. Anamwambia akilewa ni matusi vipigo na anarudi akiwa amebebwa kwa machela.
- Salim mwathiriwa mwenzake naye yuko hospitalini.
- Alipolewa alijikuta kwenye chumba cha Bi . Kizee ambaye alimwagiza alipe kuwa hakuna huduma za ubwete.

**DHAMIRA**

- Mwandishi anadhamiria kueleza madhara yanayoletwa na uraibu wa pombe.
- Pia anatueleza umuhimu wa kuomba msamaha hasa unapogundua kuwa umekosa.

**MAUDHUI**

***Ulevi***

- Tembo alilewa kiasi cha kurudi nyumbani akiwa amebebwa kwa machela.
- Moshi alifia ulevini. Alianguka na kulala kingalingali huku viputoputo vya hewa vinamtoka kinywani.
- Mapipa ya mamapima ya changaa yalisheheni vituko. Si panya kuoza, nyoka wafu, si doda na nguo za ndani.

***Madhara ya pombe***

- Tembo yuko hospitalini na anatueleza kuwa hajapata kuona wala kubanduka kitandani kwa sababu ya pombe.
- Kutengwa na jamii, kaka na dada za tembo walimtapika kitambo. Pale hospitalini anajihisi mpweke kwa sababu amekosa mtu yeyote wa nasaha kuenda kumchungulia.
- Kutowajali familia, mkewe anamwambia , “ mwenzio kalenda ikishawadia sikuoni tena wajitapa una mke na watoto usiojua walacho wala wavaacho”.

- Uzinifu. Alipolewa tembo alijikuta kwa kitanda na bi. Kizee.
- Tembo aliibiwa pesa hata zile zilizokuwa kwa akaunti yake zilikuwa zimeibiwa.
- Kutumia pesa kwa mambo yasiyo ya kimsingi Bi. Kizee alimwambia " Hakuna huduma za ubwete kwa hivyo alihitaji kulipa".
- Tembo akilewa ni matusi na vipigo. Anarudi nyumbani akiwa amebebwa na machela

**Msamaha.**

- Tembo alimwambia mkewe kwa barua kuwa " nimekosa mbele ya Mungu , mbele yako emmi wangu na mbele ya uso wa ulimwengu.

**Mapuuza.**

- Tembo hakujali familia yake. Mkewe anasema " wajitapa una mke na watoto usiojua walacho wala wavaacho.

**Uzinzi**

- Tembo anapolewa anajipata nyumbani kwa Bi. Kizee ambaye anamwagiza kulipia huduma, Anasema " Hakuna huduma za ubwete hapa lipa usichonge viazi".

**WAHUSIKA**

1. **Tembo**

**Sifa zake**

***Ni mlevi***

- Analewa kiasi cha kurudi nyumbani akiwa amebebwa na machela.

***Ni Mwenye majuto***

- Anajutia yale yote aliyoyafanya na uraibu wa pombe na ndio maana anamwomba mkewe msamaha.

***Katili***

- Mkewe anasema," ukilewa ni matusi na vipigo". Kwa alimpiga na kumtusi mkewe alipokuwa amelewa.

***Mwenye mapuuza***

- Anajitapa ati ana mke na watoto ambao hujui walacho wala wavaacho.

**Umuhimu wa Tembo**

- Amechangia kukuza maudhui ya madhara ya uraibu wa pombe.
- Kupitia kwake tunapata kujua sifa za muuguzi Nasir kuwa ni mwenye utu.
- Tembo anawakilisha watu ambao wameathirika kiafya kama vile kupoteza macho kwa sababu ya uraibu wa pombe.

**2. Emmi ( mkewe Tembo)**

**Sifa zake**

***Mwenye kukata tamaa***

- Alimpeleka mumewe hospitalini na kumwacha huko. Tembo anasema," ningali palepale uliponiacha siku ile, yapata miezi miwili sasa.
- Anamwambia mumewe ampe talaka.

***Mshauri mwema***

- Anamshauri mumewe kuacha pombe, anamwambia kuwa pombe si chai ya kujinywea tu.

**Umuhimu wa Emmi**

- Ni kielelezo cha wanawake ambao wanapitia changamoto katika ndoa. Changamoto zinazoletwa na uraibu wa pombe.

3. **Bwana Salim**

**Sifa zake**

***Ni mlevi***

- Tembo anatueleza kuwa amefanya urafiki na mwathiriwa mwenzake anayeitwa salim.

***Mshauri mwema***

- Anamshauri Tembo kuwa kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa upishi. Anaendelea kumpa Tembo matumaini kuwa atapona.

***Mwenye utu***

- Tembo anasema Salim amemfaa kwa hili na lile na pia ndiye aliyeisalimisha hali yake na kama si yeye pengine angekuwa anaitwa mwendandazake.

4. **Muuguzi Nasir**

**Sifa zake**

***Mwenye utu***

- Tembo anasema kuwa Mungu amekirimia bwana Nasir moyo wa ajabu.

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

***Msemo***

- ★ Kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa upishi. ( UK 50)

***Tabaini***

- ★ Mapipa ya mamapima yalisheheni, si panya wa kuoza, si nyoka wafu, si doda na nguo za ndani.

***Tashbihi***

- ★ Jamaa wa Salim kufurika wodi kama mchwa kichuguuni wanavyokizingira kitanda chake. ( UK 51)

***Taswira***

- ★ Tunapewa maelezo ya yule Bi. Kizee . Alikuwa ghofu la mtu, mifupa yahesabika , mishipa ya damu imechungulia kwenye ngozi Chakavu iliyokunjana kama ya ndovu.
- ★ Mandhari ya hapo kwa Bi. Kizee yalikuwa kijumba cha udongo, kimeezekwa kwa mabati mabovu na kilango kina mianya.

***chuku***

- ★ Kilango cha nyumba ya Bi. Kizee kilikuwa na mianya ya kutosha kupitia ngamia.

***Maswali balagha***

- ★ Hakuna starehe nyingine uliyoona ila kunywa pombe?
- ★ Wazazi na wakwe zako pia uwape heshima?
- ★ Jamani mume wangu hivi wewe huwezi kurekebisha tabia zako?

***Kuchanganya ndimi***

- ★ Tear gas.( UK 53)
- ★ Sweetheart. ( UK 54)
- ★ I'M Angelica . (UK 54)
- ★ Maintenance. ( UK 55)
- ★ Thank you.( UK 55)
- ★ You are in safe hands. ( UK 55)

***Hadithi ndani ya hadithi***

- ★ Kisa cha Salim kuhusu mhudumu na mkufu wadhahabu . ( UK 56)

***Ushairi***

- ➢ Shairi la janga la kujitakia . ( UK 50)

**8. KIFO CHA SULUHU-Dominic Maina Oigo**

**MTIRIRIKO**

Ni kisa cha msichana Abigael, mwanafunzi wa chuo kikuu mwaka wa tatu kinachoanza kwa mazungumzo kati yake na Natasha rafiki yake wa muda mrefu sana. Wanazungumzia changamoto za kimaisha na kiuchumi. Changamoto hizi zinaonekana kuwaelekeza kwenye maovu ya kujiingiza kwenye mapenzi haramu na ya kiholela ili kujipatia pesa na riziki.

Katika mazungumzo ya wawili hawa, ndipo Natasha anapomshauri Abigael kutumia dawa anayompa, impe suluhu ( mpenzi wake haramu) usingizi, kisha amuibie na kisha kutoroka kwake. Walipania kuzitumia pesa hizo kujirembesha zaidi ili wavutie wanaume zaidi na hivyo kuboresha maisha yao.

Siku walipokutana suluhu na Abigael, Abigael alifanya alivyoambiwa na Natasha. Baada ya kuweka kidonge kile kwenye kinywaji na kunywesha suluhu, suluhu alilala fo fo fo. Abigael alitoa kisu kikali chenye makali kuwili kutoka kwenye mfuko mdogo alionunuliwa na suluhu ili kumwua suluhu. Kwenye pilkapilka za kutafuta pesa kabla ya kumwua, Abigael alipatana na barua ya Bi, suluhu kwa mumewe. Barua hii ilizungumzia adha na changamoto chungu nzima alizokuwa amepitia Bi. Suluhu kwenye ndoa yao.

Abigael alitokea kujua kuwa suluhu alikuwa mbunge na mwanzoni mchochole akifanya kazi ya kuuza makaa na mwenye mapenzi kwa mkewe na familia yake. Aliishia kubadilika. Barua iliendelea kueleza maovu ya suluhu kwa kuwa na vimada wengi alikopotezea pesa hata kutowajibikia familia yake. Abigael alishtushwa na kujua suluhu ndiye alimuua mamake kwa kuhofia kuchukuliwa hatua kwa kulinyakua shamba lake. Anatamatisha barua kwa kumwambia kuhusu mipango yake ya kujitia kitanzi kutoka adha hizo zote anazopitia.

Abigael alimaliza kusoma barua ile huku akibubujikwa na machozi. Sasa alipata kukitegua kitendawili cha kifo cha mamake aliyepatikana ameuawa na watu wasiojulikana. Abigael alighairi nia ya kumwua suluhu, akachukua mfuko na kisu chake akajiendea huku akifanya ahadi na moyo wake kuwa atafanya bidii kulihali , ajiandalie riziki yake na kumwachia Mungu wajibu wa hukumu.

**Dhamira**

- Mwandishi alikusudia kuelimisha dhidi ya kisasi na kuhukumu, kuwa ni kazi ya Mungu.
- Alikusudia kufunza athari za mapenzi ya kiholela na haramu kwa wanafunzi na walio kwenye ndoa.
- Mwandishi alikusudia kufichua maovu mengi ambayo hutekelezwa na viongozi.

**Ufaafu wa anwani**

- Hadithi nzima imejikita kwa mipango ya Abigael ya kutaka kumwangamiza suluhu baada ya kumtilia kidonge kwenye kinywaji. Abigael alikuwa ametoa kisu kwenye mfuko wake alionunuliwa na suluhu ili achukue pesa kwanza, kisha akapatana na barua iliyomghairisha nia yake ya mauaji.
- Hukumu ya Abigael kwa suluhu ya kutaka kumwua inaoneka kufa baada ya kuisoma ile barua iliyomfunulia mengi asiyotarajia . Anaishia kughairi hila ya mauaji na kuamua kufanya bidii kulihali, ajiandalie riziki yake na kumwachia Mungu wajibu wa hukumu.
- Kifo cha Bi suluhu, anachoonekana kapanga kufanya , kinaoneka kusababishwa na suluhu. Anaeleza adha zote alizompitishia na kusema kuwa. “Mume wangu wewe umeniua”.( UK 62)
- Bi suluhu anaona kifo chake huenda ni kifo cha suluhu, kumaanisha kitasuluhisha machungu na majuto aliyo nayo, au kitamtia Suluhu furaha kwa yeye mkewe kumwondokea. Anasema... “Mume wangu, wewe umeniua na iwapo kifo changu kitakuwa kifo cha suluhu, basi silalamiki.” ( UK 62)

**MAUDHUI**

***Ndoa na changamoto zake***

- Bi. Suluhu anapitia changamoto chungu nzima kwenye ndoa yake na suluhu. Analalamikia suluhu kuwatenga, kulala nje, kumwachia jukumu lake pekee kuwalea wanao, kuwa na vimada wengi nje ya ndoa, kutofaa kifedha. Anasema maudhi haya yamesababishia kukesha na kujuta kuolewa naye na hata kutaka kujitia kitanzi. Huku

Abigael akimnywesha Suluhu kile kinywaji, Suluhu alianza kusutwa kwenye nafsi yake kwa nini alioa kijanajike ambacho hakikujua namna ya kumpenda. Akawa anafikiri namna ya kumshawishi Abigael awe mkewe wa kando na mara akawazia jinsi ya kumwangamiza mke wake. Hii inadhihirisha changamoto ambazo wawili hawa walihisi kwenye ndoa yao.

***Mapenzi***

- Abigael na Natasha walipendana sana na hata kuishi kwenye chumba kimoja pale shuleni ili kupunguza gharama ya maisha. Rafiki hawa waliaminiana na kushauriana, kupeana tumaini na kushirikiana kupunguza upweke. ( UK 59)
- Abigael na suluhu ni wapenzi. Mapenzi yao ni ya njia panda maana Abigael anatumia penzi la Suluhu ili kupata pesa awe mtu. Vilevile Natasha anaona kama suluhu anatumia Abigael kama chombo cha kujifurahisha ( UK 59). Hali hii ya penzi la kinafiki inaishia kumfanya Abigael na Natasha kupanga kumtilia Suluhu kidonge kwenye kinywaji ili Abigael ajipatie pesa za kujiboresha zaidi ili wawavutie wanaume zaidi wa kuwaboreshea maisha. Mpango huu unakosa kutimia Abigael anapopata barua ya mkewe Suluhu, Bi. suluhu kwenye mfuko akitaka kumwibia pesa kabla ya kumwua.
- Suluhu anaonekana kumpenda Abigael kwa dhati. Msimulizi anasema "Huku suluhu akinyweshwa kinywaji, akili yake ilizidi kumsuta kwa kuoa kijanajike ambacho hakikujua kumpenda. Akawaza jinsi ya kumshawishi Abigael awe mkewe wa kando. Anaendelea kusema "Alifikiri na kufikiri . Anatamani kila siku awe na Abigael ili azidi kufurahia mahaba yake. Suluhu alikuwa tayari kufanya lolote ili kudumisha uhusiano huu." (UK 69)
- Bi suluhu anaonekana kumpenda mumewe licha ya mabaya anayomfanyia. Anatamatisha barua kwa kumwita ; " wako wa milele" ( UK 62) . Anamwambia kuwa alimpenda sana tangu siku ile siku alipomtaka awe mke wake, muda wote huo waliokuwa pamoja, hakumwendea kinyume, hakumsaliti wala kutaka kulipiza kisasi chochote.

- Suluhu alimpenda mkewe kwa dhati mwanzoni. Bi suluhu anasema kwenye barua kuwa anamshukuru kwa mema yote aliyowahi kumtendea kabla ya kugeuka na kuwa mumunye, alivyoipenda yao mwanzoni.
- Suluhu anaonekana kubadilika na kughairi ahadi alizopeana kwa mke wake mwanzo ndoani. Anaishia kumtelekeza na kujitenga mbali naye na hata kutelekeza majukumu yake ya ndoa kama kulea watoto. Alipokuwa akinyweshwa kinywaji na Abigael, msimulizi anasema kuwa akili yake ilizidi kumsuta kwa kuwa kijanajike ambacho hakikujua namna ya kumpenda. Akawa anafikiria namna ya kumshawishi Abigael awe mkewe na kando na hayo akiwazia jinsi ya kumwangamiza mkewe" ( UK 60. Hii inaonyesha penzi la kinafiki alilokuwa nalo Suluhu kwa mkewe.

***Ukatili/ mauti/ mauaji***

- Abigael na Natasha wanapanga njama za kikatili za kumwua Suluhu kwa kumtilia kidonge kwenye kinywaji. Abigael anakaribia kutekeleza hili janga. Anasitishwa na barua ya kushtua anayopata kwenye mfuko wa suluhu.
- Suluhu ana njama mbaya ya kumwangamiza mke wake. Msimulizi anasema; "Akawa anafikiria namna ya kumshawishi Abigael awe mkewe wa kando na mara akiwazia jinsi ya kumwangamiza mke wake." ( UK 60).
- Suluhu alimwua mamake Abigael kutokana na wasiwasi ikiwa angechukua hatua za kisheria kwa kulinyakua shamba lake ( UK 61).
- Bi. Suluhu anawazia kujitia kitanzi kutokana na adha nyingi alizosababishiwa na Suluhu anasema kwenye barua kuwa. " Mume wangu, wewe umeniua na iwapo kifo changu kitakuwa kifo cha suluhu, basi silalamiki" ( UK 62)

## WAHUSIKA

### 1. Natasha

Ni rafiki wa dhati wa Abigael. Wanasoma pamoja kwenye chuo kikuu.

**Sifa zake**

***Ni mwenye mapenzi***

- Alimpenda Abigael kwa dhati na kuwa naye katika hali zote.

***Ni mshauri mbaya***

- Alimshauri Abigael kumtilia dawa kwenye kinywaji na kumwibia Suluhu.

***Ni msomi***

- Alikuwa anasoma na Abigael kwenye chuo kikuu. Waliishi pamoja. Natasha alikuwa amesoma pale kwa zaidi ya miaka saba.

***Ni mvumilivu***

- Alivumilia akiendeleza masomo kwa kipindi kirefu. Msimulizi anasema kuwa alijua amesoma pale kwa zaidi ya miaka saba na hakuelekea kuhitimu (UK 58)

**Umuhimu wa Natasha**

- Ni kielelezo cha marafiki ambao hupeana ushauri wa kupotosha wenzao.

2. **Abigael**

Ni mpenzi wa kando wa suluhu. Ni mwanafunzi chuoni na rafiki wa dhati wa Natasha.

**Sifa zake**

***Ni msomi***

- Alisomea katika chuo pamoja na Natasha.

***Ni mwenye kujali /kuwajibika***

- Alitegemewa na babake kwa kila kitu. Vile vile alitegemewa na wanuna wake kwa karo. Hii inaonyesha kuwajibika kwake katika hali hii.

***Ni mzinzi/ mkware***

- Alizini na suluhu kwa manufaa ya hela.

***Ni katili***

- Alipanga njama ya kumwua Suluhu ili kumwibia pesa.

***Ni mwenye kujirudi***

- Baada ya kusoma barua ya bi. suluhu, anajirudi na kughairi nia ya kumwangamiza. Msimulizi anasema; "Moyoni alifanya ahadi na nafsi yake; atafanya bidii kulihali ajiandalie riziki yake na kumwachia Mungu wajibu wa hukumu."( uk 63)

***Ni mwenye mapenzi***

- Alimwonyesha Suluhu mapenzi ; " Alimnywesha kinywaji kama mtoto mdogo.
- Alitamani kila siku awe na Abigael ili azidi kufurahia mahaba yake. ( UK 60)

**Umuhimu wa Abigael**

- Ni kielelezo cha wanafunzi katili ambao hupanga njama za mauaji
- Anaendeleza maudhui ya elimu. Anasoma na Natasha katika chuo kikuu
- Kupitia kwake tunapata sifa za Suluhu kuwa ni mkware. Alizini na Abigael na vilevile alikuwa na vimada wengine tunavyoelezwa kwenye barua ya bi. Suluhu.

### 3. Suluhu

Ni mume wa Bi. Suluhu na mpenzi wa kando wa Abigael.

**Sifa zake**

***Ni mzinzi/ mkware***

- Alizini na Abigael licha ya kwamba alikuwa na mke

***Ni katili***

- Alimwua mamake Abigael kwa kuhofia kumchukulia hatua za kisheria baada ya kulinyakua shamba lake.
- Alikuwa anafikiria namna ya kumshawishi Abigael kuwa mke wake wa kando na mara akiwazia jinsi ya kumwangamiza mke wake. ( UK 60)
- Alitelekeza mkewe na wanawe bila usaidizi wowote ilhali alikuwa na uwezo wa kifedha wa kufanya hivyo.

***Ni mkarimu***

- Alimnunulia Abigael mfuko. ( UK 69)
- Alimsaidia mamake mkewe alipokuwa mgonjwa. ( UK 62)

***Ni mwenye matapo***

- Alisifia saa yake ya dhahabu kila wakati. ( UK 59)

***Ni mwenye mapenzi***

- Alimpenda Abigael kwa dhati kiasi cha kufikiria kumshawishi Abigael awe mkewe wa kando.( UK 60)
- Bi. Suluhu anamweleza kupitia kwa barua kuwa alimshukuru alivyoipenda familia yake kabla ya kwenda segemnege.

***Ni fisadi***

- Alitumia pesa za wananchi kwa kuwalipa wasichana wa vyuo baada ya kula uroda nao. Alipanga binti chuoni ahitimu kabla ya muda wake kufika. ( UK 61)

***Mkware***

- Alikuwa akiwalipa wasichana wa vyuo vikuu baada ya kula uroda nao.

- Alikuwa na Hawara mwingine aliyeishi kumpangia chumba kule mjini.
- Alikuwa na mahusiano na Abigael licha ya kuwa alikuwa na mke

**Umuhimu wa Suluhu**

- Anaendeleza maudhui ya ukatili. Alimuua mamake Abigael
- Kupitia kwake tunapata sifa za bi. Suluhu kuwa ni mvumilivu. Alivumilia mateso kwenye ndoa
- Anawakilisha wanaume ambao si waaminifu katika ndoa zao

4. **Bi.suluhu**

Ni mkewe suluhu

**Sifa zake**

***Ni mvumilivu***

- Alivumilia adha zote alizofanyia na suluhu. Anasema kwenye barua yake; "Nimevumilia kwa miaka mingi kwa ajili ya wanetu. Nimevumilia madhila yako kwa muda mrefu..."( UK 61)

***Ni msiri***

- Hakufichua siri ya mauaji ya mamake Abigael kwa askari.
- Anaahidi kufukiwa na siri zote za suluhu azijuazo licha ya Suluhu kumkosea.

***Ni mwenye kuwajibika***

- Alijibidiisha kuwalea wanao bila msaada wa mumewe suluhu.

***Ni mwenye mapenzi***

- Alimpenda mumewe kwa dhati kiasi cha kutotaka kumtia mashakani, wala kufichua siri zake.

***Ni mshauri mwema***

- Anamuasa mumewe kubadilika na kujutia mabaya aliyoyafanya. Anasema....! “Nitaendelea kukuasa. Sitachoka kukuasa ikiwa ni Mfano wa kumchezea mbuzi gambusi.” ( UK 62)

**Umuhimu wa Bi.Suluhu**

- Ni kielelezo cha wanawake ambao huvumilia kwenye ndoa zao licha ya changamoto nyingi wanazopitia
- Kupitia kwake tunapata sifa za Suluhu kuwa ni katili. Alimtesa Bi. Suluhu na kumuua mamake Abigael
- Anaendeleza maudhui ya uwajibikaji. Analea wanawe bila usaidizi wa Suluhu.

## MBINU NA MATUMIZI YA LUGHA

**Nahau**

- ★ Kuwa kupe. ( UK 58)
- ★ Kujitia kitanzi. ( UK 61)
- ★ Gonga mwamba. ( UK 58)

**Uhuishaji/Tashhisi**

- ★ Wakapigwa na upepo wa maisha. ( UK 58)
- ★ Wakatapikwa na dunia yenyewe bila Simoli. ( UK 58)
- ★ Moyo ulimpapa na woga ukamvamia. ( UK 60)
- ★ ...... Ni ishara ya penzi letu ambalo linaanza kuchipuza. ( UK 60)
- ★ Mara alichomoa kibeti kilichokuwa kimefura na kushiba. ( UK 60)
- ★ Kisu chake kilimkodolea macho.( UK 60)
- ★ Kile kisu kilikuwa palepale juu ya kitanda kikiendelea kumkejeli na kumcheka Abigael. ( UK 63)

**Takriri**

- ★ Hivihivi. ( UK 58)
- ★ Yaleyale. ( UK 59)
- ★ Haraka haraka. ( UK 60)
- ★ Alifikiri na kufikiri. ( UK 60)
- ★ Palepale. ( UK 63)

**Tabaini**

- ★ Si kwamba yeye alikuwa amechagua azaliwe katika aila isiyo na kitu.
- ★ Si kwamba yeye hakutamani kuishi mama mabinti wengine. ( UK 58)
- ★ Si kule kujaribu tu kwa njia ya maombi. ( UK 58)

**Maswali balagha**

- ★ .... kumwondolea ukungu njiani ? ( UK 68)
- ★ Umesahau mume wangu? ( UK 61)

- .....serikali kupiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la Dafrau?. ( UK 61)
- .....ulivyoisha kumtunga mimba na kumwacha bila tumaini? ( UK 61)
- Umesahau kilichokuleta humu?. ( UK 60)

**Misemo**

- Kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake
- Kitumbua kimeingi mchanga. ( UK 61)
- Kumchezea mbuzi gambusi.( UK 62)
- Kutia msumari kwenye kidonda. ( UK 63)
- Mambo kwenda segemnege.( UK 62)

**Methali**

- Jitihada ikababakia kuondoa kudura. ( UK 58)
- Amlaye nguruwe huchagua aliyenona. ( UK 59)
- Yaliyopita si ndwele. ( UK 60)
- Ukitaka kumwua nyani , usimtazame usoni. ( UK 59)

**Taharuk**i

- Msomaji anabaki na shauku ya kujua alivyoovaa suluhu. Msimulizi anasema ; "Baada ya suluhu kumaliza kuvua vya kuvuliwa " ( UK 59)
- Ni taharuki kwa msomaji Bi.suluhu kupitia kwa barua yake kwa suluhu anaposema; " ama cheo chako cha ubunge ulichokipa kwa njia nizijuazo mimi...( UK 61) Msomaji anataka kujua mbinu hizi ni zipi?
- Vilevile msomaji anabaki na shauku ya kujua hatima ya Suluhu baada ya kunyweshwa dawa. Je ? Aliamka? Na alipogundua nia ya Abigael, alichukua hatua gani.
- Ni taharuki kwa msomaji anapotaka kujua hatima ya Bi. Suluhu . Je? Alijitia kitanzi au aliendelea kuishi ? Wanao je? Nani aliendelea kuwakimu?.
- Msomaji ana hamu ya kujua hatima ya Abigael . Je? Alibadilika na kuwacha kuzini na suluhu? Na kama waliachana, aliendeleaje kujikimu kuimarisha na kuwasadia babake na wanuna wake?

- ★ Ni taharuki kwa hatua ambayo Abigael alichukua baada ya kujua kuwa suluhu ndiye aliua mamake. Je alimshtaki au la?
- ★ Msomaji anatamani kujua hatua aliyochukua suluhu baada ya kusoma ile barua ya mkewe. Kama alibadilika na kuwa mume mzuri au aliendeleza zile tabia zake chafu alizokuwa akilalamikia mkewe.

**Tashbihi**

- ★ ......akaanza kumnywesha kinywaji kama mtoto mdogo .( UK 60)
- ★ Kulitupa penzi langu kama jogoo na mti wake. ( UK 60)
- ★ Umejibaidi kama ardhi na mbingu. ( UK 61)

**Nidaa**

- ★ La !( UK 58)
- ★ Unajua la kufanya ! ( UK 60)
- ★ Henda umesahau! (UK 60)
- ★ Labda hujui ! ( UK 60)
- ★ Narudia sitawaambua !( UK 61)
- ★ Nitafikiwa na siri zote nizijuazo !

**Sadfa**

- ★ Ni sadfa kuwa suluhu akiwazia kumwangamiza mkewe kwenye fikra zake siku ile akinyweshwa kinywaji na Abigael, kumbe hapohapo Abigael alikuwa amemtilia dawa kwenye kinywaji hicho na alikuwa na kisu chenye makali kuwili alichopania kutumia kumwangamiza nacho suluhu. ( UK 60)

**9. AHADI NI DENI-*Rayya Timammy***

**MTIRIRIKO**

Fadhumo alikuwa na furaha tele siku ile Kwani alikuwa amepata barua. Barua iliyokuwa imemwita katika shule zinazohesabiwa kuwa ndizo nzuri zaidi katika kaunti yao. Siku ilipofika walisafiri hadi mjini ijapokuwa baba ni maskini alimtimizia mahitaji yake yote. Kabla kuachana, Fadhumo alimwahidi babake kuwa atasoma kwa bidii.

Maagano yalikuwa kwamba haturudi nyumbani mpaka mwisho wa mwaka. Hata kabla ya kufunga shule habari zilikuja kuwa babake amefariki kutokana na ajali mbaya barabarani . Likizo ilipoisha alirudi kuanza kidato cha pili. Hata huo mwaka haukufika nusu alipata tena habari mbaya. Maskini sasa alikuwa kiate . Huu ndio ulikuwa mwanzo wa visa na matatizo yake Fadhumo. Alipoanza muhula wa tatu aliachishwa shule katikati kwani alikuwa hana karo. Maskini alikuwa ndiye kifungua mimba wa kike, hivyo ilibidi atoke shule arudi awe mlezi wa nduguze.

Fadhumo alikubali kuolewa kwa sababu yule bwana alikubali atamsomesha nduguye wa kiume amalize na akaahidi pia wale wengine watatu wa kike watasaidiwa .Miaka tatu ilipita kama upepo na baada ya miaka sita na kujifungua watoto watatu ari yake ya kusoma ilirudi. Aliweza kusoma akamaliza kidato cha nne halafu baadaye akajiunga na koleji ya kufunza namna ya kufundisha watoto wadogo. Baada ya hapo akataka kusoma stashahada.

Mumewe alipata wengi waliomtia maneno. Mjomba wake Adan ( mumewe Fadhumo) alimweleza Adan kuwa mwanamke hapaswi kusoma maana atakuja kukukimbia kabisa. Adan alimsikiliza tu lakini alijua hawezi kumkataza mkewe kusoma. Alijua mkewe hakuwa na nia mbaya naye na aliamua yuko tayari kusimama na mkewe popote na hata ikibidi kumsafirisha bora akate ile kiu yake ya elimu.

**DHAMIRA**

- Kuonyesha vile elimu ni muhimu kwa watoto wote wawe wa kike au wa kiume.
- Kuonyesha vile taasubi ya kiume inavyoweza kumkandamiza mwanamke. Kwa mfano mjombake Adan hakutaka Adan kusomeshwa.
- Lengo kuu la mwandishi ni kueleza watu kujua umuhimu wa kuweka ahadi. Fadhumo alimwahidi babake kuwa atasoma na ndio maana aliamua kurudi shuleni.
- Mwandishi pia anaeleza kuwa ni vizuri kuweka ahadi .Adan alimwahidi mukewe kuwa atasoma na hakutaka kuvunja ahadi.

**ANWANI.**

- Fadhumo alimwahidi baba kuwa angesoma kwa bidii. "Ninajua baba nitasoma sana, ninajua huna pesa lakini umejaribu sana kulipa karo na mahitaji mengine.(uk64)
- Alipotokea mume aliyetaka kumwoa Fadhumo alikubali kwa sababu ya ahadi aliyompa bwana yule maana alikubali atamsomesha nduguye wa kiume amalize na akaahidi pia wale wengine watatu wa kike watasaidiwa (uk 66)
- Adan alikuwa amemwahidi mkewe kuwa atasimama naye popote na hata ikibidi kumsafirisha bora aikate ile kiu yake ya elimu ndio maana hakuyatilia Maana yale aliyokuwa anaambiwa na mjomba wake.

**MAUDHUI.**

**ELIMU.**

- Fadhumo alikuwa na furaha tele siku ile kwani alikuwa amepata barau iliyokuwa imemwita katika shule moja kati ya zile shule zinazohesabiwa kuwa ndio nzuri zaidi katika kaunti yao (uk64)
- Baada ya kuolewa na kukatisha masomo yake Fadhumo alirejelea masomo yake na alipata walimu wa kumfunza nyumbani (uk67) Alidurusu na alipofanya mtihani alipata alama ya C-.

**KAZI.**

- Bw.Khalif alifanya Kazi ya udereva wa serikali (uk 64)
- Baada ya kufuzu na kupata astashahada Fadhimo alipata kibarua na akawa anasomesha watoto wadogo (uk67).

**UMASKINI.**

- Fadhumo alikubaliana na babake kuwa hatorudi nyumbani mpaka mwisho wa mwaka kwa vile pesa za kulipa nauli ya kwenda na kurudi kila muhula hazikuwepo(uk 64)
- Fadhumo aliachia shule katika Kidato cha tatu kwani alikuwa hana karo baada ya wazazi wake kufariki hakuwa na yeyote wa kumsaidia.

**MAUTI.**

- Babake Fadhumo alifariki kutokana na ajali mbaya ya barabarani (uk 65)
- Mamake Fadhumo pia aliaga dunia (uk 65).

**NAFASI YA MWANAMKE KATIKA JAMII**

- Mwanamke anastahili kukaa nyumbani kutunza nyumba na watoto na kumtizama mume bali si kwenda kazini.
- Mwanamke akisoma atakuja kumtoroka mumewe mjombake Adan anasema "yapi haya nasikia mkeo anasoma?Akasoma,atasoma mpaka wapi, atakuja kukumkimbia atakuwa jeuri.(uk 68). Hii ndio imani ya jamii hii kuhusu mwanamke.

**UKATILI.**

- Fadhumo alipata jamaa ya babake ambaye alikuwa tayari kumsaidia kulipa karo lakini kwa masharti Bwana huyo alimwambia angemtimizia mahitaji yake yote ila shule zikifungwa aende aishi naye kama kimada wake (uk66)

**WAHUSIKA.**

**FADHUMO.**

***1.Mwenye bidii.***

- Fadhumo alikuwa mwenye bidii masomoni ndio maana aliitwa shule moja Kati ya zile zinazohesabiwa kuwa ndizo nzuri zaidi katika kaunti yao (uk 64)
- Mwalimu mkuu anasema wasichana wote wangalikuwa kama Fadhumo kwa bidii na utafiti shule yake ingefanya vyema sana (uk 65)
- Adan mumewe Fadhumo anasema kuwa hajaona mwanamke mwenye bidii kama Fadhumo. Alifanya ulezi na uzito wote wa ndoa uonekane kanda la usufi(uk 67).

  ***2.Mwenye mapenzi dhati.***

- Aliwapenda ndugu zake na ndio maana alikubali kuolewa na Adan kwa sababu alikubali atawasomesha nduguye wa kiume na wengine watatu wa kike atawasaidia.

**Umuhimu wa Fadhumo**

- Kupitia kwake tunapata sifa za Adan kuwa ni mwenye mapenzi ya dhati. Alimpenda mkewe sana
- Anaendeleza maudhui ya elimu. Alirudi shuleni hata baada ya kuolewa
- Ni kielelezo cha wanawake wenye bidii katika ndoa zao.

**2.Adan**

***1.Mwenye mapenzi ya dhati***

- Alimpenda sana mkewe Fadhumo ndio maana hakuyaamini Maneno mengi aliyopewa na watu (uk 67)
- Adan alimtazama mjombake kwa huruma na kuondoka hapo lake Li moyoni (uk 68).

2.***Mwenye busara.***

- Hakufuata ushauri mbaya wa mjomba wake

**3.MJOMBAKE ADAN.**

***1.Ana taasubi.***

- Anatahadharisha Adan kwamba akiendelea kumwacha mkewe kwenda kazini na kusoma atamkimbia na kuwa jeuri (uk 68). Pia anamuuliza "kwani nani anayevaa suruali katika nyumba ile"

***2.Ni mkarimu***

- Alimlea na kumfikisha Adan alipo baada ya babake kufariki (uk 68)

**4.BABAKE FADHUMO.**

**1.*Mwenye bidii***

- Alifanya Kazi ya udereva wa serikali

- Hakutaka wanawe waishi maisha ya kijungu Jiko kama alivyoishi kwa hivyo alifanya bidii kuyakimu mahitaji yao (uk 64)

***2.Mwenye matumaini.***

Alikuwa na matumaini mengi sana kwa watoto wake ndio maana alijitahidi kulipa karo na mahitaji yake (uk 64).

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Tashbihi.**

- Maneno hayo yalikuwa kama hirizi aliyoamua kuivaa ili yamwongoze (uk 65).
- Mawazo yalikuwa yanayompitia akilini mzomzo kama picha katika kioo cha runinga (uk 65)
- Fadhumo alimtazama machoni mwake, alionekana kama mtoto mdogo aliyekuwa akimtazama mamake(uk 66)
- Macho yake yalikuwa yanang'aa kama ya mtoto aliyepewa peremende (uk 67)

**TASHIHISI.**

- Fadhumo roho ilimruka (uk 65)

**METHALI.**

- Uzito wote wa ndoa unaonekana kanda la usufi (uk 67)
- Asojua Maana haambiwi Maana (uk 68)
- Ahadi ni deni (uk 64

**MSEMO.**

- Ikawa ndiyo mwanzo mkoko unaalika maua (uk 67)

**UTOHOZI.**

- Koleji (uk 67)

**10. TOBA LA KALIA-*Douglas Ogutu***

**MTIRIRIKO**

Hadithi hii inaanza huku jack akipokea simu ya Siri. Simu ya Siri ilikuwa ya kuwaarifu jack, Kalia na mamake siri- Bi. Mshewa ambaye alikuwa mwalimu wa kiswahili katika shule ya upili waliosomea jack na siri, kuwa walifaa kuhudhuria mahojiano na kituo cha runinga ya kikwetu. Hawakujua walichokuwa wanafaa kuzungumzia siku hiyo, ilikuwa ni siri ya Siri.

Siku ya mahojiano, wote watatu – Kalia, Bi mshewa na jack walihudhuria. Mtangazaji, na mwelekezi wa kipindi alikuwa Jane Hatibu. Baada ya makaribisho, salamu na utangulizi wa kipindi ilikuwa zamu ya siri kuzungumza.

Ni katika mahojiano haya ambayo Siri alipasua mbarika na kutoboa siri kuu iliyomwelekeza kuwa Uchina aliko sasa. Alisema kuwa kulikuwa na mashindano ya somo la sayansi miongoni mwa shule za upili katika kaunti yao. Mshindi angepata ufadhili wa masomo kuanzia shahada ya kwanza hadi shahada ya uzamifu katika chuo kikuu cha uhandisi. Wadhamini wa tuzo hiyo walikuwa wataalamu wa uhandisi kutoka Uchina.

Ni katika shindano hili ambapo Jack alinyang’anywa ushindi wake wa alama tisini na saba na kupewa siri. Jane kambo, nafasi yake ya pili ilibaki hivyo hivyo na nafasi ya tatu ya siri ya alama tisini kupewa jack. Uhaini huu ulipangwa na kuratibiwa na bwana Kalia, babake siri ambaye alikuwa mmoja wa wanakamati katika wizara ya sayansi na teknolojia. Alibatili matokeo haya.

Hali hii ilimtia Siri katika hali ya kujihukumu na akaamua kuungama mbele ya ulimwengu kupitia runinga ya kikwetu. Ilishangaza wengi, wakiwemo wazazi wake, nao pia wakalazimika kuungama pia. Mamake aliungama kwa kuchukua pesa alizotuzwa Jack- hangepewa kwa sababu alikuwa yatima, kisha kuzitumia kuanzisha biashara ya viatu. Babake aliungama kwa kubatili matokeo ya tuzo na ufadhili wa jack na akaahidi kumsomesha baada ya hapo. Watatu hawa walirudi nyumbani huku wana furaha na huru na huku wakizungumzia baadhi ya vyuo ambayo Jack angeweza kusomea.

## DHAMIRA

- Mwandishi alidhamiria kumulika ufisadi na udanganyifu unaofanywa katika nyanja za kishindani kama tuzo, haswa ubatilishaji wa matokeo.
- Ilikuwa dhamira yake pia kueleza madhila wanayopitia yatima kama vile kubadilishiwa ushindi na kunyanyaswa kifedha kwa vile hawana namna ya kupigania haki.
- Mwandishi alinuia kuelimisha namna toba ni muhimu kwa wanajamii waliokuwa na kinyongo dhidi ya wenzao na furaha na uhuru wanaoishia kuwa nao baada ya kusamehewa.

## ANWANI

- Siri bin Kalia anaomba toba kwa jack mbele ya ulimwengu mzima kupitia runinga ya kikwetu. ( UK 74)
- Kalia, babake siri na mumewe naye hakusita kuomba msamaha kwenye runinga ya kikwetu. Vilevile alimtaka siri kutojisumbua na kumsomesha Jack, maana yeye mwenyewe angeshughulikia suala hilo.
- Bi. Mshewa anamwomba msamaha Jack kwa kuitisha nusu ya faida Kila mwezi. Toba hii anaiomba kwa niaba yake ili wanake ( familia ya Kalia) wasipate laana.

## MAUDHUI

### *Ukatili*

- Kalia anafanya ukatili kwa kubatilisha ushindi wa Jack katika shindano la masomo ya sayansi. Hii inasababisha Jack kukosa ufadhili wa masomo ya shahada ya kwanza hadi ya uzamilifu katika chuo kikuu cha uhandisi kutoka Uchina. Kalia alifanya haya kwa ushawishi aliokuwa nao kama mmoja wa wanakamati katika wizara ya sayansi na teknolojia.
- Bi mshewa alikabidhiwa zawadi ya Jack katika shindano la masomo ya sayansi. Alitumia pesa hizi kumwanzishia biashara ya kuuza viatu na kisha kutaka kupewa nusu ya faida kwa pesa zake za ushindi. Huu ni ukatili.

- Wazazi wa siri wanafanya ukatili kubatilisha ushindi wa Jack na kuishia kukosa nafasi ya kuyaendeleza masomo yake, ilhali wao walikuwa na uwezo wa kumsomesha siri hata bila ufadhili wowote ule. ( UK 73)
- Ni ukatili kwa familia ya Kalia kuweka siri hii mbaya ya ubadilishaji wa nyota ya Jack kwa miaka mingi hadi siku hii siri alipoamua kupasua mbarika.

***Adha/ changamoto wanazopitia mayatima***

- Jack anabadilishiwa ushindi wake wa shindano la masomo ya sayansi kwa sababu ni mnyonge na hakuwa na uwezo wa kutetea haki zake kama yatima
- Bi. Mshewa anamdhulumu Jack kwa kumwanzishia biashara na pesa zake za ushindi wa shindano la masomo ya sayansi na tena kumwitisha nusu ya faida kila mwezi, mara anapoona biashara hiyo imeanza kunawiri. Jack hakuwa na budi ila kutii maana hali yake ya uyatima haikuruhusu kuwa na nguvu za kupigania haki zake.
- Jack anakosa namna ya kuendeleza masomo yake kwa ukosefu wa pesa. Hii ni kwa sababu alikuwa yatima na hivyo wazazi wa kumshughulikia majukumu haya hawakuwepo.

***Toba***

- Siri bin Kalia aliomba toba kwa Jack mbele ya ulimwengu kupitia runinga ya kikwetu. Hili alipanga kufanya kisiri bila ufahamu wa wazazi wake na hata jack. Anapendekeza kumsomesha Jack, jambo ambalo babake Kalia anaahidi kulishughulikia .
- Babake Siri anaomba msamaha kwa Jack kwa kubadilisha uongozi wake halali kwenye shindano la masomo ya sayansi.
- Bi. Mshewa, mamake Siri anamwomba Jack msamaha kwa kuona tamaa Jack alipoanza kuimarika katika biashara yake na kuishia kumwitisha nusu ya faida ya kila mwezi. Hili anafanya ili kuepuka laana kwa wanawe. ( UK 74)
- Kalia anaomba toba kwa Jack kwa kushiriki ubadilishaji wa ushindi wake katika shindano la masomo ya sayansi. Anaongezea kuwa atashughulikia kumsomesha Jack zaidi.

- Jack anakubali toba ya siri, Kalia na Bi. Mshewa. Anasema kuwa hana ngoa nao. Anaendelea kuwashukuru kwa kumruhusu kufanya biashara. Anafurahi sana na kushabikia suala la yeye kupewa nafasi ya kuendeleza masomo yake. Furaha inaoneka kutanda kati ya Kalia, Bi. Mshewa na Jack huku wakirudi nyumbani baada ya kufanya toba na Jack. Wote hawa walihisi furaha na huru baada ya toba hii. wanazungumzia vyuo ambavyo Jack angependa kusomea, huku wakiwa njiani.

***Elimu***

- Jack na siri walikuwa marafiki wa miaka mingi. Vilevile walikuwa marika na walisoma shule moja ya msingi na vilevile sekondari. ( UK 69)
- Jack na Siri wanaonekana kuwa wanafunzi wa bidii na ubunifu mkubwa wanapoibuka wa kwanza na wa tatu katika shindano la masomo ya sayansi. Katika wawasilishaji ishirini bora, Jack na siri waliibuka miongoni mwa watano bora.
- Mamake siri, Bi. Mshewa anaoneka kufurahia ufasaha anaozungumza kiswahili Jane Hatibu kila mara alikuwa akitabasamu na kutingisha kichwa.
- Vilevile Bi. Mshewa alifundisha kiswahili katika shule ya upili waliosomea siri na Jack.
- Kalia alikuwa msomi, ndio maana alikuwa mmoja wa wanakamati katika wizara ya sayansi na teknologia. Wakati huu wa tuzo ya masomo ya sayansi alikuwa wiki nzima akishughulika na mipango ya kufanikisha hafla hiyo.
- Siri ni msomi . Jane Gatoni anamsifia kwa ugwiji wake katika lugha ya kiswahili kinyume na wengine waendao nje ya nchi zao ambao hugeuka na kudharau lugha yao. Vilevile Siri anawafundisha wachina wengi kiswahili. Siri anatetea kauli hizi za kupenda kiswahili hata akiwa nje ya nchi kwa sababu ya vitabu alivyosoma akiwa shule ya upili ; mwisho wa kosa. Huu ni usomi wa hali ya juu kwa siri.

**WAHUSIKA**

1. **Jack**

Ni rafiki ya siri

**Sifa zake**

***Ni mwerevu***

- Aliibuka mshindi kwenye shindano la somo la sayansi, japo nafasi yake ilipokwa, siri anasema kuwa kazi yake ilikuwa ya kupigiwa mfano na mawazo na fomyula alizoibua Jack zimetumiwa vitabuni.
- Katika mtihani wa kidato cha nne yeye pamoja na siri walipita kwa alama za juu. Hii haikutosha maana Jack alimpiku siri kwa alama tatu.
- Alikuwa na ujuzi wa kuunganisha mitambo na kuhakikisha kuwa mawasiliano ya siri na wazazi wake yalifanikiwa. Hii ni licha ya yeye kuwa hajasoma na kufika chuo kikuu.

***Ni mwenye kusamehe***

- Alikuwa radhi kuwasamehe wote, kuanzia kwa Siri hadi wazazi wake licha ya kupokwa nafasi ya ushindi wake kwenye shindano la somo la sayansi miongoni mwa shule za upili.
- Siri anamtaja Jack kama ambaye hana kinyongo hata baada ya kutendewa maovu. ( UK 73)

**Umuhimu wa Jack**

- Anaendeleza maudhui ya elimu. Alikuwa mwerevu na mwenye bidii shuleni
- Ni kielelezo cha watoto mayatima ambao hupitia hali ngumu na hata kukandamizwa katika jamii
- Kupitia kwake tunapata sifa za wazazi wa Siri kuwa ni katili.

**2. Siri**

Ni mwanawe kalia na Bi. Mshewa. Vilevile ni rafiki wa dhati wa Jack.

**Sifa zake**

*Ni msomi*

- Alisoma pamoja na Jack kwenye shule ya msingi na shule ya upili. Wote na siri walipata alama za juu kwenye mtihani wao wa mwisho wa kidato cha nne.
- Anaeleza namna anavyopenda kusoma kiswahili na licha ya yeye kuwa msomi wa kisayansi, alisoma riwaya ya mwisho wa kosa na vile vile yeye husoma riwaya na tamthilia mbili kila mwezi na angalau diwani ya mashairi kila baada ya miezi miwili.
- Aliibuka wa tatu kwenye shindano la somo la sayansi kwenye shule za upili.

*Ni mpatanishi/ mpenda toba*

- Alipanga mahojiano ya runinga ya kikwetu yaliyoishia kuvumbua uovu aliofanyiwa Jack na hapohapo kuombana msamaha na kuamua kuishi vizuri hapo na hata baadaye.

*Ni mwenye mapenzi*

- Aliwapenda wazazi wake ndio maana aliwasiliana nao kila mara kutumia njia ya skype. Jack ndiye huunganisha mitambo.

  **Umuhimu wa siri**

- Ni kielelezo cha watu ambao hujuta baada ya wengine kutendewa maovu na kuomba msamaha
- Anaendeleza maudhui ya elimu. Alikuwa mwerevu na mwenye bidii shuleni

3. **Kalia**

Ni babake siri na mumewe bi. Mshewa.

**Sifa zake**

*Ni mwenye mapenzi*

- Alimpenda mwanawe sana kiasi cha kumpoka Jack ushindi na kumpatia Siri nafasi ya kupata ufadhili wa shahada ya uzamifu kutoka Uchina.

***Ni fisadi***

- Alimpoka Jack nafasi ya ushindi wa shindano la somo la sayansi na kukosa nafasi ya ufadhili wa shahada ya uzamivu Uchina. Alitumia nafasi yake ya kuwa mwanakamati katika wizara ya sayansi na teknolojia iliyoshughulika na mipango ya kufanikisha hafla hiyo.

***Ni katili/ dhalimu***

- Alimpoka Jack ushindi wa shindano la somo la sayansi na kukosa nafasi ya ufadhili wa shahada ya uzamifu Uchina. Licha ya yeye kuwa na uwezo wa kifedha kumwelimisha mwanawe siri, pia hakuchukua nafasi ya kumwelimisha hadi baada ya Siri kutoboa siri kwenye runinga.

***Ni mnafiki***

- Waliahidi kuwa wangemfunza Jack hadi afikie kilele cha masomo yake katika mazishi ya wazazi wake waliofariki katika ajali ya barabara, ila badala yake hawakumsaidia na mbaya zaidi kumpokea Jack ushindi wake kwenye shindano la somo la sayansi.

**Umuhimu wa Kalia**

- Ni kielelezo cha wazazi ambao ni fisadi. Anamwibia Jack ushindi wake
- Anaendeleza maudhui ya ukatili namna alivyomfanyia Jack

4. **Bi.mshewa**

Ni mkewe Kalia na mamake siri.

**Sifa zake**

***Ni mnafiki***

- Waliahidi kuwa wangemfunza Jack hadi afikie kilele cha masomo yake katika mazishi ya wazazi wake waliofariki katika ajali mbaya ya barabarani, na hawakufanya hivyo. Badala yake alimwitisha Jack nusu ya faida ya biashara yake ya viatu alipoona fanaka kwenye biashara hiyo.

***Ni msomi***

- Ni mwalimu wa kiswahili katika shule waliyosomea Jack na siri, na alifurahi sana Jane Gatoni alivyozungumza kiswahili kwa ufasaha.

***Ni mwenye kujirudi***

- Anaungama makosa yake kwa kuonea Kijicho mafanikio ya biashara ya Jack ya kuuza viatu na kumwitisha nusu ya faida . Anasema kuwa hataki laana kwa wanawe. ( UK 74)

5. **Jane Gatoni**

Ni mtangazaji wa runinga ya kikwetu.

**Sifa zake**

***Ni mchangamfu***

- Aliwakaribisha wageni ; Kalia, Bi. Mshewa na siri kwa uchangamfu kwenye mahojiano siku hiyo.

***Ana umilisi wa kiswahilli.***

- Alizungumza kiswahili kwa ufasaha uliomfurahisha Bi. Mshewa ambaye anafundisha kiswahili katika shule ya upili ya Kayole.

***Ni mkarimu***

- Aliwakaribisha Kalia, Bi.mshewa na siri kwenye kipindi cha mahojiano kwenye runinga ya kikwetu, kisha kuwakaribisha kwa kuwapa sharubati ya machungwa.

***Ni mwenye shukrani***

- Alishukuru Siri kwa kukubali mwito wa kuhudhuria kipindi hicho cha nyumbani ni nyumbani. ( UK 79)
- Kipindi kilipoisha aliwasalimia watatu hao, aliwashukuru kwa muda wao kisha akahitimisha kipindi. ( UK 75)

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Tashbihi**

- Meno meupe mithili ya theluji. ( UK 69)

**Taswira**

- Tunapewa taswira za mwonekano wa Siri. Msimulizi anasema kuwa; "Urefu wa kimo , rangi ya maji ya kunde na macho meupe mithili ya theluji....." ( UK 69)
- Tunapata taswira ya ukumbi wa mahojiano. Anasema "Ukumbi wa mahojiano ulishamri usafi asiowahi kuona Jack. Makochi yenye rangi ya manjano yalipendeza mno...."
- Msomaji anapewa taswira ya urembo wa mtangazaji Jane Gatoni. Anasema ; "Alikuwa mrembo kupindukia na mavazi yake yalioingiana sawasawa na mada alizoshughulikia katika kipindi chake cha nyumbani ni nyumbani" ( UK 70

**Tabaini**

- Si masomo, si michezo, si kifedha. ( UK 69)

**Uhuishaji**

- Lilikuwa limetii (shati) amri ya kunyooka. ( UK 69)
- ........tamaa ilinivaa. ( UK 74)

**Nidaa**

- ........ safari hizi! ( UK 69)
- ........ Amani ! ( UK 71)
- Mwanangu! ( UK 71)
- .........kipasua mbarika! ( UK 72)
- Jack! ( UK 72)
- ............. Si mimi niliyeshinda! ( UK. 72)

**Methali**

- Lisilobudi hubidi. ( UK 74)
- Maji alikwisha yavulia nguo, sharti ayaoge. ( UK 74)

**Majazi**

**Siri**

Jina lake halisi ni siri bin Kalia. Alificha siri ya kufichua kupokwa kwa ushindi wa Jack wa lile shindano la somo la sayansi na akakosa ufadhili. Msimulizi anatueleza kuwa, siri alimwonya Jack dhidi ya kumweleza yeyote haswa wazazi wake. Hatimaye alitoboa siri ile kwa ulimwengu kupitia runinga ya kikwetu na wakaishia kuombana msamaha.

**Jack masumbuko.**

Ni rafiki yake siri.

Masumbuko ni hali ya taabu dhiki na mashaka. Jack masumbuko anapitia hali ya masumbuko; Kwanza kwa kupoteza wazazi wake na kubakia yatima, kisha katika uyatima huu anapokwa ushindi wake wa shindano la somo la sayansi. Vilevile anakosa karo na kukosa kujiunga na chuo kikuu licha ya kupita mtihani wake, ni miaka saba sasa. Jack pia analazimika kumpa bi.mshewa nusu ya faida ya biashara yake ya kuuza viatu. Hana budi ila kusalimu amri kwa sababu ya unyonge wake. Haya yote ni masumbuko.

## 11. NIPE NAFASI-Mzamane Nhalapo

### MTIRIRIKO

Mama aliamka mapema huku macho yakiwa mekundi kana kwamba alikuwa amelia usiku kucha na kusema,"Leo tunaenda makongeni kwa jamaa ya baba yenu", kwa sababu tukiendelea kukaa hapa hatutaweza kupata chakula.”

Tulianza safari. Hewa ilikuwa ya baridi shadidi na iligandisha mwili kabla ya kufika kijijini mwili wa mkhathini ulikuwa umekakamaa na ngozi yake ilikuwa imechujuka. Hakuwa anapumua.

Tulipofika kwa jamaa yake baba kulikuwa na mchanganyiko wa furaha na huzuni.Jamaa yake baba ilifurahi kutuona sisi watoto wa Ndugu yao, lakini taswira ya mama akiwa amebeba maiti ya ndugu yetu Mkhathini iliwatia wasiwasi.

Mama alikuwa na maswali ya kujibu hasa kwa kutoomba ruhusu ya kuja kutoka kwa Mumewe au wakwe zake. Mama alijibu "Ninawataka wanawake waelewe kuwa wanaume wanaposhindwa kutekeleza wajibu wao kama viongozi katika familia kiasi kwamba watoto wao wanakufa njaa, hawafai kukaa tu bila kuchukua hatua zozote."

Jibu lile la mama lilileta minong'ono katika nyumba ile, wanaume katika nyumba ile walikuwa hawatulii walihisi kuwa mama alikuwa amewatusi na bila shaka kuna wale waliotamani wangekuwa na nafasi wasingechelea kumtia mikononi na kumrudi vilivyo.

Mama akiendelea kusema kuwa wanawake wanachukuliwa kuwa watu dhaifu na wenye vitambuzi finyu wanalazimika kuomba ruhusu ya kufanya hata mambo madogo kama vile kuwatembelea marafiki na wazazi wao, kutafuta ajira, kujiendeleza kimasomo, kutafuta ufadhili au mikopo hata serikali zinanyima wanawake uhuru.

Matweba na wanaume wenzake walikuwa wamejaribu sana kuzilinda tamaduni na desturi, pamoja na kuisimamisha familia ya Belo. Mwishoni mwa nwaka huo, mamangu alikuwa mwalimu wa shule ya msingi, bila idhini ya mumewe wala wazazi wa mume wake.

**ANWANI.**

Wanaume katika hadithi hii hawataki wanawake kupewa ruhusu ya kufanya mambo.

Mama Kazili alihitaji kuomba ruhusu kutoka kwa mumewe au wakwe ya kufanya mambo madogo kama vile:

- Kuwatembelea marafiki na wazazi wao
- Kutafuta ajira
- Kujiendeleza kimasomo
- Kutafuta ufadhili au mikopo

Wanaume walikuwa katika nyumba ile walitamani wangekuwa na nafasi wasingechelea kumtia mikononi na kumrudi vilivyo hii ni kwa sababu walihisi kuwa mama Kazili alikuwa amewakosea heshima.

**DHAMIRA.**

- Lengo kuu la mwandishi ni kuonyesha namna utamaduni katika serikali ilivyowakandamiza wanawake, kwa mfano chama cha taifa cha Basutoland ambayo kila mara inajigamba kwamba imechaguliwa na wanawake kwa kuwa wanaume wanashabikia chama cha Basutoland Congress party, mama Kazili anasisitiza kuwa jamii na serikali zinawanyima uhuru.
- Mwandishi pia alitaka kuonyesha changamoto nyingi ambazo mwanamke anapitia katika jamii, kwenye ndoa na hata taifa zima lenye sera za kumkandamiza.
- Mwandishi alidhamiria kuonyesha nafasi kuu ambayo mwanamke anatekeleza kwenye jamii haswa kuisimamisha ndoa na kuwalea watoto.

**MAUDHUI.**

**1.UTAMADUNI**

- Wazazi wa baba ya msimulizi walimtaka mama yake kuelewa kuwa mume kuwa na wake wengi lilikuwa jambo la kawaida jambo ambalo 'mke mwema' hakufaa kulalamika (uk76)
- Mwanamke alistahili kuomba ruhusu kutoka kwa mumewe au wakwe alipotaka kutembelea jamaa. Matweba alimuuliza ,'ina maana kwamba hukuomba ruhusu ya kuja huku kutoka kwa mumeo au wakwe zako?'.(uk 78)
- Sheria za kijamii zinamchukulia mwanamke kama mtoto anayetarajiwa kuwa chini ya uelekezi na utunzaji wa mwanaume (uk 80)
- Maamuzi yaliyofanyiwa kwenye kraal yalikuwa hayawezi kubatilishwa. Maamuzi hayo yalichukuliwa kuwa matakatifu kwa Maana waume walitakaswa na Viongozi wa familia na mwenyezi Mungu (uk 81)
- Mama Kazili alitaka kuwaacha watoto wake kwa jamaa mpaka hali itakapokuwa sawa lakini jamaa za mumewe wakasema hawatakubali amdhalilishe mumewe kwa kuwatawanya watoto wake kwa kusingizio cha kutafuta kazi pasi na kibali kutoka kwa yeyote.

## 2.NAFASI YA MWANAMKE KATIKA JAMII

- Mwanamke alistahili kuzaa ili kuendeleza familia. Msimulizi anasema kuwa mamake alihitaji kuwa makini alipozungumza la sivyo,wanagemkumbusha kuwa Ndugu yao hakumwoa kutoka Swaziland kuwaulia watoto, aliolewa pale kuwatengeneza watoto na kuendeleza familia ile (Uk 78)
- Mwanamke kuadhibiwa na mumewe-Msimulizi anasema kuwa mwanamke mmoja aliadhibiwa Vikali kwa kumwambia mumewe waziwazi kuwa alikuwa mzembe (uk79)
- Wanawake wanachukuliwa kuwa watu dhaifu na wenye utambuzi finyu, wanalazimika kuomba ruhusu ya kufanya hata mambo madogo kama vile kuwatembelea marafiki na wazazi wao.
- Mama Kazili akiendelea kusema kuwa serikali ilitekeleza hila ambayo kila mara inajigamba kwamba imechaguliwa na wanawake kwa kuwa wanaume wanashabikia chama cha Basutoland Congress party. Jamii na serikali zinawanyima wanawake uhuru (uk 80)
- Wanawake waliketi sakafuni na wanaume waliketi kwenye viti (uk81)

## 3.UMASKINI.

- Mamake  Msimulizi kukopeshwa pesa za nauli ya gari na mwanamke mwenye huruma kijijini.(uk77)
- Msimulizi na mamake walisafiri hadi huku kwa jamaa ya baba yao kwa sababu nyumbani hawakuwa na chakula

## 4.BIDII

- Mwishoni mamake Msimulizi alikuwa mwalimu wa shule ya Msingi ,bila idhini ya baba wala wazazi wa mume kutokana na mshahara, walienda shule.

## 5.MAUTI

- Mkhathini aliaga dunia (uk77)

**6.USHIRIKIANO**

- Wafuga farasi walikuja kuwachukua watu katika janibu hizi waliwajali wengine kuliko wale walioishi kwenye sehemu tambarare au mjini.

**WAHUSIKA**

**MOSHE (BABAKE MSIMULIZI)**

***.Mwenye bidii.***

- ➢ Alienda Afrika Kusini kufanya kazi migodini (uk76)

***Ana mapuuza.***

- ➢ Alipuuza familia yake alipokosa kutuma pesa za matumizi

***Ni mzinzi.***

- ➢ Kulikuwa na uvumi kwamba alikuwa na mke mwingine huko migodini.

**Umuhimu wa Moshe**

- Ni kielelezo cha wanaume ambao wanakosa kujukumika kikamilifu majukumu ya unyumba
- Kupitia kwake tunapata sifa za mama Kazili kuwa ni mwenye kuwajibika, anawakimu wanawe kikamilifu bila usaidizi wa mumewe

**WAZAZI WA MOSHE.**

***Ni Watamaduni***

- ➢ Walikuwa wamedinda kusikiliza malalamishi ya mamake Msimulizi kuhusu suala la mke mwingine na walimtaka mamake kuelewa kuwa mume kuwa na wake wengi ilikuwa jambo la kawaida.

**MAMA KAZILI**

***Mvumilivu.***

- Yeye na watoto wake walivumilia hali ngumu ya maisha hata mumewe alipokataa kuwatumia pesa za matumizi na Kutumia wazazi wake.

***Ni Jasiri***

Alikabiliwa na jamaa za mume wake hasa waliposema arudi swaziland .Alisema "Hakuna yeyote anayeweza kunilazimisha kurudi swaziland hata huyo mume wangu"

***Ni Mwenye bidii***

- Aliupanga utamaduni na kuhakikisha kuwa amekuwa mwalimu bila idhini ya wazazi wa mume wala mume na kutokana na mshahara wake mdogo aliwapeleka watoto wake shuleni.

**Umuhimu wa Mama Kazili**

- Anawakilisha wanawake ambao ni jasiri kiasi cha kupinga maovu dhidi yao
- Anaendeleza maudhui ya uwajibikaji. Anawakimu wanawe kikamilifu licha ya mumewe kutelekeza majukumu yake
- Kupitia kwake tunapata sifa za Moshe, kuwa ana taasubi za kiume.

4***.Matweba***

***Ana taasubi ya kiume***

- Yeye pamoja na wanaume wa familia ya Belo wanawakandamiza wanawake kuwa chochote mwanamke afanyacho lazima aombe ruhusa.

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

**1.Chuku**

- ★ Hewa ilikuwa ya baridi shadidi na iligandisha hata boho za mifupa mwilini(uk77)

**2.Uzungumzi nafsia**

- ★ Mamake Msimulizi alikuwa akijizungumzia kwa kusema "Nitarudi na kufanya kazi ili niweze kuwakimu leo lazima watapata chajio....(uk77)

**3.Mbinu rejeshi**

- ★ Msimulizi anakumbuka kesi moja iliyokuwa imefanyika miaka miwili iliyopita kijijini habelo, ambapo mwanamke mmoja alikuwa amemwambia mumewe waziwazi kuwa alikuwa mzembe (uk79)

## 12. NILITAMANI-Phibian Muthama

### MTIRIRIKO

Tumaini anapitia hali ngumu ya kifedha. Hadithi inaanza adhuhuri hii yenye jua la utosini anapoanza kutembea kijiji baada ya kijiji, vichochoroni na barabarani angalau kutafuta riziki. Anahisi njaa sana.

Baada ya kuishi na Nina kwa muda sasa, Tumaini aliamua kuhama na kujiishia. Nina alikuwa mwenye roho safi na alimfaa kwa mengi ila hakutaka kuendelea kumtegemea sana. Alienda stendi na kuomba usaidizi wa konda na akafikishwa kariokoo, naye konda akafanya hivyo.

Kwenye tembea tembea zake, Tumaini alipatana na booking office ya mabasi ya Tahmeed. Hapo alienda akaomba msaada wa ajira, chakula na nauli. Alipewa shilingi elfu tano za Tanzania na namba yake ya simu. Hapo alizitumia hizo pesa kuununua urojo na kisha

kununua mboga za matembele alizoenda nazo nyumbani kwa kyondo. Rafiki yake Jenifer alifurahi sana kwa ujio wake

Jumamosi moja Tumaini alitumiwa pesa na rafiki yake. Hii ilikuwa bahati ajabu. Aliamua kubarizi coco beach. Huku alipatana na mwanaume mmoja kwa kina Romeo. Mwanaume huyu alikuwa mtanashati na mwenye matumaini makubwa ya mapenzi ya kweli na ndoa kwa Tumaini. Mwishowe waliingia garini na Tumaini na akaanza kupelekwa asikojua. Baada ya mwendo wa saa moja hivi Romeo aliegesha gari na kuanza kumwonyesha Tumaini majumba ya kifahari karibu na ufuo wa bahari. Romeo hatimaye alimpasulia Tumaini mbarika kuwa walipokuwa palikuwa peponi naye Romeo hakuwa mtu wa kawaida. Kidogokidogo Tumaini alisikia mawasiliano ya Romeo kwa simu yakisema; "*We need her blood faster*!" Tumaini alishtuka sana. Huku Romeo akiendelea kuzungumza kwa simu, Tumaini aliruka nje na kuponyoka. Hii haikuwa ndoto yake kati ya mambo mengi aliyotamani.

**DHAMIRA**

- Mwandishi alikusudia kukashifu tamaa nyingi zinazoweza kuelekeza mtu kwa hatari
- Vilevile alidhamiria kuelimisha watu wawe macho na makini kutoamini watu wanaoonekana kuwa wazuri kwa macho, huenda wana nia mbaya kwao.
- Dhamira ya mwandishi vilevile ni kuwatia moyo vijana ili watie tija zaidi katika juhudi zao za kutafuta ufanisi na wasitegemee wala kutarajia kupata ufanisi huu kwa njia za mkato.

**ANWANI**

Kutamani ni kupata hamu ya kupata au kuwa na kitu fulani.

- Tumaini anayatamani maisha aliyoishi Nina. Anasema ; "Nilihisi nikaze kamba , nami niishi maisha kama yake au zaidi ya yake, maisha yanikubali, nami nikayakubali, tukakubaliana na kukafaana " ( UK 85)

- Tumaini anabarizi kwenye ufuo wa bahari pale coco beach, mawazo ya tamaa ya maisha mazuri yanamvaa. Anasema; "Nikaanza kuvuta taswira ya maisha mapya, nifanyeje nipate kitakacho?"
- Baada ya kupatana na Romeo, Tumaini anamwona mtanashati na kutamani kuwa mpenzi wake wa ndoa. Amwoe kama jana vile. ( UK 89)
- Mwishoni mwa hadithi, msimulizi – Tumaini analaani tamaa nyingi aliyokuwa nayo na ambayo aliona kama karibu imwelekeze pabaya na kwenye hatari nyingi.  Anasema 'Nilitamani niwe na mali na mume mzuri lakini si kwa namna hii.' ( UK 91)

**MAUDHUI**

***Tamaa***

- Tumaini anatamani kuyaboresha maisha yake na kuyatoa kwa hali mbaya yaliyo ndani. Anasema ; "Nimekuwa nikiwaza na kutafakari sasa jinsi ya kuishi maisha bora , yanifaayo na niyafaayo........Natumai na kuota mambo yatakuwa barabara" ( UK 84)
- Tumaini anatamani maisha aliyoishi Nina. Anasema alimwonea Kijicho alivyokuwa na mume mzuri, mali nyingi waliyomiliki naye. Anasema; "nilihisi nikaze kamba nami niishi maisha kama yake au zaidi ya yake, maisha yanikubali nami niyakubali, tukubaliane na tufaane" ( UK 85)
- Tumaini alipokuwa anabarizi kwenye ufuo wa bahari pale coco beach, mawazo ya tamaa ya maisha mazuri yanamvaa. Anasema; "Nikaanza kuvuta taswira ya maisha mapya, nifanyeje nipate nitakacho? ( UK 88 )
- Baada ya kupatana na Romeo, Tumaini anamwona mtanashati na kutamani kuwa mpenzi wake wa ndoa. Amwoe kama vile jana. ( UK 89)
- Hatari aliyopitia Tumaini kuishia kupelekwa peponi na Romeo aliyetokea kuwa si mtu wa kawaida na hata kuhatarisha maisha yake aliposikia mazungumzo ya simu ya Romeo......; "*we need her blood faster*!" Inamfanya Tumaini kulaani tamaa ya kuzidi aliyokuwa

nayo. Anasema; “ Nikatamani nijipate kwetu Kenya ikiwa miguu yangu ingeniruhusu. Nilitamani niwe na mali na mume mzuri lakini si kwa namna hivi.”

***Umaskini***

- Ni uchochole au ukosefu wa uwezo wa kifedha wa mtu kujikimu. Tumaini anahisi uchovu baada ya kutembea mwendo mrefu na kwenye jua la utosini kutafuta riziki. Anasema; “Nimetembea tangu asubuhi kijiji baada ya kijiji, vichochoroni na barabarani, kusaka cha kutafunia siku hii na pengine cha kusukuma wiki!” Hii ni hali ya umaskini bila shaka.
- Ukosefu wa pesa unamfanya Tumaini kuomba konda ampeleke mjini japo hakuwa na hela. Konda anamkubalia na kumpeleka hadi kariokoo. Vilevile analazimika kuomba usaidizi wa kifedha pale kwenye booking office ya Tahmeed na anapewa shilingi elfu tano za Tanzania. Hizi anazitumia kuununua urojo na mboga za matembele alizoenda nazo kwa kyondo kwa rafiki yake Jenifer aliyefurahi sana.
- Umaskini na tamaa vinamfanya Tumaini kujiingiza kwenye hatari iliyotishia kumpotezea maisha. Anashawishika kumpenda Romeo, mtu waliyejuana kwa kipindi kifupi sana hadi anampeleka kwenye gari hadi sehemu asiyojua na kumpasulia mbarika kuwa hakuwa mtu wa kawaida na alikuwa amempeleka peponi. Tumaini anatoka na kunusurika kwenye mtego huu na kalaani umaskini na tamaa iliyomfikisha kwenye hali kama hii.

***Udugu na kufaana.***

- Ni hali ya kusaidia mwenzake japo hamna mahusiano ya kiukoo na bila kutarajia kitu kwa niaba ya huo msaada.
- Nina anaonekana rafiki wa dhati. Tumaini aliishi kwake kwa miezi mitatu bila manung’uniko na kung’aa kwa mambo mengi. Tumaini anasema; “kila siku niliona kama nipo likizoni maana alinitembeza sehemu hadi sehemu, kuona miji tofautitofauti na kujua jinsi nitakavyokabiliana na hali ya maisha katika nchi hii. Alinifunza mambo aina aina si upishi, si kuishi na watu kwa wema na kunitoa usungo!” ( UK 84)

- Konda anaonekana mtu mwenye utu anapomsaidia Tumaini kwa kumsafirisha mjini akiwa hana hela. Huu ni udugu na kufaana wa hali ya juu.
- Mhudumu wa kampuni ya Tahmeed aliyekuwa upande wa kushoto anamsaidia Tumaini na shilingi elfu tano za Tanzania. Hizi zinamsaidia kununua urojo na mboga za matembele anazoenda nazo kwa Jenifer jioni ile.
- Jenifer anamhifadhi Tumaini kipindi hiki anachopitia hali ngumu ambayo hakuwa na pesa wala kibarua. Tumaini anasema; " alikuwa si mtu wa makuu. Alitosheka na hicho tu nami nilipenda uelewa wake. Ni nadra kupata mwanamke wa namna yake mjini zama hizi, nadra sana." ( UK 77)
- Romeo anaonekana mwenye msaada kwa Tumaini mwanzoni. Anamtaja Tumaini kimapenzi na kutaka kumwoa pia. Anamwambia Tumaini atakavyomfanya Kuwa tajiri. Inakuja kufikia mwishowe Kuwa kumbe huu haukuwa udugu wa kufaana wala mapenzi ya kweli kwake bali utapeli. Alikuwa mtu asiye wa kawaida na alipanga njama ya mauaji ya Tumaini, ikabidi Tumaini atoroke.

**WAHUSIKA**

1. **Tumaini**

**Sifa zake.**

***Ni mwenye tamaa***

- Anatamani kuishi maisha kama ya Nina. Anasema; "Nilihisi nikaze kamba nami niishi maisha kama yake au zaidi ya yake...." ( UK 85)
- Alitamani maisha mema; " ... Nilitamani na kutaka. Nilipanda gazi kutoka kutamani na kuanza kutaka. Nilitaka yaliyo mema na mazuri. Maisha matamu." ( UK 87)
- Anatamani mapenzi na ndoa ya Romeo. Anasema; " Nilitamani niwe mpenzi wake wa ndoa. Anioe kama jana vile..." ( UK 89)

***Ni mwongo***

- Alimdanganya konda kuwa  amepoteza kipochi chake cha pesa ili apate usafiri hadi mjini. ( UK 85)
- Alikuwa akimdanganya  Jenifer Kuwa alikuwa amekula kila akitoka ili asimzidishie ghadhabu na gharama nyingi. ( UK 88)

***Ana mlahaka mzuri na watu***

- Aliishi vizuri na Nina na hata Jenifer.
- Alijua kuwarai konda na yule mhudumu wa mabasi ya Tahmeed ili kupata msaada. Aliitaka na akapata.

***Ni mwenye kujali***

- Alijali hali ya Jenifer ndio maana alimdanganya kuwa alikula atokako ili asimzidishie ghadhabu na gharama nyingi. ( UK 88)

***Ni mwenye kushawishika***

- Alishawishika na muonekano wa Romeo na maneno yake ya kushawishi na kukubali kwenda naye kwa gari asikokujua.

***Ni mcha Mungu***

- Alimlilia Mungu wake ili amwonyeshe njia wakati ule akiwa katika hali ngumu ya kifedha. ( UK 85)
- Aliwaza kuwa Mungu alikuwa ameenda likizo asiweze kumsaidia katika hali ngumu aliyokuwa nayo, ila akaamini kuwa hakuwa amemwasha kamwe. Alizidi kujipa matumaini. ( UK 87)
- Siku ile alipotumiwa visenti na Nina kwenye laini yake, aliona kama Mungu ametuma malaika wake. ( UK 88)
- Baada ya kupatana na Romeo, Tumaini alifurahi sana na kumshukuru Mungu (UK 89) kwa kukutana na mwanaume mtanashati duniani na aliyetamani kuwa naye kwenye ndoto zake.

**Umuhimu wa Tumaini**

- Anaendeleza maudhui ya tamaa. Tamaa yake inaendekeza na kukaribia kumsababishia maafa.
- Kupitia kwake tunapata sifa za Romeo kuwa ni katili. Alipanga kumuua Tumaini
- Ni kielelezo cha wasichana wenye tamaa ya kupitiliza ambayo huishia kuwasababishia madhara

**2. Nina**

**Sifa zake**

***Ni mkarimu***

- Alitumia Tumaini visenti kwenye laini yake siku ile alipompigia simu kumjulia hali. ( UK 58)

***Ni mwenye mapenzi/ kujali***

- Alimfaa sana Tumaini alipofika pale kwao. Anasema ; " Nina alikuwa kama mwanangu, alinichunuku yule mama...." ( UK 84).
- Tumaini anasema kuwa Nina aliishi naye kwa upendo. ( UK 84)

***Ni mwenye mausia***

- Alimwelekeza Tumaini namna ya kuishi humo mjini. Akamweleza namna wabongo walivyo wasanii, na awe makini nao. Awapende ila ajichunge. ( UK 84- 85)

***Ni tajiri***

- Walikuwa na uwezo mkubwa wa kifedha na kujihikimu. Tumaini anasema kuwa walimiliki Mashamba ya misitu na magari ya usafiri, viwanda na nyumba yao ya kuishi kama kasri la sultani vile. ( UK 85)

**3. Mhudumu wa booking office ya Tahmeed ( aliyekuwa upande wa kushoto)**

***Ni mkarimu***

- Alimpa Tumaini shilingi elfu tano za Tanzania alipomweleza shida alikuwa nazo.

***Mwenye shauku/ kusita***

- Alisita kuongea na Tumaini huku akishuku kuwa huenda angekuwa tapeli. ( UK 86)

***Ni msikivu***

- Alitoka nje na kumsikiliza Tumaini kama alivyokuwa ameomba.

4. **Romeo**

**Sifa zake**

***Ni mtanashati***

- Tumaini anashabikia siku aliyokutana na mwanaume mtanashati zaidi duniani. ( UK 89)

***Ni tapeli/ mwongo***

- Alimdanganya Tumaini mwanzoni kuwa alimpenda sana na alitaka kumwoa, kumbe mwishowe alikuwa na nia ya kumpeleka peponi na kumwua.

## MBINU ZA UANDISHI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Tanakuzi**

- ..,... yanifaayo na niyafaayo. ( UK 84)
- Mlango huu ukifungika na huu mwingine unafunguka. (UK 87)
- Mimi naye, naye nami. (UK 87)
- Nilivyo vitamani vyote nikavilaani. ( UK 90)
- Nafumba macho nikiyafumbua. (UK 90)

**Nahau**

- Kusaka tonge. ( UK 84)

- ★ Nikanze kamba.  ( UK 85)
- ★ Sikukata tamaa. ( UK 87)

**Takriri**

- ★ Tofautitofauti. ( UK 84)
- ★ Ainaaina. ( UK 84)
- ★ Huu na huu. ( UK 85)
- ★ Narandaranda. ( UK 86)
- ★ Nijipate. ( UK 85)
- ★ Maisha yaleyale. ( UK 85)
- ★ Nahitaji. ( UK 86)
- ★ Nadra. ( UK 87)
- ★ Mimi naye, naye nami. ( UK 87)

**Tabaini**

- ★ Si upishi, si kuishi.... ( UK 84)
- ★ Pumzi si zangu. ( UK 90)

**Nidaa**

- ★ Bora uhai! ( UK 85)
- ★ Eweee! ( UK 85)
- ★ Hakuna ibada iliyonipita! ( UK 87)
- ★ Niliuona kama laana hasa! ( UK 88)
- ★ Westlands! ( UK 89)
- ★ Mashallal! ( Uk 89)
- ★ Mwanaume mtanashati zaidi duniani! ( UK 89)
- ★ Sio mchezo kumpata wa kitu yako eti! ( UK 89)
- ★ Kuniangamizia Mwanga! ( UK 90)
- ★ Bahati iliyoje! ( UK 90)
- ★ Alaa! ( UK 90)
- ★ Yarabi! ( UK 90)
- ★ Duh! ( UK 90)
- ★ Pyu! (UK 90)
- ★ Pumzi si zangu! ( UK 91)

**Uhuishaji**

- ★ Miguu iliyojaa vizuri. ( UK 85)
- ★ Maisha yanikubali nami niyakubali, tukubaliane na tufaane. ( UK 85)
- ★ Sura ya tewengu niliyokuwa nimevaa. ( UK 85)
- ★ Nikawa naona nimefumaniwa na maisha. ( UK 85)
- ★ Machweo yanabisha. ( UK 86)
- ★ Maswali yalikuwa yanasema na akilia yangu. (UK 87)
- ★ Kila dakika ikiunda saa na kuunganisha siku. ( UK 87)
- ★ Maisha yashakuwa mkondo mpya. ( UK 88)
- ★ Nilitaka nifukuze ukata. ( UK 88)
- ★ Uzuri wake uliukubalisha moyo wangu. ( UK 89)
- ★ Niliona kama mwezi umechukua zamu ya jua. ( UK 90)

**Tashbihi**

- ★ Kuishi kama kasri la sultani vile. ( UK 85)
- ★ Nami niishi maisha kama yake au zaidi ya yake. (UK 85)
- ★ Meupe kama theluji. ( UK 89)
- ★ Tukawa kama pacha wa huba. ( UK 90)
- ★ Maisha kama peponi. ( UK 90)

**Methali**

- ★ Maskini hachoki, akichoka keshapata. ( UK 85)
- ★ Mikono mitupu hairambwi. ( UK 86)
- ★ Kawia, ufike. (UK 90)

**Maswali ya balagha**

- ➢ Nifanyeje mimi mgeni? (UK 85)
- ➢ Ningerudi na nini hasa? ( UK 87)
- ➢ Bibi angenipokeaje? ( UK 87)
- ➢ Maisha ni kuishi leo, wa kesho aishile? (UK 88)
- ➢ Mbona mitihani inanizonga namna hivi? ( UK 91)

**Utohozi**

- ★ Mesenja. ( UK 85)

**Dayalojia**

- ★ Kuna dayalojia kati ya Tumaini na mhudumu wa kampuni ya mabasi ya Tahmeed aliyekuwa upande wa kushoto.
- ★ Kuna dayalojia kati ya Tumaini na Romeo.

**Sadfa**

- ★ Ilikuwa sadfa kuwa namna Tumaini alivyokuwa akimwangalia Romeo, alipata kuwa wakati huo Romeo naye alikuwa anamtazama. ( UK 90)

**13. PUPA-F.M Kagwa**

**MTIRIRIKO**

Mwakuona alizaliwa na kulelewa katika mtaa duni wenye nyumba zisizo za thamani. Alikuwa mwanambee miongoni mwa watoto kumi na wawili. Chakula pia kilikuwa shida nyumbani kwao.

Jioni moja alitoka shuleni Kazamoyo, Mwakuona alimwona bibi fulani. Alimsalimu kisha akajitambulisha kama mfanyakazi katika kampuni moja maarufu mjini ambayo ilikuwa ikitafuta vijilanga wa kudhamini.

Mwakuona naye alimtazama bibi yule kama mwokozi wake kutoka kwenye lindi la umaskini. Majadiliano yalinoga na baada ya muda mfupi wakaafikiana kuwa Mwakuona alikuwa atafute pasipoti katika muda wa juma moja. Nauli ya ndege ingegharamiwa na mwajiri wake angefanya jitihada kutimiza maagano.

Jioni ile mwakuona alipelekwa katika chumba mlimokuwa na wasichana wengine kadha. Mashaka, kijana chipukizi aliyekuwa amepitia ugumu wa maisha kule chenga-ways, mwingi wa huruma alimeza mate machungu na kujitahidi kumshauri atulie. Walishauriana kuwa watakapojinasua sharti watafute namna wangerudi masomoni wasome wawe wanaharakati ili wahamasishe wengine.

Baada ya miezi saba, Mwakuona aliweza kujinasua na kutoroka.Bidhaa muhimu mhimili mkuu wa biashara ametoweka .Askari wamo taabani kwa kupagazwa utepetevu. Tayari Mwakuona alikuwa amejinasua.

**DHAMIRA**

- Lengo juu la mwandishi ni kuwaonya vijana hasa wanaotoka katika familia chochote kutoshawishika haraka.
- Kuonya wale wanaofanya hila kama BI.mtego kuwa watakutana na mkono mrefu wa Sheria.

**ANWANI.**

Pupa ina Maana ya kuwa na tamaa. Mwakuona aliingiwa na pupa ndio maana hakuyapima mambo ya yule wakala kwa mfano:-

- Aliona vyakula alivyotamani kama pizza,nguo za bei rangi za kucha na midomo n.k
- Aliona mashangingi akaona kasri akaona ameheshimika katika jamii.
- Kwa akraba yake, aliona akiwanunulia nguo za bei na vyakula aina aina.
- Mwakuona anasema kuwa pupa imenitumbukiza kwenye kisima nilichochimba,sasa naingia nwenyewe (uk99)

**MAUDHUI**

**1.UMASKINI.**

- Mwinamo ulikuwa mtaa wenye nyumba nyingi zilizojiinamia ovyo kwa uzee. Kuta za nyumba zilijengwa kwa mabati makuukuu, kukandikwa kwa udongo, mahema makuukuu au hata katoni na karatasi (uk92)
- Kiu zaidi kwa Bwana na Bi.mtondo lilikuwa kupata angaa kibaba cha unga wa chakula, hii inadhihirisha umaskini uliokuwepo (uk92)
- Mwakuona na nduguze wakubwa wakati mwingi waliishia kuramba vyungu au kukwangura ukoko ili wadogo wao wapate angaa tonge kwani walitambuliwa na utapia mlo (uk92)
- Kutokana na ufukara wa wazazi wa mwakuona hakuweza kulipia Matangazo gazetini kuhusu kupotea kwa Mwakuona.

**3.TAMAA**

- Tamaa ilimfanya Mwakuona kuamini yote aliyoambiwa na wakala yule-Bi. Mtego. Aliona vyakula alivyotamani kama pizza, nguo za bei, rangi za kucha na midomo, wanja machoni n.k(uk93)

**4.ELIMU**

- Mashaka anamwambia Mwakuona kuwa watakapojinasua sharti warudi masomoni wasome ili wawe wanaharakati na waweze kuupinga udhalimu (uk98).
- Mwakuona alikumbuka walimu wakiwashauri kuwa elimu inawezesha kupata akili tambuzi, wachuje vifaavyo na kuacha vibaya.

**5.SIRI**

- Mwakuona aliyaweka siri mambo yote ambayo walikuwa wakifanya na wakala yule kwa mfano aliweka siri simu aliyopewa
- Mwakuona aliweka siri safari na nauli aliyopewa na wakala
- Aliweka siri viatu vya thamani kiasi na nguo alizofich
- Bi. Mtego aliweka siri nia yake ya kumpeleka Mwakuona Chengaways

**5.UKATILI.**

- BI.Mtego aliwadanganya wasichana wadogo eti anawapeleka ng'ambo baada ya wao kuandaliwa ili waelewane na mazingira ya ngambo na kuwaridhisha waajiri watarajiwa (uk95)kumbe wanapelekwa kwenye jengo la kifahari la Chenga-ways.

**6.ANASA NA STAREHE.**

- Kwenye jengo la kifahari la Chenga-ways kuna wasichana waliovalia nusu uchi mara wanaume waliokalia viti vya kifahari pale mapokezini wanasema "Nataka huyu au nipe yule" (uk96)
- Kabla ya kuandama chaguo lake Mwanamume angeenda kulipa palipoandikwa pay here.

- Mwakuona alitokwa na machozi njia mbilimbili kujua kwamba amegeuzwa kifaa cha kuuzwa na Kutumiwa ovyo na wanaume (uk 98)
- Serikali ilizifumbia macho biashara chafu iliyoendelea Chenga-ways baadhi ya waliokuja mle walikuwa maafisa tajika serikalini (uk99)

**8.Haki**

- Mwakuona na rafikiye mashaka walikuwa wamekubaliana kuwa wakiweza kujinasua watapiga ripoti kwa kituo cha polisi ili waweze kuwanusuru maskini wenzao na kuiangamiza biashara ile haramu (uk101).
- Ili kutafuta haki pia Mwakuona akilenga kutafuta Yaliyomo mashirika ya habari asimulie yaliyomfika wahalifu wale waanikwe (uk101).

**WAHUSIKA.**

**1.Mwakuona.**

***Mwenye Pupa***

- Alitamani vyakula kama pizza, nguo za bei rangi za kucha na midomo n.k Tamaa hii ilimwelekeza kutekwa nyara

***Mwepesi wa kushawishika***

- Anaamini ahadi za Bi.mtego na kutoroka nyumbani licha ya kuwa hawakuwa wamejuana kwa muda mrefu.

***Jasiri***

- Alijiamini na kutoroka licha ya kuwa ilikuwa vigumu sana kwa yeyote kutoroka kutoka maeneo yale.

***Ni Mcha Mungu***

- Anamkumbuka Mungu amuepushe na shari, afike asikokujua (uk100)

**UMUHIMU WA MWAKUONA**

- Anaendeleza maudhui ya pupa, anatamani vitu asivyoweza kupata.
- Kupitia kwake tunapata sifa za Bi.Mtego kuwa ni katili, Alipanga utekaji nyara wa Mwakuona.
- Anawakilisha wasichana ambao hushawishika haraka na mwishowe kujipata matatani k.m Mwakuona anashawishiwa na kujipata katika jengo la Chenga-ways

**2.Bi.Mtego**

***Ni Katili***

➢ Anaendeleza biashara haramu ya kuwateka wasichana nyara na kuwaingiza kwenye madanguro.

***Ni mwongo***

➢ Anadanganya Mwakuona kuwa atampeleka ngambo kufanya kazi kumbe anampeleka kwenye madanguro.

**Umuhimu wa Bi. Mtego**

- Ni kielelezo cha wanawake ambao huwahadaa wasichana wa shule na kuwapeleka katika madanguro kwa manufaa yao wenyewe
- Kupitia kwake tunapata sifa za Mwakuona kuwa ni mwenye tamaa.
- Anaendeleza maudhui ya ukatili. Aliendeleza biashara ya ukahaba kwa watoto wa shule kwenye jengo la Chengaways

**MBINU ZA UANDISHI.**

**Tashbihi.**

★ Nyumba nyingi za kule zilijiinamia ovyo kwa uzee kama zinazoomba msaada kwa yeyote aliyeziona (uk92)
★ Mwakuona aliminywa na maisha mithili ya mjusi aliyebanwa na mchanja kuni katikati ya gome na gogo..(uk92).
★ Alikuwa msiri kama kaburi (uk 94)
★ Mwakuona alifurahi ghaya kwa kuandaliwa kama malkia kamili (uk 95)
★ Ngozi ilikuwa tepetepe kama ya mtoto mdogo (uk 95)

- ★ Dunia ni kama shamba la mahindi huzaa mahindi na vizimwili (uk 99)
- ★ Kalowa jasho chepechepe anahema kama njiwa anayekimbizwa na mwewe(uk 100)
- ★ Anatetemeka kama kifaranga aliyenyeshwa (uk100)

**TASWIRA.**

- ★ Kuta za nyumba zilijengwa kwa mabati makuukuu, kuandikwa kwa udongo, mahema makuukuu au hata katoni na karatasi (uk92)
- ★ Nywele za nduguze Mwakuona zilikuwa za hudhurungi huku miguu ikiwa myembamba kama ya korongo isiyojua viatu ila kutawaliwa na tekenya, imekaukiana na kuunga matege (uk 92)

**MSEMO.**

- ★ Kuzaa mwana sikazi Kazi ni kuulea(uk92)
- ★ Usimwage mtama penye kukuu wengi (uk94)
- ★ Mbwa hafi maji aonapo ufuo.

**NAHAU.**

- ★ Kuzipa taabu kidogo (uk93)
- ★ Alipiga moyo konde (uk96)

**METHALI.**

- ★ Kumtoa nyoka pangoni (uk95)
- ★ Hayakuhusu ndewe wala sikio (uk94)
- ★ Dari la mnyonge haliendi joshi (uk95)

**SITIARI.**

- ★ Chenga ways kumwachilia aende ni sawa na kujitia kitanzi (uk100)

**TANAKALI ZA SAUTI.**

- ★ Kalewa chepechepe (uk100)
- ★ Ngozi ikawa tepetepe (uk 95)

**MASWALI YA MAZOEZI**

1. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili changamoto wanazopitia watoto (alama 20)
   (a) Sabina
   (b) Ahadi ni deni

2 . "Wooooooh! Woooh! Joojo! Nimewakamata! Nimewafumania, wanafiki wakubwa nyie!"

a)Weka dondoo kwa muktadha wake (alama 4)

b)Eleza mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili (alama 4)

c)Jadili sifa na umuhimu wa msemaji (12)

2. Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya; Msiba wa kujitakia na Kifo cha Suluhu (alama 20)
3. Kwa kurejelea hadithi ya Kila Mchezea Wembe, eleza madhara ya pombe kwa jamii (alama 10)
4. *Hadithi ya Pupa:* "Dunia ni kama Shamba huzaa maindi na vizimwili!"

(a)Eleza muktadha wa maenno haya (alama 4)

(b)Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa katika muktadha huu (alama 2)

(c)Eleza wasifu wa mzungumzaji wa maneno haya (alama 6)

(d)Jadili maudhui ya elimu kama yanavyojitokeza katika hadithi hii (alama 8)

4. "*This attitude of voting for the son or daughter of your community is old-fashioned because if he does not have better policies, you will continue to suffer under his leadership.*"

(a)Weka dondoo kwa muktadha wake (alama 4)

(b)Jadili mtindo kwenye dondoo hili (alama 4)

(c)Jadili maudhui yoyote sita yanayojitokeza kwenye hadithi hii (alama 12)

5. “Ubahimu unaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake. Jadili ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya ‘Nipe Nafasi’ (alama 10)